Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI

**Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 15 Februari, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma Dua*

## HATI ILIYOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):**

Taarifa iitwayo "*The Monetary Policy Statement Review July to December, 2007*".

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 130

**Kuigawa Wilaya ya Nzega**

**MHE. TEDDY KASELLA-BANTU** aliuliza:-

Kwa kuwa, nilipoapishwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Bukene, niliandika barua kuomba Bukene iwe Halmashauri na pia iwe Wilaya pekee, kwani ina sifa zote zinazotakiwa kuwa Wilaya/Halmashauri inazo. Pia; na kwa kuwa, katika mkutano wetu mmojawapo wa *RCC Tabora* Mheshimiwa Lucas Lumambo Selelii Mbunge wa Nzega alieleza kuwa hatua zote zilishapitishwa ipasavyo, kilichobaki ni fedha za kugawa Wilaya/Hamashauri ya Nzega:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa, sasa ni wakati muafaka kugawa Wilaya ya Nzega na kuwa na Wilaya za Nzega na Bukene?

(b) Kwa kuwa, sera ni kupeleka huduma na maendeleo karibu na wananchi; na kwa kuwa, Halmashauri ya Nzega ina Kata 37 na ziko mbalimbali sana. Je, Serikali haioni kwamba, kuna haja ya kuigawa Halmashauri ya Wilaya ya Nzega ili ziwe mbili, yaani Halmashauri ya Nzega na Bukene?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Teddy Kasella-Bantu, Mbunge wa Bukene, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, uanzishwaji au ugawaji wa maeneo mapya ya kiutawala hapa nchini unatawaliwa na Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 (Mamlaka za Wilaya) na Sheria Na. 8 (Mamlaka za Miji) za mwaka 1982 na Sheria ya Taratibu za Uanzishwaji wa Mikoa na Wilaya Na. 12 ya mwaka 1994.

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa suala la kugawa Wilaya ya Nzega na Bukene kuwa Wilaya mbili lilijitokeza kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa wa Tabora *(RCC)* kilichokaa tarehe 5 Oktoba, 2007. Kikao hicho kilielekeza Uongozi wa Wilaya ya Nzega kuanza mchakato huo katika ngazi ya Halmashauri ili uweze kupata baraka za Baraza la Madiwani, baadaye kuwasilishwa katika Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa. Maombi hayo yakipitishwa na Mkoa ndipo yawasilishwe kwa Waziri Mwenye Dhamana ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pale atakapoona inafaa baada ya kufanya uchambuzi yakinifu Mamlaka husika itashauriwa kwa hatua zaidi. Uongozi wa Wilaya ya Nzega haujafanya huo mchakato kama kikao cha *RCC* kilivyoelekeza.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo zoezi la ugawaji wa maeneo mapya ya utawala huwa muafaka endapo Serikali inalo fungu la kuyajenga Makao Makuu ya Wilaya, Uanzishaji wa Halmashauri, gharama za uwekaji wa Miundombinu pamoja na watumishi. Hivyo, zoezi hili linahitaji kiasi kikubwa cha fedha. Lakini kama lilivyo lengo la Serikali la kusogeza huduma karibu na wananchi, Serikali itaendelea kufanya zoezi hili kwa awamu kulingana na uwezo. *(Makofi)*

(b) Mheshimiwa Spika, uanzishwaji wa Halmashauri za Wilaya unao mchakato ambao unatakiwa kufuatwa. Halmashauri za Wilaya huanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sheria ya Serikali za Mitaa ya Mamlaka ya Wilaya Na. 7 ya Mwaka 1982 imempa Waziri Mwenye Dhamana na Serikali za Mitaa, Mamlaka ya kuanzisha Halmashauri, baada ya kushauriana na Rais. Kwa msingi huo Halmashauri ya Wilaya ya Nzega inapaswa kujadili suala hili katika vikao vyake na kupitisha azimio na kulipeleka katika Kikao cha Ushauri cha Mkoa wa Tabora. Taarifa hiyo ikitumwa Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI itafanyiwa kazi na Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa atatoa uamuzi kulingana na mazingira yatakayokuwepo.

Namwomba Mheshimiwa Mbunge awasiliane na Halmashauri yake kufuata utaratibu huo nilioeleza.

**MHE. TEDDY KASELLA-BANTU**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. La kwanza, kwa kuwa tulipokuwa kwenye Mkutano wa RCC Tabora ilielezwa kwamba habari hizi ziko tayari kwenye hatua za mwisho kama nilivyoeleza katika swali la msingi. Tukakubaliana kwamba wafuatilie Makao Makuu kama hiyo barua ipo na kama haipo kwa nini haipo kwa sababu tayari ilishafikishwa kwenye maamuzi hayo.

Kwa kuwa kila mara swali linakuwa fedha na kwa kuwa sasa hivi tumezungumza tumeona fedha nyingi zinakwenda kwenye Kampuni Hewa RICHMOND kwa hiyo zipo. Je, sasa Waziri ananiambiaje katika kutekeleza angalau moja Wilaya/Halmashauri ya Bukene?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA):** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza. Barua hiyo au mchakato mzima haujatufikia katika Ofisi yetu. Sisi tulichowashauri au Mkoa ulivyoshauriwa ni kufuata mchakato kuanzia ngazi ya chini. Kwa sababu kuna mambo mengi, kuangalia idadi ya watu lazima waeleze, Kata, mipaka lazima waielezee bayana.

Wakishaieleza na vikao vya Madiwani wakishakubaliana kwa sababu kule chini ndiko kwenye matatizo. Wanakubaliana kwamba kipande hiki au Kata hizi zinakwenda upande huu na hizi zinakwenda upande huu ndio mchakato wenyewe, bado haujafanyika.

Kwa hiyo, amesema liko katika ngazi ya Wilaya, wakishakubaliana kule ndipo watakapoleta kwenye Kikao cha *RCC* tena na baadaye kuleta kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa yaani (TAMISEMI). Lakini mpaka sasa hivi mchakato huu haujakamilika kwa Wilaya hii. Zipo Wilaya nyingine ambazo zimeleta, lakini bado huo mchakato haujakamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la fedha katika bajeti iliyopita mwaka jana hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya ugawaji wa Wilaya au Halmashauri yoyote. Fedha zilizotengwa ni kwa ajili ya zile Wilaya mpya zilizoanzishwa na Halmashauri mpya zilizoanzishwa. Kwa hiyo labda kwa mwaka huu tutalipa kipaumbele hilo suala la ugawaji wa maeneo ya Utawala ili tujiandae kwa ajili ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa mwaka 2009. (*Makofi)*

**MHE. JUMA H. KILLIMBAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali dogo moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, matatizo yaliyosemwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega yanafanana kabisa na Halmashauri ya Wilaya ya Iramba. Katika majibu yake Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu amesema zipo hatua zinazopaswa kufuatiliwa ili kupata sifa ya kupata Halmashauri ya Wilaya. Kwa kuwa Wilaya ya Iramba imetimiza yale masharti yote aliyoyasema kuanzia vikao vya Halmashauri yenyewe, *RCC* na hadi

kuleta muhtasari kwake yeye Ofisi ya Waziri wa TAMISEMI na hata Waziri Mkuu. Je, ni lini sasa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba itagawanywa kuwa na Halmashauri mbili ile ya Iramba Magharibi na Iramba Mashariki?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli maombi ya Wilaya ya Iramba kugawanywa katika Wilaya mbili yametufikia Ofisini kwetu na mpaka sasa hivi kuna Wilaya 35 ambazo zimefikisha maombi katika Ofisi yetu na sisi tumeshaweka kwenye mpangilio na kuangalia vigezo ambavyo vinatakiwa katika uanzishwaji wa maeneo ya kiutawala.

Kama nilivyosema kwamba tatizo kubwa ni fedha. Zipo Wilaya ambazo zinakidhi kabisa vigezo vya kuanzishwa kwa Wilaya mbili. Lakini tunaangalia kwa mwaka huu kwamba kama hali inaruhusu tutaweza kuzigawa hizo Wilaya kwa awamu kulingana na vigezo ambavyo vipo ambavyo tumejiwekea sisi wenyewe.

Na. 131

**Kuunganisha Baadhi ya Vijiji Kurahisisha Huduma**

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania ni nchi moja, na ili kuwafikia watu kwa urahisi kwenye baadhi ya maeneo ya nchi yetu ni vema baadhi ya maeneo hayo yakaunganishwa:-

(a) Je, kwa nini Kijiji cha Tanganyika (Kilombero) kisingeunganishwa kiutawala na vijiji vya Njombe ili kuweza kupata huduma kwa urahisi?

(b) Je, kwa nini Serikali isirekebishe mipaka ya baadhi ya maeneo na kuunganisha na maeneo ya Wilaya au Mikoa mingine?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mbunge wa Njombe Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Tanganyika kilichosajiliwa tarehe 24 Desemba 1975 na kiko katika Kata ya Masagati Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero. Kijiji hiki chenye Vitongoji vinne (4) kina Kaya 340 zenye jumla ya wakazi 2,181 ambao shughuli yao kubwa wanazozifanya ni kilimo ikiwa ni pamoja na kilimo cha matunda hususan machungwa. Aidha, wananchi wa Kijiji hicho wanajishughulisha na ufugaji wa nyuki ikiwa ni shughuli mojawapo ya kujiongezea kipato.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria za Serikali za Mitaa namba 7 ya Mwaka 1982, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero ndiyo iliyohusika na mchakato wa kuanzishwa kwa Kijiji cha Tanganyika. Katika kijiji hicho kuna huduma na juhudi zinazoendelea kutekelezwa kama ifuatavyo:-

**1. Afya:** Zahanati moja inayoendeshwa na Kanisa la Kilutheri, Dayosisi ya Ulanga Kilombero. Kwa upande wa Serikali, Halmashauri ya Wilaya inao mpango wa kujenga zahanati ili kuongeza huduma za afya Kijijini hapo.

**2. Elimu:** Kijiji kina Shule ya Msingi moja kwa kuungana na vijiji vingine wamejenga Sekondari moja iliyoanza mwaka 2008.

**3. Maji:** Uimarishaji wa huduma ya maji safi, salama na usafi wa mazingira kupitia programu inayogharamiwa na Benki ya Dunia kwa hiyo suala la maji nalo linapewa kipaumbele.

**4. Barabara:** Ujenzi na ukarabati wa barabara yenye urefu wa kilometa 15 inayounganisha Kijiji cha Tanganyika na Kijiji cha Taweta ambako ni Makao Makuu ya Kata ya Masagati imefanyiwa ukarabati na kutumika kwa kipindi cha mwaka mzima.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero inatambua kuwepo upungufu wa huduma mbalimbali katika Kijiji cha Tanganyika na vijiji vingine vya Kata ya Masagati. Upungufu huo hautokani na Kijijji hicho kuwa mbali na Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya hiyo bali ni kutokana na ufinyu wa Bajeti.

Aidha, Halmashauri ya Wilaya inaendelea kila mwaka kuandaa na kutekeleza mipango na Bajeti kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma katika vijiji vyake vyote 81 kikiwemo Kijiji cha Tanganyika. Hata hivyo Ofisi yangu haijapokea taarifa yenye pendekezo la kuunganisha kiutawala Kijiji cha Tanganyika na vijiji vingine vya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe.

(b)Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Namba 7 na Namba 8 za Mwaka 1982, Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa anayo Mamlaka ya kuanzisha eneo jipya la utawala kama Kijiji, Wilaya, Mji na Manispaa ikiwa ni pamoja na kurekebisha mipaka ya maeneo yaliyopo na yatakayoanzishwa. Katika kutekeleza maelekezo hayo ya kisheria, Waziri atapashwa kupata ushauri kutoka Mamlaka zilizopo ikiwa ni pamoja na Sekretariati za Mikoa husika. Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI imekwisha kutoa maelekezo kwa uongozi wa Mikoa kufanya vikao vya pamoja ili kuandaa mapendekezo ya kuunganisha baadhi ya maeneo yao ikiwa ni pamoja na uundaji wa Mikoa mipya.

Mheshimiwa Spika, lengo la kuweka mipaka ni kukidhi mahitaji ya Serikali ya kiutawala na pia kuwezesha upatikanaji wa huduma mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa urahisi. Hata hivyo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa mipaka ya kiutawala haiwazuii wananchi kupata huduma kutoka upande mwingine wa Mamlaka ili mradi wananchi hao wanazingatia Sheria za Mamlaka ambayo huduma hizo hupatikana.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA**: Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri wa majibu mazuri. Tanganyika, hiki kijiji ni majirani zangu wakati wa mvua wanapata huduma zote Njombe. Sasa nauliza swali hili bila ya kuongea na wenzangu wanaosimamia maeneo hayo kwa sababu ni tatizo la Kitaifa.

Mheshimiwa Spika, ukitoka Njombe kuelekea Mbeya kuna kijiji kinaitwa Kiguru kiko chini ya Wilaya ya Makete, lakini inabidi upite mara tu ukimaliza Iringa unaingia Mbeya Igawa, ukimaliza Igawa pale mbele tena unaingia Kimani, Iringa. Ukimaliza Kimani na Kifumbe unaingia Mbeya ndio uende Mbeya ukaingie Tukuyu ndio ukafike Kiguru. Kutokana na uzoefu wa kuunda miji na Waziri Mkuu analijua hili kwamba wakati mwingine *initiative* haitoki kule chini mnasubiri juu huku hawaleti. Kwa hiyo, wameamua kwamba iwe kutoka pande zote kwamba pendekezo la kubadili kitu au mpaka au kijiji au mji linaweza likatoka kwa Serikali Kuu. Je, haoni kwamba njia hii nayo ingetumika katika kutekeleza hili ninaloliomba hapa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**: Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi kwamba Mamlaka husika yaani Halmashauri ya Wilaya ya Njombe na Halmashauri ya Wilaya Kilombero kati ya Wilaya hizo hamna Wilaya yoyote ambayo imeomba kwamba kijiji hicho kihamishiwe upande wowote. Kwa hiyo, mimi ninachoona ingekuwa ni vyema tuwasiliane na pande zote mbili kama kutakuwa na ulazima wa kukihamisha hicho kijiji kwenda Njombe au vinginevyo tuwasiliane na Mamlaka husika ili tuone kwamba je wananchi wenyewe wako tayari kuhamia Njombe au kubaki katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero.

Na. 132

**Kukarabati Jengo la Polisi la Wilaya ya Nkasi**

**MHE. PONSIANO D. NYAMI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Jengo la Polisi la Wilaya ya Nkasi liliwekewa jiwe la msingi mwaka 1983 na kwamba mpaka sasa jengo hilo halijafunguliwa na limeanza kuchakaa:-

Je, ni lini jengo hilo litakarabatiwa kwa kupakwa rangi, kukamilisha matengenezo madogo madogo na kisha kufunguliwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mbunge wa Nkasi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, jengo la Makao Makuu ya Polisi ya Wilaya ya Nkasi lililoko Namanyere ni jengo kubwa na la kisasa ambalo linakidhi mahitaji ya kuwa Kituo cha Polisi. Jengo hilo liliwekewa jiwe la Msingi na Mheshimiwa Salim Ahmed Salim wakati huo akiwa Waziri Mkuu mnamo tarehe 03 Julai, 1985. Kwa sasa jengo hilo linatumika kwa shughuli za Polisi ingawa halijafunguliwa rasmi na limeanza kuchakaa kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge hivyo kuhitaji kufanyiwa matengenezo.Ni nia ya Serikali kuona kwamba majengo yote ya Ofisi na makazi ya Askari Polisi kote nchini yanakuwa katika hali ya kuridhisha.

Hata hivyo azma hiyo nzuri ya Serikali imekuwa ni vigumu kutekelezwa katika wakati muafaka kutokana na mahitaji makubwa ya Ofisi na nyumba za kuishi Askari hapa nchini na ufinyu wa bajeti ya maendeleo ya Wizara inayotengwa kwa ajili ya Jeshi la Polisi kila mwaka. Jeshi la Polisi litaendelea kutenga fedha kutoka katika bajeti yake ya kila mwaka kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za kuishi Askari na vituo vya Polisi kikiwemo Kituo cha Polisi Wilaya ya Nkasi.

**MHE. PONSIANO D. NYAMI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru niulize maswali mawili ya nyongeza. Tangu mwaka 1983 hadi leo ni miaka 25 iliyopita. Jengo halijakamilika vizuri ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kulimalizia jengo hili kikamilifu hata baada ya miaka 25 kupita halijakamilika, hivi dhamira ya Serikali ipo kweli hapo kulimaliza?

Swali la pili. Kwa nini Makao Makuu ya Polisi waliamua kuzuia kufunguliwa kwa jengo hilo mwezi Novemba 2007 alipokuja aliyekuwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Lowassa. Ni vigezo gani walivyovitumia kuzuia isifunguliwe wakati Wilaya tulikuwa tumeshakubaliana lifunguliwe na je mtakubaliana kwamba sasa Waziri Mkuu aliyopo anayetoka Mkoa wa Rukwa Mheshimiwa Pinda pale atakapokuwa anatembelea ndiye alifungue sasa?

**NAIBU WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimwa Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mheshimiwa Nyami kwamba Serikali inayo dhamira ya kuimarisha jengo hilo. Lakini kama tulivyoeleza katika jibu la msingi kwamba kutokana na ufinyu wa bajeti bado tunapata matatizo ya kumalizia ukarabati jengo hilo. Lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kila hatua zinachukuliwa kuhakikisha kwamba jengo hilo linakarabatiwa na linakuwa katika hali ya kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jibu lake la pili, kwa dhana hiyo hiyo kwamba nia yetu ni kulikarabati jengo lile. Ndiyo maana wakati Mheshimiwa Waziri Mkuu Edward Lowassa alipotembelea Mkoa wa Rukwa tuliomba lisifunguliwe rasmi jengo hilo kwa nia kwamba mara baada ya kulikarabati na kuwa la kisasa zaidi ili jengo hilo liweze kufunguliwa likiwa na hadhi nzuri zaidi. Kwa maana hiyo nataka nikubaliane naye kwamba nitamwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyopo aje kulifungua rasmi jengo hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la majengo ya Ofisi ya Jeshi la Polisi yaliyopo yanafanana na tatizo la Wilaya ya Bukombe. Wananchi wa Wilaya ya Bukombe walishirikiana sana na Jeshi la Polisi na hatimaye wakajenga majengo mazuri ambayo mpaka sasa hivi hayajakamilika. Je, Serikali wanaweza wakakubaliana na mimi wapate nafasi ya kuja kutembelea Wilaya ya Bukombe waone majengo ambapo Askari Polisi wanafanyia kazi lakini pia wapate nafasi ya kuongea na wananchi wa Bukombe?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ni sera ya Wizara sasa hivi kujenga na kuboresha majengo ya kuishi askari wetu. Ningependa kuwafahamisha au kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba tumekuwa na maongezi na *NSSF* na tumekwishapata kiasi cha shilingi 16 bilioni na awamu ya kwanza ya majengo inaanza.

Kwa hiyo, ningependa kumshukuru Mheshimiwa Mbunge Luhahula kwamba katika Wilaya yake kwa kuwa imeshaanza shughuli hiyo kwa hiyo tutajiunga nao na nilitaka kumwahidi kwamba mimi mwenyewe binafsi nitatembelea jimbo lake na hayo mengine tutayazungumza katika jimbo lake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa wale walioko kwenye *Gallery* huyu anayeshangiliwa sana hivi sasa ndiyo Naibu Waziri mpya katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mbunge wa Bukoba Mjini Mheshimiwa Balozi Kagasheki. (*Makofi)*

Na. 133

**Ugonjwa wa Ukoma**

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA** aliuliza:-

Kwa kuwa, ugonjwa wa ukoma umekuwepo nchini kwa miaka mingi, na kwa kuwa ugonjwa huo huwaathiri watu kwa kuwapotezea viungo vyao vya mwili hasa vidole vya mikononi na miguuni na hata kuharibu sura zao:-

(a) Je, kuna aina ngapi za ukoma, na zipi ni dalili na athari za ugonjwa huo?

(b) Je, ni Watanzania wangapi na wa mikoa ipi wameathiriwa zaidi na ukoma tangu nchi yetu ipate uhuru wake?

(c) Je, ugonjwa huo una tiba, na ni nini mwelekeo wa upungufu au ongezeko la wagonjwa kwa kila mwaka hapa nchini?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Spika, kuna aina mbili za ukoma kwa kuzingatia kiasi ambacho mgonjwa ameathirika kama ifuatavyo:-

*1.Paucibacillary (PB) type*: Hii ni pale ambapo mgonjgwa ana baka moja hadi mabaka manne kwenye ngozi yasiyo na uwezo wa kuhisi na hakuna vifundo vyovyote vya mishipa ya fahamu vilivyovimba.

*2.Multibacillary (MB) type*: Hii ni pale ambapo mgonjwa ana mabaka matano au zaidi kwenye ngozi na kuna vifundo vya mishipa ya fahamu iliyovimba hususan kwenye mikono, miguu na usoni.

3.Kuwepo vijinundu kwenye mwili vyenye rangi ile ile ya ngozi bila kupoteza hisia.

Mheshimiwa Spika, zipo athari nyingi zinazosababishwa na ukoma na baadhi yake ni kama ifuatavyo:-

·Kuathiri ngozi na mishipa ya fahamu;

· Kukatika kwa viungo mbalimbali vya mwili hususan vidole vya mikono na miguu na; na

· Kusababisha ulemavu wa kudumu na hivyo kuchangia kwenye umaskini.

(b) Mheshimiwa Spika, idadi ya Watanzania walioathirika kwa ukoma kulingana na takwimu za Wizara kwa mwaka 206 ni jumla ya watu 3,481. Kati ya hao 3,450 walikuwa wapya na 31 ilikuwa ni marudio.

Aidha, watoto chini ya miaka 14 walikuwa 210. Katika uwiano wa kijinsia; wanawake walikuwa 1,481 na wanaume 2,000 au 1:14 Mikoa iliyoathirika zaidi ni Mtwara, Morogoro, Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Kigoma na Tanga.

(c) Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa ukoma una tiba kamili ya mchanganyiko wa dawa maalum aina tatu za mseto katika kidonge kimoja au *multi-drug therapy (MDT).* Dawa hizi zinapatikana katika hospitali zote, vituo vya afya vyote na baadhi ya zahanati za Serikali na Mashirika ya Dini, na dawa hizo zinatolewa bure kwa wagonjwa.

Ikumbukwe kwamba dawa hizi zinaua bakteria wa ukoma na hivyo kusimamisha ugonjwa usiendelee, lakini dawa hizo hazina uwezo wa kuondoa ulemavu, kama upo tayari.

Mheshimiwa Spika, mwelekeo wa ugonjwa huo hapa nchini, ni kwamba umepungua sana. Miaka ya 1980 kulikuwa na wagonjwa wapya zaidi ya 30,000 kila mwaka; na hivi sasa idadi hiyo imepungua hadi chini ya wagonjwa 3,500 kwa mwaka.

Kwa taarifa tu, tangu mwaka 2006 Tanzania imefikia lengo la Kimataifa la kutokomeza ukoma yaani mgonjwa mmoja au chini kwa kila wananchi 10,000 (1/10,000).

**MHE. MASOLWA COSMAS MASOLWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa kuna baadhi ya watu walioathirika na wamekuwa ombaomba na kuzurura mijini. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia hao watu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba kuna baadhi ya wagonjwa ambao wameathirika na kupata ulemavu wa ugonjwa wa ukoma Serikali inazo kambi ambazo inawatunza baadhi ya wagonjwa hawa kwa hiyo wanapata huduma zote ambazo zinastahili katika zile kambi. Lakini vile vile napenda niseme kwamba wagonjwa wa ukoma ni kama wagonjwa wengine, tukumbuke kwamba wanahitaji msaada wa jamii na hawahitaji kunyanyapaliwa. Ningependa kusisitiza kwa wananchi kama jamii mwenzetu akipata tatizo hili tuendelee kumsaidia na tuweze kumsaidia yale mahitaji ya kawaida.

Na. 134

**Chanjo za Kimataifa za Kinga ya Afya**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa upo utaratibu wa Kimataifa wa afya wa kudhibiti magonjwa mbalimbali kama vile ndui, kolera, Homa ya manjano – *yellow fever* n.k. kwa njia ya chanjo za Kinga za muda maalum.

(a)Je, ni Magonjwa yapi ambayo bado chanjo za kinga za afya kwa Watanzania wanaosafiri nchi za nje zinahitajika?

(b)Je, kuna maendeleo yoyote katika utafiti wa kupta chanjo ya kinga ya UKIMWI duniani?

**NAIBU WAZ IRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo kwanza napenda kutoa maelezo mafupi ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chanjo hutolewa kwa watu ili kuwajengea uwezo wa kujikinga na magonjwa mbalimbali, kuzuia magonjwa kuenea kudhibiti na hata kutokomeza kabisa baadhi ya magonjwa. Kwa mfano, ugonjwa wa ndui umetokomezwa duniani kwa kutumia chanjo.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa kuna mikakati ya kimataifa chini ya Shirika la Afya Duniani (*WHO*) ambayo nchi wanachama zimeridhia kuitumia katika kudhibiti magonjwa mbalimbali ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza. Hata hivyo nchi yoyote inao uhuru wa kuweka masharti ya chanjo dhidi ya ugonjwa fulani kwa wasafiri wanaoingia nchini mwao. Magonjwa ambayo bado Watanzania wanaosafiri nchi za nje wanashauriwa kupata chanjo ni ugonjwa wa homa ya manjano na homa ya uti wa mgongo.

Chanjo ya ugonjwa wa uti wa mgongo inahitajika kwa watanzania wanaosafiri kwenda Saudi Arabia ambapo chanjo ya ugonjwa wa manjano inahitajika kwa Watanzania wanaosafiri kwenda Afrika ya Kusini na nchi nyingine zinazohitaji uthibitisho wa kupata chanjo hiyo kwa wasafiri wa kimataifa.

(b) Mheshimiwa Spika, kuhusu maendeleo ya kupata chanjo ya kinga ya Ugonjwa wa UKIMWI, juhudi zinafanyika kitaifa na kimataifa kwa ushirikiano wa wataalam mbalimbali. Aidha nchini Tanzania majaribio ya chanjo ya ugonjwa wa UKIMWI yanaendelea kufanyika katika Chuo Kikuu cha Sayansi za Afya Muhimbili kwa kushirikiana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (Kliniki ya Makuti) na Kituo cha Utafiti cha Mbeya. Mtu wa kwanza kufanyiwa majaribio hayo alipatiwa chanjo hiyo tarehe 20 Februari, 2007 na mpaka sasa watu 20 tayari wamekwishajitolea kufanyiwa majaribio ya chanjo hiyo. Wakati ufuatiliaji unafanyika kwa watu waliojitolea kufanyiwa majaribio ya chanjo hiyo, michakato mbalimbali ya kisayansi inaendelea ili kupata chanjo kamili ya ugonjwa huu kwa kushirikiana na wanasayansi mbalimbali wa kimataifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi zinazoendelea katika mapambano ya kuzuia na kudhibiti UKIMWI nchini, Serikali inazidi kuunga mkono kauli ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete kwamba Tanzania bila UKIMWI Inawezekana.

Naomba nitumie fursa hii kupitia Bunge lako Tukufu kuwaomba wananchi kwamba waendelee kujilinda ili kujiepusha na kupata maambukizi ya UKIMWI na kwa wale ambao tayari wameambukizwa wajilinde kuepuka maambukizo mapya na pia wasiambukize wenzao.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO**: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa imedhibitika kwamba chanjo ya homa ya manjano ya *yellow fever* bado inahitajika South Africa na hata baadhi ya nchi za Asia na kwa kuwa wako wasafiri wengi wanaokwenda maeneo hayo; na kwa kuwa chanjo inayoletwa inaletwa katika vipimo vya kumi kumi au dozi za watu kumi kumi na inakuwa vigumu kupata chanjo ile akienda peke yake mpaka atafute wenzake. Je, si vizuri jambo hilo likarekebishwa ili kupunguza vishawishi ambavyo vinavyoweza kujenga hata rushwa ya mtu asipigwe sindano lakini aweze kupigiwa muhuri na kuondoa?

Pili, kwa kuwa imeonekana kwamba kuna majaribio ya dawa za chanjo ya UKIMWI hapa nchini Je, Wizara inawaambia nini wananchi wanaopenda kujitolea kutumiwa kama watu wa majaribio katika chanjo hizo?

**NAIBU WAZ IRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, chanjo hizi kwa wale wanaosafiri wanapaswa wapate chanjo pale inapobidi waende kwa maana hiyo nashauri kwamba kwa sababu chanjo hizi zina utaratibu wake wa kuzihifadhi inapobidi mwananchi apate chanjo ili aweze kusafiri na kuzuia kupata ugonjwa kule anapokwenda. Kwa maana hiyo suala la kwamba dozi zinakuja kwa watu kumi kumi mimi napenda nitoe wito kwamba inapodisi mwananchi apate chanjo wataalam watoe chanjo kwa kadri inavyowezekana na taratibu za uhifadhi wa dawa ili chanjo hii iweze kutolewa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni kwamba kama nilivyosema majaribio ya dawa hizi kwa kupata chanjo watu wanajitolea kwa hiyo kwa sababu kama inavyojidhihirisha wanajitolea hakuna malipo yoyote ambayo analipwa.

**MHE. ZUBEIR ALI MAULID:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii kwa kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa haya mataifa tunaishi kwa mashirikiano. Je kwa nchi zile ambazo tunakwenda na tunaombwa tuwe na chanjo wale raia wa nchi zile wanapokuja hapa Tanzania nasi huwa tunaomba kuona hizo za homa ya manjano pamoja na uti wa mgongo kwa wale wanaotokea Saudi Arabia?

**NAIBU WAZ IRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba ni sheria kama unataka kwenda nchi ambayo tuna mahusiano uwe umechanjwa na vile vile nchi yetu wanapoingia wageni na wenyewe kama kuna hitajika kufanyiwa chanjo basi ni lazima wanaokaguliwa kabla ya kuingia nchini kabla hawajaingia nchini kwa sababu utaratibu huu upo katika viwanja vyetu vya ndege kwa hiyo wanachekiwa na kama hakutimiza masharti basi hatua zinachukuliwa kumwelekeza jinsi gani afanye kabla yajaruhusiwa nchini.

**MHE. DR. ALI TARAB ALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa kuna habari ya kwamba chanjo ya UKIMWI ambayo imekuwa ikifanyika Marekani, Haiti na nchi nyingine imeleta athari mbaya kwa wale washiriki wa chanjo hiyo *toxic effect*. Je, kuna uhakika gani kwamba athari hizo hazitakuwepo kwa washiriki wa chanjo yetu hapa?

**NAIBU WAZ IRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, utafiti unaofanywa unafanywa kitaalam kwa maana hiyo kwa sababu unafanyika kitaalam katika taasisi ambazo zina wataalam waliobobea nina matumaini kabisa hakuna tatizo lolote linaweza likatokea ndiyo maana tunafanya utafiti huu.

Na. 135

**Zao la Mbata**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. JANETH B. KAHAMA)** aliuliza:-

Kwa kuwa zao la mbata linalotokana na minazi limerudi nyuma sana kama zao la biashara:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha kuwa zao hilo linafufuliwa katika Mikoa ya Pwani yote na kulifanya liwe miongoni mwa mazao makuu ya biashara Tanzania?

(b) Kwa kuwa, minazi ya asili ni mirefu na husababisha ajali mbalimbali kwa watu na hata wakwezi wa minazi wenyewe kuanguka hata wengine kupoteza maisha yao na kuumia. Je, Serikali ina mpango gani au imefanya utafiti gani wa kupata njia bora na au vifaa halisi kwa ajili ya kuangulia nazi ili kuepusha ajali pia kurahisisha uvunaji salama wa zao hilo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Janeth Bina Kahama, Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba zao la mbata linalotokana na minazi limepungua sana kama zao la biashara hususan kuanzia miaka ya 1980. Utafiti uliofanywa na Mpango wa Taifa wa Kuendeleza Minazi ulibaini kwamba sababu kubwa za kushuka kwa uzalishaji wa nazi ni pamoja na:-

(i) Athari za wadudu waharibifu kama vile chonga na mbu wa minazi.

(ii) Ugonjwa wa kunyong'onyea kwa minazi *(lethal disease).*

(iii) Bei ndogo ya mbata ikilinganishwa na bei ya nazi za kawaida.

(iv) Kutokuwepo chombo maalum cha kusimamia masuala ya mbata.

Mheshimiwa Spika, Mpango mahsusi wa kufufua zao la minazi ni kuendeleza utafiti wa zao hili; katika nyanja mbalimbali:-

(i) Uzalishaji wa mbegu bora zenye uwezo wa kustahimili magonjwa, mashambulizi ya wadudu na enye kutoa mazao mengi.

(ii) Kuendelea na utafiti ambao umewezesha kubaini mbinu husishi za kuwadhibiti wadudu na mbu wa minazi.

(iii) Kuendelea na utafiti wa kutokomeza ugonjwa wa kunyong'onyea.

(iv) Kuendelea kushauri upandaji wa minazi asili *(East African tall)* kwa kuwa ina sifa ya kuhimili upungufu wa maji kuliko minazi mifupu au chotara.

(b) Mheshimiwa Spika, Wizara yangu haijawahi kufanya utafiti wowote juu ya njia bora ya kuangulia nazi. Hata hivyo uzoefu umeonyesha kwamba nchi nyingine kama vile India, Philippines na Indonesia njia rahisi na salama ya kuangua nazi ni utumiaji wa fito *(harvesting poles)* zinazotokana na aina maalum ya minazi, badala ya kutumia wakwezi. Wizara yangu itaangalia uwezekano wa kuanzisha utaratibu wa teknolojia hiyo kwa wakulima wa minazi nchini.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri naomba kuuliza maswali madogo mawili. Kwa kuwa miaka ya 1980, Wizara ya Kilimo iliandaa miche ya minazi chotala na ikasambaza; sasa naomba kuuliza kwamba ilileta mafanikio gani au tulikwamia nini na hiyo minazo chotala.

Swali la pili. Kwa kuwa Chuo cha Utafiti cha Ukiriguru kipo maeneo ya Kanda ya Ziwa. Je, Serikali sasa haioni chuo hiki kikatumiwa katika kufanya utafiti ambayo itasambazwa katika Mikoa hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, tangu mwaka 1979 mpaka mwaka 2004 tulikuwa na chombo kinachoitwa *National Coconut Development Program,* chombo ambacho kilikuwa kinashughulikia kuangalia uendelezwaji wa suala hili la minazi. Chombo hiki kimefanya kwa miaka 26 na tafiti zimefanyika mbalimbali wametafiti takribani mbegu 70 za minazi na kugundua kwamba *East African Tall* ndiyo ambayo inastahimili magonjwa inatoa nazi nyingi kati ya nazi 30 mpaka 40 kwa mti mmoja. Kwa hiyo, ndiyo mbegu ambayo ilionekana ndiyo nzuri zaidi kuliko ile ya chotara au ile mifupi. Kwa hiyo, mpaka sasa hivi sisi tunasisitiza wakulima wetu wachukue mbegu hizi za minazi hii inayoitwa East Africa Tall ambayo imebuniwa na kuzalishwa na kituo chetu cha kuendeleza tafiti za kilimo Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la chuo hiki cha Ukiriguru, tutaangalia uwezekano huo lakini kwa kufuata aina ile ya minazi ambayo ni mizuri zaidi ambayo inastahimili magonjwa na kuzaa sana kama niliyosema ya *East African Tall* ndiyo imeonekana inafaa zaidi.

**SPIKA:** Naona wanaouliza wote sio maeneo yanayolimwa nazi. Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o. (*Kicheko*)

**MHE. LEDIANA M. MNG'ONG'O**: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa maeneo ya Musoma Vijijini kama maeneo ya Bukima, Majita na maeneo ya Ludewa nazi zimekuwa zinalimwa kama zao la kienyeji. *(Makofi)*

Je, Wizara ipo tayari kufanya utafiti na kujua kwamba nazi zinalimwa kule na kuweza kuhamasisha wananchi nazi kama zao la biashara?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika iko tayari kuja maeneo hayo kama zao la biashara.

**MHE. DR. SAMSON F. MPANDA**: Mheshimiwa Spika, naomba kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri hii Bodi ya Mazao mengineyo mpango wake ukoje mpaka sasa hivi kwani mbata, mboga mboga na vitu vingine vingeweza kuchukua nafasi yake katika kufanya shughuli hizo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, labda nisema tu kwamba zao la mbata miaka ya 1970 mpaka 1986 ilikuwa inasimamiwa na chombo kinachoitwa *GAPEX*. Chombo kile kilipoacha kushughulikia mazao haya yakiwemo iliki na mengine zao hili likawa halina chombo chochote cha kuweza kulisaidia.

Kwa hiyo, sasa hivi Bodi ambayo itasaidia mazao yote ni Bodi ya Mazao Mchanganyiko ambayo tulishaahidi hapa Bungeni kwamba tunaishughulikia na Waraka upo tayari. Lakini Bodi hiyo haiwezi ikaanzishwa kabla ya Sera za Masoko haijakamilika kutoka Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko.

Wizara hiyo sasa hivi iko katika hatua kubwa kabisa sera hii ya masoko na pindi watakapomalizia na Wizara yetu itakuwa tayari kuunda Bodi hii ya Mazao Mchanganyiko yakiwemo mahindi, maharage, vitunguu na kadhalika.

Na. 136

**Miradi ya Utalii wa Utamaduni**

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi 15 duniani zilizoteuliwa kunufaika na mradi wa *(UNWTO) Sustainable Tourism for Eliminating Poverty (ST-EP) Initiative*, na kwa kuwa Pangani na Saadani wamepewa dola za kimarekani 77,500 ili kuboresha miradi ya utalii wa utamaduni:-

(a) Je, kwenye kipindi cha mwaka 2006/2007 Pangani imenufaika katika miradi mingapi ya utalii?

(b) Je, katika mwaka 2007/2008 kutakuwa na miradi mingapi ambayo imeorodheshwa tayari?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Rished Abdallah, Mbunge wa Pangani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kwa mwaka 2006/2007 Wizara yangu iliwasilisha miradi Shirika la Utalii Duniani kuomba Ufadhili kupitia *Sustainable Tourism for Eradication Poverty (ST-EP Initiative).* Baada ya miradi hiyo ni ile ambayo tayari ilikuwa na msingi wa utalii wa utamaduni, ambapo ni Pangani tu iliyobahatika kupitishwa mwaka huo wa 2006/2007.

(a) Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Pangani imefaidika na Mradi wa Pangani – Saadani *Coastal Community Tourism*, Mradi ambao uliandaliwa kwa ushirikiano kati ya wataalam toka Wizara yangu. Shirika la Utalii Duniani (*UNWTO*) liliidhinisha mradi huo na kutoa fedha za utekelezaji wake ambao umeanza rasmi mwaka 2007/2008.

Kiasi cha fedha zilizopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huu ni *USD 77,500*. Mradi huu unategemewa kuwa wa miaka mitatu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2007/2008 Mradi wa *Pangani- Saadan Coastal Comuunity Tourism* utaendelea kutekelezwa. Mpango kazi (*work Plan*) wa utekelezaji wa mradi huu utajumuisha kazi zifuatazo:-

- Ujenzi wa *Tourism Information Centre* ambayo ni sehemu ya kupokelea wageni.

- Ununuzi wa samani za ofisi.

- Ununuzi wa kompyuta, *printer* na *scanner.*

- Ununuzi wa pikipiki kwa ajili ya usafiri wa mratibu wa mradi.

- Mafunzo mbalimbali yatatolewa kwa vikundi vinavyofanya biashara ya utalii au inayohusiana na utalii.

- Mafunzo yatatolewa kwa waongoza misafara ya utalii katika maeneo husika.

**MHE. MOHAMED RISHED ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, Bajeti ya mwaka 2007/2008 imebakia miezi minne

kufikia ukomo wake na hizi fedha zilizotolewa kwa ajili ya mradi huu wa Pangani hazijaanza kutekelezwa hakuna kinachoendelea na mimi ndiyo jicho lake kule Pangani. Je, anataarifa gani kwa sababu zipi mradi huu haujaanza?

Swali la pili, katika majibu yake amesema kwamba mpango huu wa kazi wa utekelezaji wa mradi ni wa miaka mitatu. Je, katika miaka miwili mingine zitatumika fedha hizi hizi au zitaongezewa fedha nyingine kwa ajili ya mradi huu?

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, misaada ya *ST-EP* ni miradi midogo midogo. Kwa hizi fedha zilizotolewa za dola 77,500 ni kwa ajili ya mradi mzima. Fedha zile ni fedha za wafadhili kwa hiyo si sehemu ya fedha za Bajeti ambazo zimepita na kwa sababu hiyo zitakapopokelewa zitatumika kwa wakati wote wa mradi bila kujali mzunguko wetu wa Bajeti.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa vijiji vingi vilivyo kando kando ya hifadhi na vile vilivyoko kando kando ya mapori ya akiba hazina barabara; na kwa kuwa wananchi hushindwa kufanya biashara nyingine yoyote ile na kulazimika kuingia porini kuwinda kwa maana ya kwenye hifadhi na mapori. Je, Serikali ina mpango gani sasa mahususi wa kuwatengenezea barabara wananchi hawa ili waweze kufanya shughuli nyingine za kiuchumi zaidi ya kuingia kwenye hifadhi na mapori ya akiba?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Ni kweli kwamba sehemu nyingi ambazo kuna vivutio vya utamaduni barabara zake hazipitiki kwa urahisi kwa sababu ya miundombinu vikiwemo vijiji mbalimbali na hasa sehemu za ufukweni za Pwani. Hata hivyo kwa sasa hivi tuko katika mipango tukishirikiana na Wizara ya Ardhi katika kuanisha maeneo ya namna hiyo ili na yenyewe yaanze kupimwa.

Na. 137

**Viwango Vipya vya Ada za Uwindaji**

**MHE. KAIKA S. TELELE** aliuliza:-

Kwa kuwa hivi karibuni Serikali iliongeza na kutangaza viwango vipya vya ada ya leseni ya uwindaji kwa kampuni zenye vitalu vya uwindaji wa kitalii; na kwa kuwa viwango hivyo vipya viliendelea kulalamikiwa na mengi ya kampuni husika kuwa bei hizo ziko juu mno:-

(a)Je, ni kampuni ngapi za uwindaji zinahusika na zoezi nchini?

(b) Je, tangu viwango vipya vya ada vitangazwe ni kampuni zipi zililipa na ni fedha kiasi gani?

(c) Kwa zile kampuni zitakazoghairi kulipa. Je, ni hatua zipi zitachukuliwa dhidi hayo hasa ikizingatiwa kuwa kwa ujeuri wao huo utaathiri Bajeti ya Serikali ya

2007/2008 pamoja na miradi ya wananchi ambayo ingetekelezwa kwa fedha za uwindaji wa kitalii katika maeneo ya vijiji inayozunguka vitalu hivyo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaika Telele, Mbunge wa Ngorongoro, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Uwindaji wa kitalii unaendeshwa na kampuni 54 katika vitalu 158 vilivyopo katika mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo ya wazi. Hivyo, ongezeko la ada za uwindaji wa kitalii (vitalu na wanyamapori) kama ilivyo katika tangazo la Serikali Na. 159 la tarehe 29/06/2007 linahusu kampuni zote 54 zenye kibali cha kuendesha uwindaji wa kitalii nchini. Tangazo la Serikali Na. 159 la terehe 29/06/2007 liliwafikia wadau rasmi tarehe 11/07/2007. Wakati huo baadhi ya kampuni zilikuwa zimeshalipia vitalu kwa kiwango cha ada za zamani zilizotumika msimu wa mwaka 2006 cha *USD 10,000.00* kwa kila kitalu.

(b) Pamoja na hayo kampuni 11 zimelipa nyongeza ya ada (ada za wanyamapori na vitalu) kikamilifu au sehemu yake ambapo *USD 622,540.00* zimekusanywa. Kampuni 42 mpaka sasa hazijajitokeza kufanya malipo. Kampuni zilizolipa nyongeza ya ada au sehemu yake ni kama ifuatavyo:-

*(i)* *Ortello Business Corporation (T) Ltd.* imelipa ada zote za wanyamapori na vitalu.

*(ii)* *Morogoro Hunting Safaris (t) Ltd.* na *Grumeti Reserves* zimelipa ada kamili za vitalu.

(iii) Kampuni ambazo zimelipia sehemu ya ada za wanyamapori waliowindwa ni; *Rana Tours Ltd, Northern Hunting Enterprises, Game Frontiers, Royal Frontiers, Eco Safaris, Intercon Adventure Safaris na Mwanautu & Co Ltd*. Kampuni za *Mwanauta & Co. Ltd na Bushman Hunting Safari Ltd* zimelipia kitalu kimoja kila mmoja kati ya vitalu viwili vinavyomilikiwa na na kila kampuni hizo.

(c) Kanuni ya 11 (2) (a) (iii) ya Kanuni za uwindaji wa kitalii za mwaka 2000 na marekebisho yake, inatoa Mamlaka kwa Mkurugenzi wa Idara ya Wanyamapori kuchukua hatua za kisheria dhidi ya Kampuni inayoshindwa kulipa ada stahili za Serikali. Hatua hizo ni pamoja na kuzifikisha kampuni husika mahakamani na kuzinyang’anya vitalu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua za awali, Wizara yangu imewaandikia wenye kampuni za uwindaji wa kitalii wote barua ya kuwataka walipe madeni yao. Aidha Wizara imefanya majadiliano na wawakilishi wa chama cha wenye kampuni za uwindaji wa kitalii (*Tanzania Hunting Operators Association (TAHOA)* kuhusu suala la ulipaji wa madeni ambapo makubaliano yamefikiwa kwamba utekelezaji wa malipo ufanyike kabla ya kumalizika kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwanza, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu ya ya kina.

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango gani wa kuyapongeza haya makampuni ambayo yamekubali kulipa moja kwa moja nyongeza ya ada hizi bila usumbufu wowote?

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa leseni za kampuni hizi zitakoma mwaka 2009; na kwa kuwa kuna hizi kampuni ambazo kwa njia moja ama nyingine ni kama zimekataa kuitikia huu wito wa Serikali wa nyongeza ya ada za leseni, je, Serikali haina mpango wa kusitisha leseni zao ifikapo mwaka huo?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, kuhusu Serikali ina mpango gani kupongeza makampubni yaliyolipa ada zao bila usumbufu, napenda kusema kwamba tumepokea ushauri wake huo na ni jambo ambalo tutakaa na kuliangalia tutafanyaje.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kuhusu hao ambao hawajalipa kabisa na kwamba Serikali tutachukua hatua gani ni kwamba makampuni ambayo hayajalipa kabisa hata senti tano ni makampuni saba. Makampuni hayo wana vitalu tisa. Wamelalamika kwamba vitalu vyao vya kuwinda, havina wanyama wa kutosha. Hata hivyo, tunayo Kamati Maalum inayohusika na kutoa vitalu na Kamati hiyo huwa inakaa mwisho wa mwaka wa uwindaji kuweza kutathmini maeneo mbalimbali yaliyowindwa, hali kadhalika ada zilizolipwa na wawindaji waliokuwa wanawinda wamefanya kitu gani na nani hawajalipa na wale ndio watatoa ushauri kwa Wizara hatua gani za kuchukuliwa. Kwa hali hiyo, ni kwamba hawa wote mwishoni mwa mwaka huu wa kuwinda ambao utakuwa kwenye mwezi Julai, washauri watakaa na kupendekeza yale ambayo wanaona Wizara ichukue hatua.

**SPIKA:** Waheshimiwa, mniwie radhi, muda hauturuhusu. Tunahamia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Mbunge wa Tumbe, Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan.

Na. 138

**Huduma ya TVT na RTD**

**MHE. SALIM ABDALLAH KHALFAN** aliuliza:-

Kwa kuwa RTD na TVT ni vyombo vya Taifa vya Habari vinavyotarajia kuwafikia wananchi wote nchini;

(a) Je, hadi sasa ni maeneo gani hapa nchini ambayo hayajafikiwa na huduma hizo za RTD na TVT?

(b) Je, Serikali ina mpango gani makini kuhakikisha vyombo hivyo vinawafikia Watanzania wote?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Salim Abdallah Khalfan, Mbunge wa Tumbe, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maeneo ambayo hadi sasa hayajafikiwa na huduma ya TvT kupitia mitambo ya kawaida ni Ruvuma, Iringa, Morogoro, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Shinyanga, Mtwara na Rukwa. Kwa upande wa Redio, karibu maeneo yote ya nchi yanafikiwa na huduma hiyo japokuwa yapo maeneo machache ambayo usikivu wake ni hafifu. Sababu za msingi za kutofika huduma hiyo ni pamoja na:-

Umbali wa urefu kutoka eneo ambalo mitambo ya kuongeza nguvu *(booster stations)* ilipo;

Uwezo mdogo wa mitambo ya kurushia matangazo;

Kukatika mara kwa mara kwa umeme katika maeneo husika;

Uchakavu wa mitambo; na

Hali ya hewa na jiografia ya maeneo husika (milima na mabonde).

(b) Mheshimiwa Spika, ili vyombo hivi viwili (RTD na TvT) viweze kuwafikia Watanzania wote, Serikali tayari imefunga mitambo ya *FM* katika Mikoa ya Dodoma, Arusha, Mbeya, Tabora, Kigoma, Mwanza, Bukoba, Musoma, Tanga, Lindi na Dar es salaam.

Aidha, fedha zitakapopatikana, Serikali inakusudia kujenga vituo na kufunga mitambo ya *FM* na Televisheni katika Miji Mikuu ya Mikoa iliyosalia ambayo ni Ruvuma, Morogoro, Kilimanjaro, Manyara, Singida, Shinyanga, Mtwara, Pwani, Rukwa na Iringa. Hatua itakayofuata itakuwa ni kuboresha usikivu katika maneo mengine yanayobaki.

Mheshinmiwa Spika, Serikali inakusudia pia kujenga mitambo ya *Radio FM* na Televisheni Tanzania Visiwani ili huduma hizo ziweze kupatikana kwa urahisi zaidi.

**SPIKA:** Mheshimiwa … looh, limenitoka kidogo hapo!

**MHE. ALI SAID SALUM:** Ali Said Salum!

**SPIKA:** Mheshimiwa Khamis, swali la nyongeza!

**MHE. ALI SAID SALUM:** Ooh!

**SPIKA:** Ali Khamis! Aah! Ali, swali la nyongeza!

**MHE. ALI SAID SALUM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi ili niulize swali moja dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa TvT ni Televisheni ya Taifa ambayo pamoja na shughuli nyingine inatakiwa itunze na iendeleze silka na utamaduni wa Mtanzania; na kwa kuwa sasa katika nchi yetu na hasa nyanja hizi za utandawazi, kumekuwa na taratibu za minenguo katika Televisheni zetu; na wakati huo, hiyo minenguo mingine inakuwa ni ya kupita kiasi jambo ambalo kwa kweli linakiuka hata mila zetu; je, isingekuwa vema kwa Televisheni ya Taifa ikaachia hii minenguo ikaonyeshwa kwenye Televisheni za binafsi kama *ITV*, *Star TV* na *Channel Ten* kuliko TV yetu ya Taifa ambayo kwa kweli wengi tunatizama na watu ambao tunawastahi?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye kwamba TvT ni Televisheni ya Taifa. Lakini, ni vizuri akaelewa kwamba dunia sasa hivi ni kama kijiji na dunia ya sasa hivi hakuna siri na TvT ni chombo ambacho kinaonyesha matukio mbali mbali ya Kitaifa. Kwanza, TvT inastahili kusifiwa kwa sababu ni Shirika ambalo linaonyesha umaarufu wa hali ya juu sana katika kuonyesha matukio mbalimbali nchini. Wote tutakubaliana na aliyoyazungumza lakini, ni dunia ya ushindani na hakuna siri. Kwa hiyo, suala la kusema kwamba TvT isionyeshe baadhi ya mambo, si sahihi, labda kama mambo yamekithiri, kuna Kamati Maalum ya Maudhui ambayo inatazama mambo ambayo hayastahili kuonyeshwa na hiyo ipo na inaendelea kufanya kazi. Kwa hiyo, cha msingi ni kuisifia TvT kwa kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yako, ninachukua nafasi hii kuwapongeza sana TvT katika matukio ya hivi karibuni. Yameonyeshwa matukio ya vurugu za Kenya, tumeona mpira wa *Finals* za *Africa Cup* ambayo haijapata kutokea. Kwa hiyo, ni chombo cha kusifiwa. *(Makofi)*

Na. 139

**Mlundikano wa Makontena Bandari ya Dar es salaam**

**MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO (K.n.y. MHE. MOHAMED H. MISSANGA)** aliuliza:-

Kwa kuwa yapo malalamiko mengi kuhusu mlundikano wa makontena ya mizigo bandarini Dar es salaam jambo ambalo linazorotesha ufanisi wa bandari uliokuwa umejengwa kwa muda mrefu na kusababisha wafanyabiashara wenye meli kupitisha mizigo yao kwenye bandari ya Mombasa; na kwa kuwa mlundikano huo pia umesababishwa na ukosefu wa vifaa vya kufanyia kazi katika Kitengo cha Makontena na uhaba wa nafasi ya kuhifadhi, kupakua na kupakia makontena katika kitengo hicho:-

(a) Je, tangu mwekezaji *TICTS* akabidhiwe kitengo cha makontena ni vifaa vya aina gani na idadi gani vya kupakia, kuhifadhi, kupanga na kupakia makontena vimenunuliwa?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kuwa eneo la *Container Terminal* linapanuliwa?

(c) Je, Serikali haioni kuwa ni vema kuiruhusu Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)* waanzishe kitengo kingine cha makontena ili kuondoa msongamano wa makontena na mizigo bandarini?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed H. Missanga, Mbunge wa Singida Kusini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, tangu mwekezaji *TICTS* akabidhiwe kitengo cha makontena tarehe 10 Septemba, 2000 hadi Januari, 2007, ameshanunua vifaa vifuatavyo:-

Kwa upande wa Vifaa vya kupakia, kupakua na kupanga amenunua *Rubber Tyre Gantry Cranes (RTG)*11, *Front Loader* 2 na *Forklift* 3.

Kwa upande wa Vifaa vya kuhamisha na kuhifadhi amenunua *Terminal Tractors* 16 na *Terminal Trailers* 15.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa vifaa katika utendaji kazi wa sughuli za bandari, ongezeko, kukua na ushindani katika biashara ya bandari kuna umuhimu wa kuwa na vifaa vinavyokidhi mahitaji ya wateja ili kuongeza ufanisi katika utendaji na kuvutia shehena zaidi. Mwekezaji *TICTS* katika kipindi cha kuanzia Januari, 2008 na mapema 2009, amepanga kuongeza vifaa zaidi. Aina ya vifaa na muda wa kuwasili ni kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa Vifaa vya kupakia, kupakua na kupanga amepanga kuingiza *Ship to Shore Crane (SSC)* 1, ambayo inatarajia kuingia ama mwishoni mwa mwaka huu au mwanzoni mwa mwaka ujao.

Vile vile *Rubber Tyre Gantry Cranes (RTGs*) 2, ambazo zinatarajia kuingia mwishoni mwa mwaka huu. *Reach Stakers* 2, katikati ya mwaka huu na zingine 2 mwishoni wa mwaka huu, *Mobile Harbour Crane* 1, inategemewa kuingia katikati ya mwaka huu na *Empty Container Handles* 2, ambazo vile vile zinategemea kuingia katikati ya mwaka huu.

Kwa upande wa vifaa vya kuhamisha na kuhifadhi anategemea kuleta *Terminal Tractors* 9 ambazo zinategemea kuingia mwishoni mwa mwaka huu.

(b) Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa mwezi Desemba, 2005, Serikali iliamua kuipatia *TICTS* gati namba 8, Yadi namba 8 na Ubungo *Inland Container Deport* kama njia ya kuwaongezea eneo la kontena. Hatua hii imeongeza uwezo wa kuhudumia meli nne kwa wakati mmoja na kuhifadhi kontena *(hold capacity)* kutoka *TEUs* 6,500 hadi *TEUs* 7,500 kwa siku. Aidha, Serikali imeruhusu kuvunjwa maghala yaliyokuwepo ndani ya Kitengo cha Kontena na shedi namba 8 kama hatua ya kuongeza eneo la Kitengo cha Kontena.

(c) Mheshimiwa Spika, kutokana na msongamano wa kontena na mizigo bandarini, ni kweli kuna umuhimu wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)*, kuruhusiwa uanzishaji kitengo kingine cha kontena. Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari imeanza mchakato wa kuanzisha kitengo kingine cha kontena. Aidha, Mamlaka inapanga kujenga magati mawili yaani gati Na. 12 na 13 kwa ajili ya kuhudumia meli za kontena kama hatua ya muda mfupi ya kuongeza uwezo wa kuhudumia shehena ya kontena na mizigo bandarini. Kwa sasa, Mamlaka inafanya uchambuzi yakinifu kwa kazi hii. Ujenzi huu umepangwa kufanywa katika utaratibu wa *Fast Track* ili ukamilike ndani ya miaka minne kuanzia mwaka 2008.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)*, tayari imeishanunua eneo lenye ukubwa wa hekari 19.6 sehemu ya Kurasini kwa ajili ya upanuzi wa Bandari ya Dar es salaam. Aidha, Mamlaka chini ya udhamini wa Benki ya Dunia katika kipindi cha 2007/2008, imepanga kufanya utafiti wa *Port Development Master Plan* kwa lengo la kubaini mahitaji ya uwekezaji wa muda mrefu katika bandari zote za Mwambao na za Maziwa.

**MHE. ATHUMANI S.M. JANGUO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninapenda niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa muda wa miaka saba mwekezaji ameweza kuleta *Rubber Tyre Gantries* na *Terminal Tractors;* hivi, hiyo ni *investment* ya kutosha kwa sababu *investment* inayotakiwa iwe katika *Ship to Shore Gantry Cranes* ambazo ndio inayoteremsha makontena; na ninaambiwa kwamba sababu ya huyu kuwekeza kidogo ni katika mkataba ule jukumu la uwekezaji bado ameachiwa *THA*; je, Serikali inaona hilo ni jambo la busara?

(b) Mkataba wa kwanza ulikuwa mwaka 2000 mpaka 2010, kabla kipindi hakijamalizika na utekelezaji ni mbovu, kwa nini Serikali imekubali kuongeza mkataba kwa miaka 15 zaidi? Je, Serikali itakuwa tayari kufuta huu mkataba wa pili na kuanza kutangaza tenda kwa wawekezaji wengine? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba katika mkataba wa *TICTS* na Serikali, kuna baadhi ya maeneo ambayo mwekezaji anatakiwa awekeze na mengine kwa maana ya ile miundombinu ya bandari itafanywa na Serikali. Kila mmoja katika pande zote hizi mbili anatakiwa kutekeleza makubaliano hayo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ufinyu wa bajeti, kwa upande wa Serikali, ni kweli kwamba Serikali na yenyewe vile vile haijaweza kupanua ile miundombinu kama ilivyotakiwa na hii imechangia kwa kiasi fulani hata mwekezaji kushindwa kutekeleza yale aliyotakiwa kufanya kwa maana ya uwekezaji.

Hata hivyo, bado Serikali inaendelea kuzungumza na mwekezaji kwa kuzingatia mkataba ili kila mmoja atekeleze upande wake wa mkataba. Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi, vifaa vingine vinategemewa kuingia mwaka huu na mwaka kesho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu jibu la swali la pili la kwamba kwa nini mkataba uliongezwa, hili ni suala ambalo kwa sasa liko kwenye majadiliano ndani ya Bunge na nje ya Bunge na Serikali na yenyewe wanaongea na hao wawekezaji ili kuona namna gani vipengele vya mkataba huu vinaweza vikanufaisha pande zote na hasa Tanzania bila kuathiri yale ambayo yalikuwa yamekubalika.

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli kabisa kulikuwa na sababu zilizofanya mkataba ule uweze kuongezwa katikati kutokana na makubaliano ya kufanya uwekezaji mkubwa kiasi kwamba usingeweza kungoja mpaka wakati ule wa miaka 10 ya mwanzo iishe.

Hata hivyo, kama nilivyosema, Serikali inaendelea na mazungumzo na kama kutakuwa na haja ya kuungalia huu mkataba upya na tayari Wanasheria wanajaribu kuuangalia, basi kazi hiyo itafanyika na Wabunge watajulishwa nini matokeo ya mazungumzo hayo yanayoendelea.

**MHE. ANNA K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza kwa sababu mimi niko kwenye Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Spika, hapa suala ni kwa nini Serikali haikungoja mkataba wa kwanza ukaisha ndipo ikaongeza mkataba wa pili? Sisi katika Kamati, tulimwita aliyekuwa *PSRC*, tukamuuliza kwa nini amefanya hivyo? Yeye akatujibu kwamba agizo lilitoka juu, yeye alitekeleza tu. Je, kwa nini agizo litoke juu limlazimishe *PSRC* kuongeza muda huu?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri sana katika maswali mawili yaliyoulizwa na Mheshimiwa Janguo.

Mheshimiwa Spika, uwekezaji hasa katika eneo hili tunaloliongelea la Bandari, ni uwekezaji mkubwa. Kipindi cha miaka 10 kilionekana kabisa kwa mpango ambao tunao kwa Bandari hiyo ya Dar es salaam, haingewezekana kabisa mwekezaji akaweza kuwekeza uwekezaji mkubwa na kuweza kurejesha pesa yake katika kipindi hicho na ndiyo maana Serikali ikachukua uamuzi wa makusudi kuweza kuongeza muda huo.

Mheshimiwa Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri, hivi sasa Serikali imeshatoa notice kwa *TICTS* na yeye *TICTS* ameonyesha utayari wake ili tuweze kuketi kitako na kuanza kupitia mkataba huo ikiwa na sehemu ya hili la kipindi

kilichoongezwa cha miaka 15 ili kiendane na uwekezaji ambao tunataka tuuone katika Bandari ya Dar es salaam.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba Bunge lako Tukufu na Watanzania, watupatie muda ili tuweze kutekeleza haya kwa sababu tumedhamiria kabisa kuigeuza Bandari ya Dar es salaam iweze kutumika kama kioo na kama kiungo muhimu cha uchumi wa Tanzania. Kwa hiyo, naomba mtupe subira, tutayafanya haya ambayo na ninyi mnataka tuyafanye katika Bandari ya Dar es salaam.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mnisamehe, najua hili halijaisha kabisa. Kwa hiyo, Serikali iendelee kujiandaa tu kwa sababu… *(Makofi)*

Na. 140

**Ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti**

**MHE. MGANA I. MSINDAI** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali katika bajeti yake ya mwaka 2007/2008, iliahidi kutoa Sh.200mil kwa ajili ya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa Daraja la Mto Sibiti litakalounganisha Mikoa ya Shinyanga, Mwanza, Mara na nchi jirani na Mikoa ya Singida, Arusha, Kilimanjaro, Dodoma na Morogoro na kadhalika; na kwa kuwa Serikali iliahidi pia kuanza kujenga Daraja hilo katika kipindi cha mwaka 2008/2009;

Je, Serikali imefikia hatua gani ya utekelezaji wa ahadi hiyo sasa ikizingatiwa kuwa mvua za masika zinaanza kunyesha na eneo hilo hujaa maji kwa zaidi ya miezi minne?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* Mkoa wa Singida, ilitangaza zabuni ya kumpata Mhandisi Mshauri ambaye atafanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa Daraja la Mto Sibiti. Zabuni kutoka makampuni mawili kati ya nane yaliyokuwa *shortlisted,* zimewasilishwa tarehe 15 Januari, 2008. Kazi ya uchambuzi wa zabuni hizo ili kumpata Mhandisi Mshauri, imekamilika mwanzoni mwa mwezi Februari, 2008 na kazi ya upembuzi yakinifu itaanza mwezi Machi, 2008 na inatarajiwa kukamilika katika mwaka huu wa fedha 2007/2008. Aidha, ujenzi wa daraja unatarajiwa kuanza katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 kulingana na upatikanaji wa fedha.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali moja la nyongeza.

Kwa vile ilipokuwa inasomwa bajeti ya mwaka 2007/2008, Serikali ilisema itatenga fedha mwaka ujao wa fedha yaani 2008/2009; na kwa kuwa sasa hivi mchakato wa bajeti ndio unaendelea; je, Serikali itahakikisha imetimiza ahadi yake kwa kujenga Daraja la Mto Sibiti?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu, ni ahadi yetu kwamba tutatenga fedha mwaka ujao wa fedha ili daraja hilo lianze kujengwa. Nimweleze tu Mheshimiwa Msindai kwamba ahadi hiyo ni ya hakika. Sisi kama Wizara, tutatenga fedha, itategemea sasa Bunge kupitisha fedha hizo ili kazi hiyo ianze. Habari njema ni kwamba, ingawaje mwanzoni tulikuwa tumesema daraja litahusisha kilomita sita za barabara lakini kutokana na fedha za kutosha kupatikana kwa ajili ya usanifu, tutafanya usanifu wa daraja na kilomita 25 za barabara katika eneo lote lile lenye chemichemi.

Na. 141

**Migogoro ya Kisiasa Nchi za Eneo la Maziwa Makuu**

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA** aliuliza:-

Kwa kuwa, migogoro ya kisiasa iliyozikumba nchi za eneo la Maziwa Makuu zikiwemo Congo DRC, Rwanda na Burundi imeileta Tanzania mzigo mkubwa wa kuhifadhi wakimbizi:-

Je, Umoja wa Ulaya umesaidiaje katika kulikabili na kulitatua tatizo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mbunge wa Morogoro Kusini, naomba kutoa malezo ya utangulizi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba migogoro katika eneo la Maziwa Makuu, imeiletea Tanzania mzigo mkubwa wa kuhifadhi wakimbizi kiasi kwamba katika kipindi cha kuanzia Machi, 2002 hadi 31 Desemba, 2007 Tanzania ilikuwa na wakimbizi wapatao 873,787 makambini na 222,000 katika makazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya hali ya amani kurejea katika nchi zao na zoezi la kuwarejesha kwao wakimbizi walio makambini kwa hiari yao kuanza, sasa wamebaki wakimbizi 209,133 makambini. Zoezi la kuwarejesha wale walio katika makazi, linatarajiwa kuanza mwezi Machi, 2008.

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwenegoha kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Ulaya ni moja kati ya wahisani wakuu wa mpango wa kuhifadhi na kuhudumia wakimbizi hapa nchini. Jumuiya hiyo imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya kazi hiyo. Katika mwaka huu wa fedha kwa mfano, Jumuiya ya Ulaya imeipatia *UNHCR* shilingi bilioni 11 kwa ajili ya kuhudumia wakimbizi hapa nchini. Fedha zinazotolewa kwa *UNHCR* zinagharamia miradi ifuatayo:-

> Huduma zote za msingi kwa wakimbizi kama vile malazi, huduma za afya, shule na kadhalika isipokuwa chakula ambacho kinatolewa na Mpango wa Chakula wa Dunia *(WFP);*
>
> Kuimarisha uwezo wa watendaji wa Serikali na Mashirika katika maeneo yanayohifadhi wakimbizi katika kuwahudumia;
>
> Kuimarisha usalama kwenye makambi kwa kulipia gharama za huduma kwa Polisi waliopelekwa kutoka Mikoa mbalimbali kulinda makambi na maeneo yanayozunguka makambi; na
>
> Kugharamia zoezi la kuwarejesha wakimbizi kwao.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Umoja wa Ulaya umekuwa mchango mkubwa katika kukabiliana na tatizo la wakimbizi na pia katika kupata ufumbuzi wa kudumu kupitia michango ya fedha na rasilimali nyingine.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili mafupi kabisa ya nyongeza pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Ninapenda kufahamu tu kama mwenyewe alivyosema kwamba Jumuiya ya Ulaya ni mojawapo kati ya wahisani wengi wakuu ambao wanatusaidia. Je, wahisani hao wengine ni nchi zipi?

(b) Wahisani wengi wangependa wakimbizi wapatiwe uraia katika nchi yetu; je, msimamo wa Serikali hasa ni upi?

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninapenda kusema kwamba kuna nchi nyingi sana kama alivyoeleza yeye mwenyewe ambazo wanatoa msaada kupitia *UNHCR* zikiwemo nchi ya Uingereza, Marekani na nchi mbalimbali. Kama anapenda kupata taarifa rasmi, namkaribisha ofisini ili nimpatie orodha kamili ya nchi ambazo wanatoa msaada moja kwa moja nchini pia kwa kupitia *UNHCR*.

Kuhusu suala la kuwapatia uraia, ninapenda kusema kwamba Serikali inafuata utaratibu wa kisheria wa kuwapatia uraia wale watakaoomba uraia lakini nia ya Serikali

ni kwamba wakimbizi wote warejee makwao. Hatutamzuia mtu ambaye anapenda kuomba uraia kufuata utaratibu wa Sheria, apitie taratibu za kawaida na pale atakapopitishwa na Wizara yangu, atapewa uraia. Ninapenda kurudia tena kusema lengo la Serikali ni kwamba wakimbizi wote warejee makwao. *(Makofi)*

Na.142**.**

**Shirika la Nyumba la Taifa Kujenga Nyumba Mtwara**

**MHE. RAYNALD A. MROPE (K.n.y. MHE. MOHAMED S. SINANI)** aliuliza:-

Kwa kuwa Manispaa ya Mtwara Mikindani imekua kwa kasi kubwa; na kwa kuwa kasi hiyo inazidi kuongezeka baada ya barabara ya Dar es Salaam Mtwara kukamilika hivi karibuni na umeme wa uhakika kupatikana:-

Je, ni lini Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)* litajenga nyumba kwa ajili ya makazi na Ofisi Mtwara ili kukidhi mahitaji yao?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed S. Sinani, Mbunge wa Mtwara Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Sheria Na.2 ya mwaka 1990 iliyoanzisha Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*, Shirika linatakiwa kufanya shughuli zake kibiashara. Kutokana na hali hii, Shirika linajenga nyumba kwa ajili ya kuuza au kupangisha katika Miji ambako kuna soko la uhakika. Serikali inaungana na Mheshimiwa Mbunge kwa kulikaribisha Shirika la Nyumba kuwekeza katika sekta ya makazi Mjini Mtwara.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Shirika la Nyumba linawasiliana na Manispaa ya Mtwara Mikindani ili kupatiwa viwanja. Baada ya kupata viwanja, Shirika lipo tayari kuanza kutekeleza mradi huu mwaka ujao wa fedha, 2008/2009.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kama ifuatavyo:-

(a) Katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani kulikuwa na uwekezaji mkubwa wa ujenzi wa Hoteli Mtwara na hoteli hii haikuweza kukamilika kutokana na ukata, je Wizara haioni kwamba ni vema ingeingia katika mpango huo ili kwanza kuokoa fedha zilizotumika pale na pili kuwa kitega uchumi kwa siku za baadaye kwa kuwa na hotel nzuri katika Mji wa Mtwara?

(b) Katika Mkoa wetu wa Mtwara, imezaliwa Wilaya mpya ya Nanyumbu ambayo kwa kweli inahitaji vitega uchumi vingi na hasa vya makazi, je, shirika hili halioni kwamba ni wakati mzuri sasa ikaangalia sehemu za Nanyumbu ili kuwekeza katika upande wa makazi?

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri Nyumba na Maendeleo ya Makazi, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mrope kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama jibu la msingi lilivyotolewa, kwa mujibu wa Sheria Na.2 ya mwaka 1990 ambayo ilianzisha *National Housing Cooperation* (*NHC*), inatakiwa ijiendeshe kibiashara na kwa bahati nzuri *NHC* imekuwa ikifanya hivyo katika kuhakikisha kwamba inajiendesha kibiashara na ndiyo maana haipati ruzuku kutoka Serikalini.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu hiyo, *NHC* viwanja vyake huwa inawakaribisha yenyewe wawekezaji wanaotaka kujenga mahoteli, siyo wanaoshindwa kujenga mahoteli waikaribishe *NHC* kujenga hoteli kwa sababu jukumu kubwa la *NHC* ni kujenga makazi ya kuishi na ndiyo maana hadi sasa hivi ina nyumba zaidi ya 16,021 katika nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ombi la Nanyumbu, kwa bahati nzuri kupitia Wizara ya Miundombinu, Wilaya mpya ya Nanyumbu imejengewa nyumba 15 na nina uhakika zipo katika hatua mbalimbali za kukamilika.

Mheshimiwa Spika, kadri itakavyokuwa inajionesha hapo baadaye, kama patakuwepo wananchi wanataka kujengewa nyumba kupitia *NHC*, maombi yale yatapelekwa na kwa mujibu wa Sheria hizo ambazo nimezitaja pamoja na Sheria Na.11 ya mwaka 2005, suala hilo linaweza likaangaliwa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana.

**SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, muda umetutupa mkono, tutamalizia tu swali la Wizara ya Nishati na Madini, yale mawili ya Hazina, tutaangalia baadaye. Kwa hiyo, namwita sasa Mheshimiwa Bakari Shamis Faki kuuliza swali la mwisho.

Na 143

**Mashirika ya Umma Yaliyouzwa**

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI** aliuliza:-

Kwa kuwa Mashirika mengi yaliyokuwa ya umma hayafanyi kazi tangu yalipouzwa:-

(a) Je, ni lini Serikali itaipitia upya mikataba iliyoingiwa wakati wa kuuzwa kwa mashirika hayo?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuziendeleza kampuni za madini ili kutoa kipaumbele cha ajira kwa Watanzania hasa kwa yale maeneo ya uchimbaji wa madini?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, naomba kutoa maelezo ya utangulizi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji kwa miaka 15 iliyopita, umefanywa chini ya usimamizi wa Tume ya Rais ya Urekebishaji wa Mashirika ya Umma (*PSRC*). *PSRC* imemaliza uhai wake wa kufanya kazi tarehe 31/12/07 na kuanzia tarehe 1 Januari 2008, shughuli zote zinazohusiana na ubinafsishaji zimehamishiwa *Consolidated Holding Cooperation* (*CHC*), chini ya usimamizi wa Wizara ya Mipango kwa kushauriana na Wizara husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu ina mashirika matatu ambayo ni Shirika la Umeme (*TANESCO*), Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) na Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*). Kati ya mashirika hayo, *STAMICO* pekee ndiyo iliyokuwa na kampuni tanzu ambazo ni *Nyanza Salt Mine, Kiwira Coal Mine, Minjingu Phosphate, Pugu Kaolin, Coast Salt Works, TANCUT, Tanzania Gemstone Industries, Buckreef Gold Mining, Williamson Diamonds Limited* na *Tanzania Meerschaum.*

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, suala la ubinafsishaji wa mashirika ya umma unasimamiwa na Wizara ya Fedha na Uchumi. Kwa upande wa Wizara ya Nishati na Madini, kampuni tanzu za *STAMICO* ziliuza hisa zake au kubinafsishwa na zingine zilifilisiwa. Kampuni zilizobinafsishwa ni Kiwira *Coal Mines limited, Nyanza Salt Mines Limited, Coastal Salt Works, Pugu Kaolin Mines, Buckreef Gold Mining* na *Minjingu Phosphate Company.* Kampuni za *TANCUT* na *Tanzania Meerschaum* zilifilisiwa.

Aidha, Serikali ambayo ilikuwa inamiliki asilimia 50 ya hisa za kampuni ya *Williamson Diamonds Limited* ilipunguza hisa zake hadi asilimia 25 mwaka 1995. Ubinafishaji wa kampuni ya Mundarara *Ruby Mining Company* ambayo inamilikiwa kwa ubia na Serikali kupitia kampuni ya *Tanzania Gemstone Industry* na kampuni ya *Tan Ruby,* kila manahisa akimiliki asilimia 50 ya hisa katika kampuni hiyo, bado haujafanyika kwa kuwa *Tan Ruby* ina mgogoro na suala liko Mahakamani.

(b) Mheshimiwa Spika, wakati Bunge lako linaridhia kumaliza muda wa *PSRC* kwenye Mkutano wa Tisa, Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge hili, iliishauri Serikali na Wizara ya Fedha ilikubali kuwa kulikuwa na haja ya kupitia upya

makubaliano ya ubinafsishaji kwa kufanya tathmini ya hali ya mashirika ya umma yaliyobinafsishwa (*Post Privatization Assessment*), *CHC* ilikabidhiwa kazi hiyo na kwa kuwa *CHC* ndiyo kwanza tu imeanza kazi mwezi mmoja tu uliopita, wataleta taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa kazi hiyo Serikalini na kupitia Bunge lako Tukufu. Wizara yangu itatoa taarifa ya hali ya *Post Privatisation Assessment* kwa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa yaliyokuwa chini yake.

Mheshimiwa Spika, sekta ya umma ilishajitoa kwenye ushiriki wa moja kwa moja kwa uzalishaji wa sekta ya madini. Hata hivyo, Serikali inafuatilia utendaji kazi wa kampuni ya madini kupitia Wizara yangu na taasisi kama *STAMICO* ili kuweza kulinda maslahi ya Taifa letu kwa lengo la kujiridhisha kwamba utekelezaji wa makubaliano ya ubinafsishaji kama vile kutoa ajira na mafunzo kwa Watanzania unafanyika. Aidha Serikali imetoa vivutio mbalimbali ili kukaribisha wawekezaji katika sekta ya madini kwa wazalendo na wageni kwa lengo la kuongeza ushiriki mpana *(broad participation)* katika sehemu zote zinazohusiana na sekta hii muhimu sana kwa uchumi wetu .

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kupatikana kwa ajira kwa Watanzania, Sheria ya Madini ya mwaka 1998, imerahisisha upatikanaji wa leseni za madini. Vile vile, katika fomu za maombi ya leseni zenyewe, Serikali imeweka sharti kwa kampuni yenye leseni kuwa na mpango wa ajira kwa Watanzania na kuwapatia nafasi za uongozi kila inapowezekana.

Mheshimiwa Spika, katika leseni za utafutaji na uchimbaji madini, kuna kipengele kinachozitaka kampuni kutoa ajira na mafunzo kwa Watanzania. Taratibu za ajira kwa wageni husimamiwa kwa pamoja na Idara za Madini, Kazi, *TIC* na Uhamiaji. Ajira za wageni katika migodi huruhusiwa kufanyika kwa kazi ambazo hazina watalaam wa Kitanzania. Kazi zote ambazo watalaam wake huweza kupatikana nchini, kampuni hutakiwa kuwaajiri Watanzania. Aidha, kwa kazi ambazo siyo za utalaamu mkubwa kama za ulinzi, udereva, huduma za kantini, vyakula na kandarasi ndogo ndogo, kipaumbele ni kwa Watanzania.

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI:** Ahsante Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili tu ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri katika majibu yake kwamba hisa zingine za *STAMICO* zilifilisiwa je, ni sababu zipi za msingi zilizopelekea hisa hizo kufilisiwa?

(b) Je, ile ahadi ya Serikali ya kuwasaidia wachimbaji wadogowadogo imeishia wapi?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, makampuni yaliyokuwa chini ya Wizara ya Nishati na Madini ni hayo niliyoyasema na kwamba zoezi la kufilisiwa lilitokana na utendaji wake wa kazi ambao ulikuwa hauna tija tena. Kusema kweli ulikuwa haiwezekani kuingia katika hatua hii ya kubinafsishwa na ndiyo maana nimesema hapa kwamba kuna makampuni

yaliyobinafsishwa na makampuni yaliyofilisiwa ambayo yalikuwa ni *TANCUT* ya Iringa na Tanzania *Meerschaum* ambayo ilikuwa Arusha.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili linahusiana na wachimbaji wadogo wadogo, kusema kweli Sera ya Madini inataka Serikali itoe kivutio kwa wachimbaji wadogo wadogo. Kwa hiyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Idara zingine za Serikali, inaandaa mkakati maalum wa kuangalia namna ambavyo tunaweza tukatoa msaada kwa wawekezaji wa kizalendo kama kuwapa mikopo na kuangalia misaada mingine ya sekta ya fedha.

Mheshimiwa Spika nadhani nimemjibu swali lake kwa upana *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Naam, hakika umemjibu. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umeisha na maswali yale mawili yaliyosalia yanasogezwa mbele.

Matangazo, Waheshimiwa Wabunge, napenda kwa mara nyingine tena tutambue kwenye *Speakers Gallery* uwepo wa Mheshimiwa Mke wa Waziri Mkuu wetu, Mama Tunu Mizengo Pinda. Naomba asimame, karibu sana Mama *(Makofi)*

Wageni wetu wengine ni kama ifuatavyo, kuna ujumbe kutoka Benki ya Dunia ambao umekuja mahsusi kushauriana na uongozi wa Bunge kuhusu mpango mkakati wa miaka mitano, *Cooperate Plan for Parliament of Tanzania five year* 2008-2012. Ujumbe huo, licha ya kuwa na Bwana Permindas Brah ambaye yupo Benki ya Dunia pale Dar es Salaam ni pamoja na mchumi, Bwana Paul Zekie, lakini mtaalamu ambaye analipwa na Benki ya Dunia kutukamilishia huo mpango mkakati, ni Bwana Niel Johnston kutoka Uingereza.

Kwa wale ambao bado hawajafahamu, kwa kifupi tu niseme ni dhamira ya Spika huyu kwamba baada ya miaka mitano Bunge letu liwe ni Bunge bora kwa fani zote katika eneo hili la Kanda ya Maziwa Makuu. *(Makofi)*

Ili kuwa na demokrasia inataka *vision* na mikakati ndani ya Bunge, nje ya Bunge, uwezeshaji wa Waheshimiwa Wabunge ili wafanye kazi zao. Kwa mfano mpaka sasa ofisi ya Mbunge haijatambulika kwa maana kamili kwamba, je, anawasaidizi au hana, mambo yote haya hivi sasa tunajaribu kuyahangaikia.

Tangazo lingine ni kwamba saa nane kamili kwenye ukumbi wa Spika, Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma za Bunge, tutakutana na wageni hawa ili tuendelee kuwapa maagizo. Ni kikao kifupi tu cha utambulisho. Watakuwa nasi Dar es Salaam kwa siku kama tano kwa hiyo tutaendelea nao lakini saa nane baada ya kuahirisha Bunge, naomba wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi na wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge, tukutane na wageni hawa wa Benki ya Dunia.

Mr. Permindas**,** *we are very grateful to the world Bank for the assistance that they are giving to our Parliament to enabling it to be Parliament of excellence in this Region, thanks very much.*

Nafurahi pia kumtambulisha, Mama Lina Mwakyembe, mke wa Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, Mwenyekiti wa Kamati Teule, karibu sana Mama. Tunakushukuru sana kuja kumuunga mkono Mzee hapa. Nadhani wewe ni shahidi, amekuwa na kazi ngumu sana lakini kazi yoyote inayofanywa kwa uaminifu, inafaraja zake, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wanafunzi 40 kutoka Shule ya Sekondari ya Dodoma, ninahakika wapo na Waalimu wao. Naomba pale walipo wasimame, ahsante sana vijana na Walimu, tunashukuru sana mnawaleta vijana wajionee *live* shughuli za Bunge. *(Makofi)*

Wapo pia Wachungaji wa Vijana wa Kanisa la Pentekoste, Bwana Barnabas Mrope na Bi. Jane Ally, naomba wasimame. *(Makofi)*

Wapo pia wanafunzi 33 kutoka Chuo Kikuu kipya cha Dodoma, wale pale. Haya ndiyo matunda ya Prof. Msolla sasa tuna Chuo Kikuu ambacho tunatarajia kiwe kikubwa kuliko vyote ndani ya miaka michahe, ahsante sana. Lakini na ninyi msome, nchi inahitaji wasomi wazuri na waadilifu. *(Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Wasira, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, anaye mgeni wake ambaye ni Samson King'uda, ni Mwenyekiti wa Kijiji cha Mariwanda kule Bunda, ahsante sana Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Tatu Ntimizi, anao wageni wake wawili ambao ni mama Mariam Rashid na Mwanae Salima Said. Karibuni sana na poleni sana na safari ndefu kutoka Igalula na njia ya wasiwasi lakini nadhani Waziri Chenge ameshasikia, Manyoni, Itigi, Tabora, haipitiki. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa nimeombwa niwatangazie Waheshimiwa Wabunge wale wote waliochukua hisa katika Benki ya Wanawake Tanzania, kutakuwa na huduma ya kutoa risiti kwa wale waliomaliza ununuzi wa hisa, majadiliano kwa wale ambao walipunjwa na kupokea malipo kwa wale ambao waliahidi kununua hisa lakini bado hawajaanza kulipa. Zoezi lote hili kwa wale ambao wana hisa au wanahisa watarajiwa wa Benki ya Wanawake Tanzania, itafanyika katika Jengo la Msekwa, katika ukumbi ambao mtaelekezwa mkifika tu kwenye lango kuu la jengo hilo la Pius Msekwa.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kikao cha pamoja cha Kamati ya Uongozi na Tume ya Huduma, Mheshimiwa Spika atakuwa na kikao saa tisa kamili na Kamati ya Uongozi ya Kambi nzima ya Upinzani, ahsante.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

Muswada wa Sheria ya Kusimamia na Kudhibiti Sekta ya Hifadhi ya Jamii wa mwaka 2008 (*The Social Security (Regulatory Authority) Bill, 2008).*

Muswada wa Sheria ya Tume ya Taifa ya *UNESCO* wa Mwaka 2008 *(The UNESCO National Commission Bill, 2008).*

Muswada wa Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa Mwaka 2008 *(The Anti-Trafficking in Persons Bill, 2008).*

Muswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria mbalimbali za Ukusanyaji wa Mapato wa Mwaka 2008 *(The Finanacial Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2008).*

*(Miswada iliyotajwa hapo juu ilisomwa Bungeni kwa Mara ya Kwanza)*

**SPIKA:** Hiyo ndiyo Miswada minne iliyosomwa Mara ya Kwanza kwenye mkutano wetu huu. Kama kawaida sasa inaenda mbele ili iweze kupitia katika hatua zinazofuata katika mkutano na mikutano ijayo.

## HOJA ZA KAMATI

### Kamati Teule ya Bunge Iliyochunguza Mchakato wa Zabuni ya Kuzalisha Umeme wa Dharura Ulioipa Ushindi *"Richmond Development Company LLC"* ya Houston, Texas – Marekani Mwaka 2006

*(Majadiliano yanaendelea*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, jana niliawaarifu kwamba ninao wasemaje wanne kwa mpangilio ufuatao:-

Tutaanza na mwanakamati wa Kamati Teule, Mheshimiwa Seleli kwa dakika 15, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, Mheshimiwa Marmo, atafuatia Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati Teule, Engineer Stella Manyanya, baada ya hapo kuanzia 5.30, mtoa hoja, Mwenyekiti wa Kamati Teule, Mheshimiwa Dr. Harrison Mwakyembe, atazungumza kwa dakika zisizozidi 60, kuanzia saa 5.30 hadi saa 6.30 na baada ya hapo tutaendelea sasa kuyaangalia yale mapendekezo kwa kifupi na kama yatakubaliwa basi nitawahoji, tutapata uamuzi, hatimaye, nitamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu ili atoe hoja ya kuliahirisha Bunge.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 28(2), Spika anao uwezo kuwahoji ikifika saa saba na kama mkikubali tukaongeza nusu saa, nakusudia kufanya hivyo ili tuweze kumaliza shughuli hizi.

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu kwamba baada ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kutoa hoja ya kuahirisha na tukishaiunga mkono basi tutamaliza mkutano huu wa Kumi kwa kuimba Wimbo wa Taifa.

Sasa namwita Mheshimiwa Seleli!

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi kwa niaba ya Kamati ili niweze kusema machache ambayo tumeyafanyia kazi kwa uaminifu mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kabla sijasema, niwashukuru Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania lakini na wananchi wote wenye mapenzi mema ambao walituunga mkono kwa simu na kwa meseji. Nasema ahsanteni sana kwa kututia moyo katika hoja ya Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, wakati tukiwa kwenye Kamati Teule, mimi peke yangu, nilikuwa Mbunge ambaye sikuwa kwenye Kamati ya Uchumi na Biashara, wenzangu wanne wote walitoka kwenye Kamati hiyo. Pia napenda nichukue nafasi hii kuwashukuru kwa jinsi ambavyo walinivumilia nikaelewa suala hilo, kwa muda kama wa wiki moja hivi, nikawa nimekuwa nao vizuri, hivyo nawashukuru sana kwa kunipa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, sisi Kamati yetu tulimtanguliza Mungu na katika kumtanguliza Mungu, ilibidi tukubaliane wote kwa pamoja na vitisho na kejeli mbalimbali ambazo tulikuwa tunazipata kwamba tufanye mambo ya uwazi na ukweli, tusimwonee mtu wala kumsingizia mtu. Kwa hiyo, nakuhakikishia, Kamati yetu hii wote watano kwa kuipenda nchi yetu Tanzania, tulitumia uzalendo mkubwa sana ndiyo maana imekuja mpaka hatua ya mwisho tukatoa taarifa ambayo wengi wetu wametusifia na kutupongeza.

Mheshimiwa Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba kazi ambayo tumeifanya ya kuchunguza *Richmond* ilikuwa ni ngumu na nzito na ilihitaji moyo wa ujasiri kwa sababu mwanzoni tulidhani tunachunguza *Richmond* kumbe tunaichunguza Serikali na Serikali kuichunguza ina mambo magumu, makubwa na kwa kweli kabla sijaendelea mbele, napenda nitumie fursa hii kusema mawili ama matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Bwana Spika, ninapenda Bunge lako Tukufu litoe onyo kali sana kwa wale waliokuwa wanawapanga watumishi wa Serikali kuja kusema uwongo mbele ya Kamati yako. Wale watumishi wa Serikali walikuwa na unyonge sana ndani ya moyo. Unamwona mtu anachokizungumza sicho kilichopo kwenye nafsi yake lakini walikuwa wamepewa maelekezo na maagizo kutoka Serikalini. Kama tusingekuwa makini na sisi taarifa yetu ingefanana na ya Serikali. Kwa hiyo, napenda nitoe onyo kali kwa wakubwa wa Serikali kwamba waache mara moja tabia hiyo hasa Kamati kubwa kama ya Bunge inapoenda kuchunguza mahali popote itakapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati, napenda kutoa onyo kali kwa watumishi wa Serikali waliodiriki hata kuinyima taarifa, majalada Kamati Teule. Wapo Watumishi waliokuja na maelekezo, waliokuja na maagizo maalumu kwamba Kamati Teule isipewe nyaraka au mafaili. Kuna mtumishi mkubwa sana wa Katibu Mkuu alikuja amefunga faili kwa *clip* yaani tusome ukurasa huku ameshikilia. Suala hili ni hatari sana na lazima Bunge lako likemee tabia ya namna hii iweze kukoma ili Bunge likihitaji kitu ni taasisi kubwa sana ambayo inaruhusiwa Kikatiba kuisimamia Serikali hivyo chochote kile kikishafika kwenye Kamati Teule ni kitu cha wazi. Naomba Bunge lako Tukufu litoe onyo kali kwa watu wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, wajumbe waliokuwa wanakuja kwenye Kamati yetu Teule, walikuwa utadhani watoto wa Madrasa au *Sunday School*, wameimbishwa na kufundishwa kitu ambacho hata hawakijui, huko nyuma wamekisimamia kukataa lakini leo anakuja anaimba kitu cha kukubali na hii ni hatari sana kwa mustakabali wa nchi yetu.

Vilevile hata viongozi wa Serikali waweze kutambua watumishi wa Umma wanaotumia ujuzi na taaluma zao na waziheshimu. Tukiendekeza maslahi ya mtu binafsi, nchi hii tutaiua na sisi tuliomo humu ndani tutakuwa mashahidi huko mbele na makaburi yetu kupigwa viboko kwa hasira za watoto wetu na wajukuu wetu.

Mheshimiwa Spika, mjadala umekwenda vizuri sana na mimi ninawapongeza wote ambao wamechangia. Ninataka kuelekeza sehemu moja ya *PPRA*, ambayo tumeizungumza kwenye ukurasa wa 150 wa taarifa yetu na ningeomba Bunge lako vilevile lichukue fursa hii maalum, kuipongeza *PPRA*, kwa kazi nzuri ambayo ilifanya. *PPRA* ndiyo ilikuwa ya kwanza, kutupa ufunguo wa kujua kilichomo ndani ya *Richmond*, kwa sababu walikuwa na takwimu na ukweli ambao walielekeza kwenye taarifa yao. Ukisoma taarifa yao, utaona jinsi ambavyo walikuwa wamejitahidi kukemea taratibu zilizokuwa zinavunjwa na kanuni mbalimbali ambazo zilikuwa zinapindishwa kwa makusudi na kukemea sheria ambazo zimetungwa na Bunge lako Tukufu hili zikivunjwa na Serikali.

Kwa hiyo ni watu ambao walikuwa mstari wa mbele, ndiyo maana tumetoa pendekezo namba moja kwamba, sheria hii ipitiwe upya. Kuwaacha tu *PPRA* kuwa ni washauri, wataliumiza Taifa letu. Kwa hiyo, katika pendekezo namba moja, Kamati Teule tumeona kwamba, sheria hii ipitiwe upya ili kuipa meno taasisi hii kubwa, isiwe taasisi ya kushauri tu, bali iwe taasisi ya kuchukua hatua pale ambapo zitapindishwa. Kwa hiyo, ninaomba hili pendekezo Waheshimiwa Wabunge wote, tuweze kuliunga mkono na liweze kufanyiwa marekebisho haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lipo pendekezo la pili, ambalo tumeliandika kwamba, *PPRA* kuwa chini ya Wizara ya Fedha; Wizara ya Fedha, ni taasisi ya manunuzi, inaongozwa na Katibu Mkuu na Waziri wa Fedha; Taasisi ya *PPRA* inapotakiwa kutoa taarifa hapa Bungeni, lazima ipitie Wizara ya Fedha; je, pale ambapo muhusika mkuu ni Wizara ya

Fedha, Katibu Mkuu au Waziri mwenyewe; atapata kigugumizi sana kuileta taarifa kwenye Bunge. Ndiyo maana tunapendekeza kwamba, chombo hiki kiwe huru.

Tukatafuta namna gani ya kukipa nafasi ya kiutawala, tukaona basi ni bora kiwe kama ilivyo taasisi ya *CAG*, kiende Ofisi ya Rais na kilete taarifa moja kwa moja kwenye Bunge Tukufu, popote pale panapoonekana kama kuna upungufu, Bunge liweze kupata taarifa hiyo, bila kuwa na kikwazo cha kupitia kwenye Wizara. Kwa hiyo, ninaomba Bunge liweze kuridhia pendekezo namba mbili, ambalo tumelitoa ili taasisi hii ya *PPRA*, iwe chombo huru ambacho kitakuwa chini ya Ofisi ya Rais, lakini moja kwa moja taarifa zake zije kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda unakwenda sana, niende haraka. Jambo lingine ambalo ninataka kulisemea ni magazeti. Magazeti yametusaidia sana; imekuwa ni changamoto na wanastahili kupongezwa kwa hali ya juu sana. Tusiwabeze na tusiwashukuru kwa kuwasifu tu, tuwapongeze hata pale wanapotuambia mambo ya ukweli. Vyombo vya habari ni kama kioo. Kioo kikikwambia uso una tongotongo, usikivunje bali jisafishe mwenyewe. Tunashukuru sana vyombo vya habari na katika kuweka taarifa sahihi, wapo wengine wamesema tumetumia magazeti ya udaku si kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, magazeti tuliyotumia ni Mwananchi, Mwanahalisi, *The Express,* Kulikoni, *Sunday Citizen, The African, This Day, The Citizen, Daily News,* Majira na Rai. Hakuna hata gazeti hata moja la udaku katika haya ambayo tumeyatumia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii, kuikumbusha Serikali kwamba, ina ahadi ya kuanzisha mafunzo maalum ili kuwaongezea ujuzi; mafunzo hayo yaanze mara moja ili kazi za waandishi hawa ziweze kufanyika kwa ufanisi na kwa umakini. Waandishi hawa wanafanya kazi za uchunguzi; mimi nimeingia kwenye Kamati Teule hii; jamani uchunguzi ni mgumu, yataka moyo na yataka kujitolea.

Kuna shuhuda wetu wa habari alikuja akiwa na bastola, akatuambia kabisa kwamba, alikwishajiweka tayari kwa sababu anatishiwa sana, wanampa taarifa mbalimbali, anatembea na bastola akiwaona awamalize. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watu kama hawa, wanatakiwa wapewe ujuzi kama Serikali ilivyowaahidi, basi iweze kutimiza kutokana na ahadi ambayo imeitoa. Tumeeleza katika ukurasa wa 122.

Vilevile niseme kwamba, hata *Richmond* mwenyewe kuachia hii kazi ni kwa sababu ya kazi nzuri ya wanahabari. Ukisoma katika habari hii wanasema kwamba, aliacha kazi kwa sababu ya kuandamwa na magazeti na ikamfanya Richmond aunde kampuni maalum ya kuyanyamazisha magazeti. Kampuni ilikuwa inaitwa *G & S Media Consultancy,* ambayo tuliwahoji wamiliki wake wakasema hata sisi tulienda kwa ajili ya njaa tu, lakini ukweli waliokuwa wanasema waandishi wa habari, hauna kificho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende suala la nne la TAKUKURU; TAKUKURU wametuangusha, wameandika taarifa sawa na barua ambayo imeandikwa usiku kwa ajili ya kuisoma asubuhi, kuwahi taarifa za vyombo vya habari. Inakuwaje miezi sita waliyofanya kazi kuanzia August mpaka Aprili, walipotoa taarifa, wakashindwa hata kutoa takwimu moja ya rushwa; tulijiuliza sana! Kama unashindwa kuona harufu hata moja, moto wala majivu ni aibu!

Kwa hiyo, tumetoa mapendekezo kwamba, TAKUKURU hawa kwa sababu hawakuitendea haki nchi hii, imeingia hasara kubwa na imeingia mahali ambapo tumetumia fedha nyingi katika mambo haya ambayo wao wangeyafanya; pendekezo lipo katika *schedule of amendments* namba tisa kwamba, Mkurugenzi Mtendaji wa TAKUKURU, awajibishwe kwa manufaa ya umma. *(Makofi)*

Namba tisa hiyo hiyo, pendekezo la pili, maafisa wa TAKUKURU walioshiriki katika zoezi hilo wako wanne nao wawajibishwe kwa manufaa ya umma, ili liwe fundisho kwa wengine wanaokiuka maadili ya utumishi wa umma kwa sababu wanalipeleka Taifa mahali pabaya sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya TAKUKURU haikuwa hata na tarehe, ukiangalia kwenye viambatisho hata tarehe hawakuweka. Hivi taarifa gani ya kina ya uchunguzi, unasahau hata kuweka tarehe? Tunaamini Kamati Teule hii ilikuwa ni ya kupangwa. Baada ya kufanya uchunguzi wale watu wa TAKUKURU, walipeleka taarifa wakaona yamo majina ya wakubwa; baada ya kuipata yule mkubwa akaamua kuiandika jinsi ambavyo aliona hadi akasahau hata kuandika tarehe. Hii ni aibu kwenye nchi hii inayofuata demokrasia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya muda, pendekezo la 20 ziko habari ambazo zinasema kwamba, hii taarifa tuliyopewa ni ya kugushi, ambayo haina tarehe. Tunaitaka Serikali, kwa sababu tuna hakika kwamba, katika ile taarifa ya awali, wakubwa wamo; ichunguze iweze kupata ile taarifa halisi na kikao kijacho itupe taarifa. *(Makofi)*

Tunazo taarifa pia kwamba, hata katika kusajili makampuni, jalada lilichezewa. Kwa hiyo, katika pendekezo namba 20 hilo hilo, tunaitaka Serikali iende *BRELA* kujiridhisha na kupata faili halisi kwa ajili ya kuona kama lilichezewa na tuna hakika kwamba, katika taarifa hiyo ya kwanza, majina ya wakubwa yalikuwemo. Kama yalikuwemo, kikao kijacho waweze kuleta ili tuweze kuchukua hatua zaidi, kwa wote ambao wamehusika katika kuharibu ushahidi ambao Kamati yako ilikuwa iupate. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kukushukuru wewe na kuwashukuru Wabunge wote, kwa jinsi ambavyo mlitupa ushirikiano mzuri sana. Ninaomba mtuombee; tunayasema haya tukiwa tunaelewa mimi na wenzangu, tumekwenda kwenye kazi ngumu ya kuona kwamba, nchi yetu inafikia mahali pazuri, lakini wenzetu wenye nia mbaya na nchi hii, wanatutishia maisha. Hili ni jambo zito, tunazo *text* ambazo tumezitunza, tutakupa Mheshimiwa Spika, ili ikitokea, ninaomba sana Bunge lako liweze kuchukua

hatua kwa mafisadi wote waliotajwa na wale ambao hatukuwataja kwenye taarifa hii, tunawajua majina yao tunayo tutampa Spika, ili aweze kuyatunza. Ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Pole sana, kupigania haki daima kunahatarisha maisha, lakini ndiyo hivyo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii, ili na mimi pia nitoe mchango wangu wa mawazo katika hoja hii ya Kamati Teule ya Kampuni ya *Richmond*, iliyowasilishwa katika Bunge hili na Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe.

Mheshimiwa Spika, ninatambua kwamba, wasemaji mahiri sana wamenitangulia, hivyo, wamenifilisi. Pia ninafahamu kwamba, Mheshimiwa Waziri Mkuu katika hotuba yake ya kuahirisha Mkutano huu wa Bunge, atalijadili jambo hili na mimi nisingependa haya ninayosema, yaingiliane na yale ambayo atayasema Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, lakini itoshe tu kwangu kusema kwamba, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa kutuwezesha kuona na kushuhudia matukio haya muhimu ya nyakati zetu. Matukio haya yamesababisha misukosuko mingi, lakini pia yamefanya demokrasia yetu kuonekana kukomaa. Misukosuko hii pia imeongeza mshikamano, umoja, utulivu na amani katika nchi yetu. Hii siyo Kamati Teule ya kwanza katika historia ya Bunge letu. Mara zote taarifa ya Kamati Teule inapoletwa katika Bunge, inaleta misukosuko kama hii. Kama sitakosea, taarifa hii ya Kamati Teule ya Kampuni ya *Richmond*, iliyowasilishwa na Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe sasa ni ya tano kutoka *Legical* mpaka Bunge la Tanganyika na Tanzania Huru.

Taarifa ya Kamati Teule ya Kwanza, kama sitakosea, iliwasilishwa katika Bunge mwaka 1980 au mwishoni mwa 1970 na viongozi kama vile Mheshimiwa Naibu Spika wetu na ilihusu kashfa ya sukari. Kwa wale wa umri wangu, watakumbuka misukosuko iliyotokana na taarifa hiyo; ninadhani ilibidi Waziri ang’atuke. Taarifa ya pili ya Kamati Teule ya Bunge ilikuwa mwaka 1987 na mimi nilibahatika kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, iliyokuwa ikichunguza mienendo ya kampuni moja ya Misri, iliyokuwa ikinunua dhahabu katika Kanda ya Ziwa; ilikuwa inajulikana kwa jina *DTT*. Misukosuko ya taarifa ya Kamati Teule ile, nayo haikuwa haba. Mnamo mwaka 1992/1993, tuliunda Kamati Teule kuchunguza matumizi ya masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati Serikali ilikuwa ikiongozwa na Mheshimiwa Dr. Salmin Amour kule Zanzibar.

Sote tutakumbuka kwamba, matokeo ya taarifa ile nayo yalisababisha misukosuko ambayo nayo haikuwa haba. Kamati ya mwisho kabla ya hii ya Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe ilikuwa Kamati Teule ya Wanyamapori, ambayo mimi nilibahatika kuiongoza, nayo ilikuwa na misukosuko yake. Ninakumbuka, tuliweza kubadilisha mojawapo ya Kumbi za Bunge pale Dar es Salaam kuwa kama Kumbi za Masumbwi na mwanakamati mmoja ninafikiri aliweza kuchaniwa shati lake. Kwa hiyo, ninachotaka kusema; Kamati hizi kwa kweli ni muhimu, nyeti na zinakomaza sana

demokrasia.  Ndiyo maana pale awali nilisema kabisa kwamba, ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwamba, ninashuhudia tena matukio haya ambayo yanakomaza demokrasia katika nchi yetu.  *(Makofi)*

Sasa kwa uzoefu wetu huu, matokeo ya kamati hizi mara nyingi ni nini? Nimesema huwa kuna misukosuko na misukosuko hii mara nyingi imesababisha mapendekezo mengine yatekelezwe papo kwa papo; kamati zote hizi, kutoka ile ya kwanza kabisa ya miaka ya 1980 mwanzoni, ya miaka ya 1992 na ile ya 1994. Mapendekezo mengine yalikuwa yanatekelezwa papo kwa hapo.  Ninadhani ninyi na sisi, sote tumeshuhudia mapendekezo ya Kamati hii Teule, mengine yametekelezwa papo kwa hapo.  Mapendekezo mengine huchukua sura ya mchakato; kamati zote hizo nilizotaja; mapendekezo yake muda wote yamekuwa yakichukua sura ya mchakato.  Mara nyingi mchakato wa kubadilisha sheria au kanuni, huchukua mkondo wake.  Mara nyingine kunakuwa na kufanya mabadiliko katika taasisi mbalimbali; mara nyingine husababisha uwajibikaji, kubadilisha au kuunda taasisi mpya na hata hatua za kimahakama kufuatwa.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, hata kwa Kamati hii, michakato hii kwa vyovyote vile itatokea.  Kutakuwa na mchakato wa kuangalia shughuli zetu na kanuni zetu; kutakuwa na mchakato wa kuchukua hatua mbalimbali za kuwajibisha watu; kutakuwa na uwajibikaji; kutakuwa pengine na hata hatua za kimahakama.  Isipokuwa kwa sasa, hatuwezi kubashiri mbele ya safari kutatokea nini, kwa sababu sote tunafahamu kwamba, yote yaliyopendekezwa na Kamati hii, lazima yafanyiwe kazi.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, alipokuwa akilihutubia Taifa kupitia Wazee wa Dar es Salaam, alisema kwamba, Serikali itayafanyia kazi mapendekezo haya na kwa sisi Serikalini, kauli hii ya Mheshimiwa Rais, kwa lugha ya kijeshi ni kama amri na lazima tuitekeleze.  *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kifupi sana, mimi kama nilivyosema pale mwanzo, nisingependa kuchafua yale mazuri yaliyokwishasemwa na wenzangu, ambayo nimesema ni wasemaji mahiri na ninapenda kuhitimisha kama ifuatavyo:  Kwamba, jitihada kubwa zilizokuwa zikifanyika na *TANESCO* na Serikali katika suala hili ili kupata mitambo ya kukodi, ilikuwa ni kulinusuru taifa kutoka katika upungufu mkubwa sana wa umeme wakati ule.  Dhamira na azma ya kupata mitambo hiyo, ilikuwa ni kupambana na janga hilo na kwa nia njema kabisa.  Katika kutekeleza azma hii, kama tulivyoona, makosa yalijitokeza; ukweli ni kuwa, yapo mambo mengi ambayo Serikali imejifunza kutokana na mchakato wa kukabiliana na dharura na sasa tunataka kuweka mkakati maalum wa namna ya kukabiliana na majanga na dharura, kwa umakini na kwa ufanisi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa baada ya hapo twende wapi kwa haraka haraka; mtakumbuka tuliyoyajadili katika Kamati ya Uongozi kuhusu Muswada muhimu sana wa Umeme *(Electricity Bill 2008)* na ule wa Petroli *(Petroleum Bill, 2008);* Kamati ya Uongozi chini ya uongozi wako, ikapendekeza kwamba, tuwe na semina ambayo Wabunge watajadili kwa kina, masuala yote yanayohusu ugavi wa umeme katika nchi

yetu na kuwa na sheria ambayo itajibu haja na namna ambavyo tutaondokana na matatizo yaliyojitokeza katika Mkataba huu wa *Richmond*.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali imekubali kuwe na semina hii ya siku mbili, kabla ya Mkutano wetu wa kujadili *budget frame* na kabla Kamati za Bunge, hazijaanza kushughulikia masuala ya Mkutano ujao wa Bunge.

Ninaamini, wakati huo tutafikia muafaka fulani na tutakuwa na sheria ambayo itakubalika pande zote, ambayo tunaihitaji hapa; nina maana Sheria ya Umeme ya mwaka 2008, ambayo ndiyo sharti moja la eneo hili kupata fedha kutoka Mfuko wa Marekani wa *Millenium Challenge Corporation.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa mara nyingine, ninaomba niseme kwamba, taarifa hii ya Kamati Teule, ni tofauti kidogo na taarifa za kamati nilizozitaja mapema; hii ni taarifa kabambe sana. Mimi ninaiunga mkono na kama nilivyosema pale awali, Serikali itazingatia yale yote yaliyopendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa ni zamu ya Makamu Mwenyekiti wa Kamati Teule, ningemwomba aje hapa mbele, kwa sababu ya hadhi yake kama Makamu Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, ili nami niweze kuongea machache, kwa kuwa wachangiaji wengi wametufahamisha mambo mengi ambayo tayari wameshayaona kwenye taarifa yetu na michango yao imekuwa ni ya kutusaidia sana. Kabla sijachangia, ninaomba nichukue nafasi hii, kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, kwa sababu alitusimamia katika ukweli na katika haki na vilevile alituonyesha na kututambulisha kilio cha Watanzania, ambao sasa walikuwa wanataka kufahamu ukweli na sio kudanganywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama kawaida, ningekuwa ninaandika *text,* ninge-*dedicate* katika ripoti; nina-*dedicate* ripoti hii au uhai wangu kwa ajili ya Watanzania wanaopata tabu kwa sababu ya mikataba mibovu na kutokuwatendea haki hasa sisi ambao ni *professionals;* tuliosoma kwa kutumia hela ndogo ambayo wao wamejinusuru huko na kufanya kazi ambazo hazina maslahi kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda pia kuwashukuru wananchi wote kwa ujumla, ambao ndiyo wanaotusimamia hata sisi, nifuatie Serikalini tukianzia na Kiongozi Mkuu wa Serikali yetu, Mheshimiwa Rais, pamoja na wote waliotuunga mkono; Waheshimiwa Wabunge wote, Waandishi wa Habari na kila mmoja, ambaye aliguswa na taarifa hii kwa namna moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niende moja kwa moja kuhusiana na upungufu niliouona katika taarifa hii ambayo tumeileta hapa kwako. Kwanza kabisa, ninaanza kwa

kuwashukuru Bwana Mohamed Gire na Bwana Mohamed Haque, ambao ndiyo wahusika wa *Richmond Development Company LLC,* jinsi ambavyo walitupokea na kuweza kutupa ushirikiano hata kama masuala haya yalikuwa yanawagusa.

Ninapenda pia nichukue nafasi hii, kuwashukuru Watanzania na ndiyo maana hata kwenye taarifa yetu, mmeona kwamba, jalada linalotuongoza linasema kwamba, tulikuwa *Richmond Printing Company RDVECO,* hatukuikuta *Richmond Development Company LLC,* kama ambavyo iliingia mkataba na *TANESCO*. Kwa hiyo, hayo ni masuala ya kisheria na ndiyo maana tunaposema kwamba, kampuni hiyo haipo, tunazungumzia masuala ya kisheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi wetu, tunakushukuru sana kwa sababu uliunda Kamati ambayo ilikuwa na umoja, pale hakukuwa na Chama chochote kile cha siasa, ilikuwa ni utaifa na ndiyo maana ninaomba nitoe rai kwa wananchi kwamba, kwa kuwa sasa Wabunge wenu tumeshatambua nini tunatakiwa kufanya si vyema sana tukayachukua masuala haya na kuyaingiza kuwa ni ya chama Fulani, mtakuwa mnaturudisha nyuma pale ambapo tayari tumeshafikia. Tuendelee na umoja wetu na ninyi pia tunaomba huko mliko, msimamie kama ambavyo nimejionea jana; Wanakijiji wa Nyakatala huko Mwanza, wamekataa kisima ambacho hakitoi maji; hiyo ndiyo tunaona sasa wananchi wameamka na watasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba niende moja kwa moja kwanza, kwa kusikitika jinsi ambavyo wataalam walihusika katika kuingia mkataba huu na sio huu tu; hata ile mikataba mingine ya *IPTL* ya *AGGREKO* na mingine ikiwepo *Net-Group Solutions,* wanaotuangusha ni pamoja na wataalam wetu; hawana *confidence,* wanaenda ku-*negotiate* mikataba wakiwa hawana kitu mkononi, wanafika pale wanamwona yule ambaye wana-*negotiate* naye, ndiyo ana *powers* kuliko wao, kwa hiyo, wanapokea kilichopo wakati wao hawajui ni nini walitakiwa ku-*offer;* hilo ni tatizo kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mara ya mwisho umeshuhudia jinsi ambavyo Wabunge, kwa umoja walisema, wasingependa kupitisha Miswada ya Sheria ya Umeme na Mafuta iliyokuwepo mpaka kwanza wapate taarifa hii. Mimi ninawashukuru nabkuwapongeza, kwa sababu katika mikataba tuliyopitia, kwa mfano, mpaka sasa mkataba ambao unaonekana kuwa na maslahi makubwa kwa nchi ni *WARTSILA,* ambao ulifuata taratibu na sheria za manunuzi; lakini mikataba mingine yote, ina makosa, ina mambo ambayo si kwamba yamefanywa na wataalam makini. Kwa mfano, katika Mkataba wa *SONGAS* kifungu cha 3(10), kinatamka kwamba, *TANESCO* na *SONGAS,* yaani katika tafasiri kwa sababu tuliwatafuta pia hata wataalam wa kutusaidia *TANESCO* na *SONGAS,* walikubaliana na kutotekeleza masharti na matakwa ya kifungu cha 20(2) cha Sheria ya Umeme, Sura ya 131, Toleo la 2002 cha *Electricity Act Cap. No. 131 of the Law of Tanzania RE 2002* na badala yake kusuluhisha mgogoro baina yao, kwa kutumia utaratibu uliowekwa na mkataba.

Kwa hiyo, unaweza kuona kwamba, hata sheria tunazotunga, hazizingatiwi kama inavyopaswa na ndipo nilijiuliza kwamba, kumbe ndiyo maana sifa za Mbunge ni kujua

kusoma na kuandika; huyu Mbunge anayesimamia na kuwawakilisha wananchi, ambaye anatakiwa kutoa utetezi, anapowekewa sifa ya aina hiyo lengo ni kwamba, Mbunge ashindwe ku-*perform* na ashindwe kuona vitu kama hivyo. Kwa hiyo, ninaomba hata sifa za Mbunge pia ziangaliwe upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika Sheria hiyo inayokuja izingatie, kwa sababu kuna kifungu kinazungumzia katika Mkaba wa *Songas* na *TANESCO* kwamba, *TANESCO* haitabadilishwa na kuingizwa katika shughuli nyingine. Sasa vifungu kama hivyo, tunapotengeneza sisi Sheria zetu, wakati vifungu hivyo havijapata majibu ni tatizo. Ndiyo maana tunawaomba warudi kwenye Mikataba waipitie, waone, vifungu vyote vyenye utata viondolewe kwanza ili Sheria ikifika isiwe na utata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo kwa upande wa utaalam liliniudhi ni kwamba, inashangaza kuona kwa mfano, katika mkataba uliokuwepo, tukiichukulia tu *capacity charge* ambayo ni gharama kwa ajili ya mitambo ile iliyowekezwa bila kuangalia hapo kama kuna zile gharama za umeme wenyewe utakaotengenezwa. Katika mipango ile haikuangalia kama tunayo gesi ya kutosha ya kuweza kuendeshea hiyo mitambo Mpaka leo mara ya mwisho, tunapokea taarifa Mkurugenzi wa *Dowans* alituthibitishia kwa barua ambayo amewaandikia *TANESCO* kwamba, ile mitambo japo ipo hapa, hawezi kuendesha kwa sababu hana gesi. Sasa sisi tumeshawekeza hapa mitambo ambayo tunailipia *capacity charge*, wakati huo huo hatumpi yule mtu gesi, tunaanza tu kwenda kwamba, hapana unajua kwa sababu maji yana bei nafuu! Sasa kwa nini kama uliona hatuna gesi ya kutosha, tuwekeze vitu ambavyo vinatuingiza kwenye gharama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mkataba ule, wataalam wetu wanafahamu fika kwamba, bei ile ya kuuza umeme ambayo *Richmond Development Company LLC* alikuwa ame-*offer* kwa wakati ule, ilikuwa inatoa gharama ya *capacity charge* ya shilingi milioni 152 kwa siku kwa hesabu tulizofanya, ambazo kama kutakuwa na kupishana ni kidogo sana. Kwenye hesabu kuna *factors* ndogo ndogo kwa mfano, ile *maximum operating capacity* kuna *factor* ndogo ya kuangalia uhalisi, lakini kimsingi tunakuwa tuko ndani ya eneo hilo. Sasa huyu anayelipwa kiasi hicho kwa siku, wewe mtaalam una-*bargain* unasema usiponizalishia mimi utanilipa dola 10,000 tu. Mara ya kwanza wakati tunasikia, tuliona labda hiyo hela ni kubwa sana na hasa ukizingatia shilingi 5,000 kwa siku kwa matumizi ya kawaida, mtu unaona ni nyingi. Kwa hiyo, ukisikia dola 10,000 unasema hizo ni nyingi sana, kumbe baada ya kufanya hesabu ni sehemu ndogo mno.

Sasa tunajiuliza; wataalam wetu ambao mnafahamu na kwenye mikataba kunawekwa *formula* ambazo mtu wa kawaida huwezi kuziona; wewe kwanza kuchukua tu kalamu ukafanya *calculation* ukajua kutokana na kushindwa kuuza umeme ule ambao tunauza kwa sasa hivi kwa *average* ya shilingi 84 mpaka shilingi 87 kwa *unit* moja; kama ukipata umeme utauuza kwa kiasi gani ili uweze kujua eneo lako ni ya kiasi gani? Si hivyo tu, tunawauliza mlitumia kigezo gani? Aah! Unajua tulikuwa na c*onsultants*, wakatuambia ile *basic practice*, Nigeria sijui na wapi huko, unajua wana-*charge* kama

10,000! Kwa kigezo gani, hakuna; sasa wataalam wa aina hiyo bado tunawahitaji? *(Makofi)*

Hatuwezi kuendelea kuiendesha nchi yetu katika sura ya aina hiyo. Ndiyo maana, wananchi wameamua kuchukua hatua mkononi, wanaingia sasa mpaka kwenye siri za ndani huko za Serikali wanatafuta, kwa sababu ufumbuzi wa matatizo yao hauonekani. *(Makofi)*

Si hivyo tu, suala hili limemgusa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nilitegemea kwamba, tungeona angalau hata kuna barua moja inayotoka aidha kwa Waziri wa Wizara ile ya kumshauri kwamba, kutokana na jambo hili na hali halisi ya taratibu na sheria zilizopo, tukitumia njia hii inaweza ikatuletea matatizo, twende katika njia hii. Kwa hiyo ni mtu akishaambiwa bwana fanya hivi ni kwenda. Ninadhani lile neno wako mtiifu tuliangalie, kwa sababu tunatii hata mambo ambayo hayastahili kutii. Ninataka kuona kwenye Sheria ya Kazi, hakuna kifungu kinachomlinda mfanyakazi asitimize jambo ambalo anaona halina maslahi kwa Taifa. Ninadhani tuangalie pia na hizo sheria ni jambo la kusikitisha, wafanyakazi wa *TANESCO* walikuwa wameikataa Kampuni ile mara chungu mbovu lakini ilipofikia wameitwa kule hawajazungumza, wanapunguza tu vigezo wanasema hiyo hiyo! Kibaya zaidi, Sheria ya Manunuzi inaelekeza kwamba, kama umeichagua kampuni ambayo ime-*tender* kiwango cha chini cha pesa, basi muifanyie uchunguzi kama kiwango cha chini kimependekezwa tu ili mradi au kweli ndiyo bei halisi na huyu mtu ataweza kufanya kazi. Ili kuhalalisha kwamba, *Richmond* anapewa ile kazi, wakaamua kumfanyia utafiti wa kina. Kampuni ya *UPGUM* ya Ujerumani, ambayo nayo ili-*offer* kuzalisha megawati 100 kwa bei ya senti 5.4, lakini si kampuni ambayo wao wameamua kuipa kazi.

Hivi kweli kama mtu unaumwa, umeenda hospitali atapimwa mtu mwingine halafu majibu ya matokeo atibiwe mtu mwingine? Mimi ninaona hilo ni tatizo. Wanaoiangusha nchi hii ni pamoja na wataalam wetu, kwa kutojiamini. Unamwuliza mwanasheria; mwenzetu wakati una-*bargain* huu mkataba ulisimamia wapi? Anasema hapana hayo ni mambo ya Wahandisi, mimi nilikuwa nimeenda tu pale. Ulienda na lipi ? Makaratasi tulikuwa tumepewa pale pale. Kweli unaenda ku-*negotiate* mkataba kwa kukuta karatasi mezani ; hujapitia ukaona vifungu ambavyo vinakwaza ; una maana gani na kazi yako wewe kama Mwanasheria ni nini; kusoma lugha au kusoma vitu ambavyo vinaweza kupelekea kuwa na *repercussion* mbaya katika nchi yako? *(Makofi)*

Watu wanao-*bargain* wanajisahau, wanasimama upande wa pili wakati wao wanatakiwa wasimame upande wao ili wakutane kati, lakini ni tofauti kabisa. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu, tulijitahidi kwa kila hali, kuangalia ukweli uko wapi kwa sababu tulifahamu kazi hii ni ya hatari na itapelekea maisha yetu, lakini tulitaka historia iweze kujua ukweli uliotendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mtazamo wangu, ninaomba kusisitiza katika yale mapendezo yetu ; mikataba ipitiwe upya ili kuweza kuona upungufu na kujinasua lakini pia hata mikataba ya maeneo mengine, kwa mfano, ya maliasili, tupitie huko kuna vitalu vimeuzwa. Pia kuna mambo mengine ambayo tunazungumza hapa hayafiki mwisho,

kwa mfano, mara ya mwisho nilizungumzia suala la *TILDO*, halikupewa ufumbuzi mpaka leo. Imekuwa Wabunge kazi yetu kupiga makofi hapa, lakini tukitoa hoja zetu, Serikali hawazifanyii kazi kwa wakati. Hilo ni tatizo ; tunaomba tufikie mahali na sisi tunapotoa hoja zetu zizingatiwe ili ziweze kutoa matunda ambayo wananchi wanayatarajia. Si kwa sababu ya kumtuhumu mtu, lakini tunaamini kwa ushirikiano huo, Serikali, Bunge na Mahakama, vitasimama kama mihimili na nchi hii itakwenda. Ndiyo maana wakati taarifa yetu ikiwa kwenye mtambo wa kuja kuwasilishwa, kuna baadhi ya Wabunge walinisikitisha sana ; usiku walifanya kazi ya *lobbying* ya kusema kwamba, eti taarifa hii ipigwe vita. Wewe Mbunge unayewakilisha wananchi, kwa sababu zipi? *(Makofi)*

Mimi niliwasifu upande wa Serikali, kwa sababu pamoja na uchache wao, walijitahidi kujitetea wakasema siyo, lakini sisi huwa tunaunga mkono hata pale isipowekezana. Kuna siku nilipata neno baya kwa watoto wadogo; ninasema baya lakini ndio mwono wao ; waliniona ninapita wakasema wanafiki waseme ndiyo, ndiyo, walinigusa sana. Kwa hiyo, imefikia mahali tuondoke hapo, tuangalie maslahi ya nchi. Ninaomba nijifagilie kidogo ili kuonyesha kwamba, suala hili siyo la upinzani, wala siyo la CCM peke yao. Mimi ninaongea kama Mjumbe wa *NEC* wa CCM. Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe ni m-*NEC* wa CCM, walipoongea akina Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, tunawafahamu vyeo vyao; Makatibu, akina Mheshimiwa Zitto Z. Kabwe Manaibu. Kwa hiyo, hili ni suala la Kitaifa si suala la Chama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba niunge mkono kwamba mapendekezo yetu yafanyiwe kazi na kuwashukuru sana Serikali kwa kukubali kupokea mapendekezo yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya. Tuzidi kuombeana afya na uhai. Bunge litaendelea kuimarishwa, mtu asiyetaka shauri yake. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. SAVELINA S. MWIJAGE:** Mheshimiwa Spika, nami ninapenda kuchangia mada hii nzuri sana, inayonigusa moja kwa moja. Sisi pamoja na Wananchi, tulikuwa tunalilalamikia Shirika la *TANESCO* bure, sasa ninaishukuru Kamati hii kwa kazi nzuri. Ninapenda kusema kwamba, pamoja na shida ya umeme tuliyoipata Wananchi wa Mkoa wa Kagera, asiyeweza mdundo atupishe, leo imejionyesha dhahiri kabisa watupishe. Nimepata *bill* ya shilingi elfu themanini wakati taa zinazowaka ni za nje tu, je, huo ni uungwana? Watu wanatafuna nchi hivi hivi tunanyamaza, sasa hivi hatukubaliani kabisa na mambo hayo na tunaomba mafisadi wote waondoke.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza Kamati kwa kazi nzuri na ujasiri wa kutoogopa vitisho walivyonavyo Mawaziri. Ninaomba mafisadi wachunguzwe kiundani, pamoja na kujiuzulu, wana mambo mengi yatakayoendelea kutuathiri kwa mfano, Buzwagi, *Tanzanite*, Bulyanhulu, Geita, Serengeti, Ngorongoro, kwenye mbuga, sehemu ya maliasili na utalii, pamoja na Karamagi na makontena yake. Mikataba yote ni mibovu

sana. Nikiwa Mwanakamati, pamoja na wewe Mwenyekiti, ninafikiri tulizungushwa kuhusu mkataba huu mpaka Kamati ya wasamalia wema ilipoundwa.

Ninarudia tena kuwapongeza sana Wanakamati. Ningesema mengi lakini uzuri ni kwamba, wamejiuzulu. Mafisadi wakubwa msiogope kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja mia kwa mia, moja kwa moja kama Mwanakamati.

**MHE. ROSTAM A. AZIZ:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nami nichangie hoja ya Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge, iliyochunguza mchakato wa zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura, ulioipa ushindi *Richmond Development Company LLC* ya Huston Texas Marekani mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii katika ukurasa wa tisa, inanitaja kwa kueleza kuwa, niliitwa na sikufika kwa maelezo kuwa nilikuwa nje ya nchi. Ningependa Bunge lako Tukufu, liweke sasa kumbukumbu ya mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa mujibu wa kifungu cha 26 cha Sheria ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge, Sura ya 206 ya Sheria za Tanzania, Vikao vya Kamati hii ya Bunge, vilifuata taratibu za Kimahakama *(Judicial Proceedings)*. Utaratibu huu, unatoa haki kwa mtuhumiwa yeyote katika Kamati hiyo, kuelezwa tuhuma zinazomkabili na pia kupewa haki ya kujitetea dhidi ya tuhuma hizo, haki ya kuleta mashahidi na haki ya kuwasilisha nyaraka kama zipo.

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, nilipokea barua ya kuitwa na Kamati Teule, Tarehe 2 Januari, 2008, siku saba baada ya tarehe niliyotakiwa kuhojiwa na siku tatu baada ya Kamati kumaliza muda wake, ilikuwa tarehe 27 Desemba, 2007. Barua hiyo ilikuwa ya tarehe 2 Desemba, 2007, siku moja kabla ya *Christmas*. Kamati Teule, ilikuwa na muda wa kutosha zaidi ya siku 45, siamini kwamba, tarehe niliyotumiwa barua ilikuwa kwa bahati mbaya, kwa kuwa Wajumbe wa Kamati Teule, wanajua mazingira ya tarehe hizo kuwa ni ngumu barua kuwafikia walengwa mpaka sikukuu zipite.

Mheshimiwa Spika, ninafadhaika sana kuona Kamati Teule, inashindwa kupata wamiliki halali wa Kampuni ya *Dowans* na kujaribu kunipa mimi umiliki, eti kwa kuwa barua pepe waliyoitumia na sanduku la barua ni vya Kampuni ninayoimiliki. Umiliki wa kampuni ya biashara upo kisheria dunia nzima, mtu hamiliki kampuni kwa kampuni hiyo kutumia barua pepe, sanduku la barua au hata kupanga kwenye jengo lake. Pia watumishi wa kampuni yangu, wanaweza kushirikiana na kampuni yoyote ambayo kampuni yetu ina nia ya kufanya nayo biashara.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kulihakikishia Bunge lako kuwa, sina hisa wala umiliki wa aina yoyote kwenye kampuni hizi mbili na nina hakika Kamati Teule, inafahamu ukweli huu.

Mheshimiwa Spika, Kampuni yangu inajishughulisha na ujenzi na nimefanya miradi mingi ya ujenzi ndani na nje ya nchi. Kampuni yangu ni ya kibiashara na inakuwa na mahusiano na kampuni yoyote, ambayo inaweza kufanya kazi nayo kibiashara na kisheria.

Inashangaza sasa kwamba, Kamati Teule iliyoongozwa na Mwanasheria mahiri, imeona kutajwa na mashahidi kadhaa ambao Kamati inakiri hawakujitolea kwenda kutoa ushahidi ila Kamati Teule iliwaita kuwaomba watoe ushahidi, ndio msingi wa majumuisho hayo. Kama waliweza kuwajua na kuwapata watu wa kunituhumu; kwa nini wanikose mtuhumiwa? Nia na madhumuni ya Kamati yanatia shaka.

Mheshimiwa Spika, kauli mbiu yako ya kasi na viwango, haijadhihirika katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati Teule. Ulipobaini Kamati haijatoa mapendekezo kwa sababu ya muda kutotosha, uliwaongezea muda na upo ushahidi kuwa, Kamati ilikuwa ikiendelea kumalizia kazi zake mpaka wiki ya kwanza ya Bunge. Inashangaza sana kwamba, Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na wewe Mheshimiwa Spika, ambao kwa pamoja mlikuwa na wajibu wa kuhakikisha kila mtuhumiwa anatendewa haki, kwa kupewa haki ya kusikilizwa, mlipuuza haki hii ya msingi kabisa ya raia.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako likiwa chombo cha juu cha kutunga sheria, kwa namna yoyote, halipaswi kuwa taasisi inayotoa haki kwa wengine na kuwanyima wengine. Ninafadhaika sana, ninaumia sana na kwa kweli ninapata tabu kuelewa Bunge linaweza kuacha hali hii iendelee.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimalizie kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie na ninaamini Bunge lina wajibu wa kipekee kabisa wa kuwa kiongozi katika utekelezaji wa haki za raia.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, hoja hii nzito na ya kihistoria ni lazima itumike katika kulinda Uhuru, Haki, Usalama na Umoja wa nchi. Lazima tujue kuwa, hoja hii inaendelea kutumika kulinda *institution* na siyo kulinda mtu au kikundi cha watu. Ninaunga mkono hoja hii, lakini pia ninampongeza Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na Tume yake yote, kwa kazi nzuri sana waliyoifanya, kufichua ufisadi kama huu, ambao umeathiri sana uchumi wa nchi hii, ambayo watu wake wameendelea kuathirika kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maamuzi ya busara waliyoyafanya viongozi wetu, kukubali kuwajibika ni mwanzo mzuri kwa nchi yetu, kuanza kuwakumbusha wananchi wetu kuanzia sasa sura ya Bunge hili lazima ibadilike, kufuatana na mazingira ya Ari mpya, Nguvu mpya na Kasi mpya.

Mheshimiwa Spika, ninaomba sasa nishauri yafuatayo katika kufikia muafaka wa suala hili:-

1. Taarifa hii sasa iwasilishwe rasmi kwenye vyombo vya Mahakama kupitia Polisi ili kupitia Wataalam (Wanasheria) *independent* na siyo Mwanasheria Mkuu wa Serikali, waweze kuchambua yale yote ya kuwasilisha kimahakama.

2. Kuwajibishwa kwa Wanasiasa ama kujiuzulu kusiishie hapo, watendaji wote waliohusika katika mchakato kuanzia kuidhinisha manunuzi hayo, nao wachukuliwe hatua za kisheria za kibinadamu.

3. Mkataba ya *RICHMOND* ambayo ilikuwa hewa, ufutwe kisheria na kuagiza mikataba mingi kama hii ipitiwe na Kamati zetu husika ili kwa ile iliyoiingiza Taifa letu kwenye hasara, isitishwe na kufanyiwa marekebisho.

4. Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukakubali misingi ya Azimio la Arusha sasa ipitiwe na kuingizwa kwenye sheria zetu ili Agizo la Rais liwekwe kisheria, kutekelezwa na kuwa na nguvu za kisheria, katika hali hii lazima tukubali kurejesha misingi hiyo ili kujenga umoja.

5. Ninashauri kuwa kuanzia sasa, maeneo yote yenye utata, yasiwe yanasubiri Vyama vya Upinzani kuyawasilisha Bungeni, wakati ukweli mengi yanatoka ndani ya Serikali yetu ya CCM na sioni sababu ya sisi wenyewe, kutoyavalia njuga matatizo yetu na kuyaweka bayana katika kipindi hiki cha uwazi na ukweli.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii na kuwaomba Wabunge wote, waunge mkono mapendekezo hayo na yale ambayo yataongezwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu.

**MHE. MERYCE M. EMMANUEL:** Mheshimiwa Spika, ninapenda nichukue nafasi hii, kumpongeza au kuipongeza Kamati nzima, kwa kazi nzuri iliyoifanya na kutuletea taarifa nzuri, iliyokamilika, ikiwa na vielelezo na ninaiamini taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu sisi wenyewe tuliomba Kamati iundwe na wewe mwenyewe ukaiteua Kamati hiyo, nina imani kubwa na Kamati hiyo na ninaiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kutokana na vielelezo vya Kamati na mapendekezo yaliyotolewa, nami pia ninaomba kuunga mkono kuwa hatua za kinidhamu na kisheria, zikuchukue mkondo wake ili kurudisha imani kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushirikiano mkubwa aliouonyesha Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, ni kweli kwamba, alikuwa na taarifa nzuri za kampuni hii na ndiyo maana alikuwa jasiri kabisa wa kupiga simu akiwa nje ya nchi. Kutokana na kiapo tulichoapa hapa Bungeni, hata kama kulikuwa na shinikizo kutoka kwa Waziri Mkuu, alikuwa na uwezo mkubwa wa kukataa shinikizo hilo, kwani alikuwa ameapa kuwa mkweli na kuitetea nchi yake. Hivyo, ningependa kuiunga mkono Kamati kuwa, anahusika kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Ofisi ya Waziri Mkuu, ndiyo Msimamizi Mkuu wa Shughuli za Serikali; na kwa kuwa ndiyo mtoaji kauli wa mwisho; na kwa kuwa Waziri Mkuu mwenyewe, ndiye aliyekuwa akitoa msisitizo na taratibu zote za ufuatiliaji wa karibu na kampuni hiyo; ninaamini kuwa, Waziri Mkuu anahusika kwa karibu, kuliingizia Taifa hasara kubwa mno.

Mheshimiwa Spika, ili kurudisha imani kwa wananchi juu ya Serikali yao, ninaungana na kujiuzulu kwao, lakini pia ninaomba ufuatiliaji wa karibu ufanyike ili kujua *Richmond* ni ya akina nani na yupo wapi ili hatua zaidi zifanyike za kufidia gharama kubwa waliyoipata Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. CASTOR R. LIGALLAMA:** Kwanza, ninapenda kuipongeza Kamati Teule ya Bunge, iliyochunguza mchakato wa zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura, ulioipa ushindi *Richmond Development Company LLC* ya Huston, Texas – Marekani mwaka 2006, kwa taarifa nzuri yenye kujitosheleza.

Kimsingi hoja hii ni ya Wabunge wa CCM, kwa maana Wajumbe wanne kati ya watano wa Kamati hii Teule ni wa kutoka Chama cha Mapinduzi. Kuna usemi wa Kiingereza unaosemao kuwa: "*There is no responsibility without Accountability.*" Hayo yaliyotokea ni matokeo ya usemi huo.

Wananchi wetu hivi sasa, tangu sakata la *BOT* kuhusu *External Payment Arrears (EPA)*, wamepoteza imani na Serikali yao, kutokana na watendaji ambao kwa makusudi, wanakiuka taratibu za Serikali kuhusu zabuni na manunuzi kwa kuzingatia Sheria ya *PPRA* ya 2004. Serikali kupuuza ushauri wa kitaalam wa *PPRA* na badala yake kupindisha sheria ni dhahiri inaonyesha mwanya wa rushwa, ambao watendaji walijiingiza.

Ripoti imebainisha wazi kuwa, taratibu zote za zabuni zilikiukwa licha ya tahadhari ya baadhi ya watendaji waadilifu, kutahadharisha juu ya kukiukwa kwa sheria na kanuni za kuendesha mchakato mzima wa zabuni ya *Richmond.* Ripoti kwamba, Kampuni hiyo haikuwa na uwezo wa kufanya kazi ya kuzalisha umeme ni kiashiria tosha kuwa, zabuni hiyo ilitolewa kwa upendeleo, bila kuzingatia maslahi ya Watanzania ambao wanabeba mzigo wa huduma ya umeme. Malipo ya shilingi milioni 152 kila siku, kwa kampuni hii ya *Richmond* kutoka *TANESCO* ni mzigo mkubwa kwa wananchi.

Ninapendekeza wale wote waliohusika na kashfa hii wajiuzulu, ili kuiletea nchi yetu sifa na utekelezaji wa dhana ya Utawala Bora.

**MHE. FELIX N. KIJIKO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia hoja hii kwa kuanza kuipongeza Tume Teule, ambayo imeweza kufanya kazi nzuri ya kufuatilia ukweli wa mazungumzo yaliyokuwa yameenea nchi nzima na kuondoa imani kwa viongozi wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ninatoa pongezi kwa Kamati kwamba, imeweza kugundua ubovu wa baadhi ya vyombo, kutokufanya kazi kama inavyotakiwa. Mfano hai ambao Kamati Teule imeweza kugundua ni pale ambapo imeweza kugundua kwamba, badala ya chombo cha TAKUKURU kutafuta ukweli wa hali halisi, haikufanya hivyo na badala yake ilikuwa ni kukanusha taarifa kuwa haikuwa sahihi. Hali nzima ya *Richmond* ukweli wake ungepatikana mapema tu kama taarifa zingeifikia Serikali mapema. Hata hivyo, suala la *Richmond* likiwa mfano hai; suala la *BOT* lichunguzwe kwa umakini na kuchukua hatua za haraka ili kujenga imani kwa wananchi. Kwa makusudi mazima, Tume Teule iundwe kupata ukweli wa sakata zima.

Baada ya kusema haya machache, ninaomba kuunga mkono hoja na kuipongeza Kamati Teule kwa kazi nzuri.

**MHE. FATMA A. MIKIDADI:** Kamati ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda, imeweza kuweka hadharani madhambi yanayofanyika katika Wizara, ambayo yanachangia kuliangamiza Taifa. Serikali na Taifa, wanapaswa kuipongeza Kamati hii. Pamoja na Kamati Teule, inawezekana kabisa kuna Kamati nyingine ambazo ndani ya Wizara zake, huenda zina madhambi ndani yake, lakini hayatolewi nje mpaka wananchi wanaipigia kelele Wizara hiyo, kwa mfano, *BOT*, Fedha na kadhalika. Kwa hiyo, ninashauri kuwa, Kamati zozote zile zinapogundua kuwa ndani ya Wizara kuna madhambi, basi iwekwe wazi ndani ya Bunge, kwani Kamati ya Uwekezaji na Biashara imeshaonyesha njia ya kufanya.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kumpongeza kwa dhati, Mwenyekiti wa Kamati Teule, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mbunge wa Kyela, pamoja na Wajumbe wenzake, kwa kazi nzuri sana, ujasiri, umahili na uadilifu, waliouonyesha katika kutekeleza hadidu za rejea walizopewa na Bunge. Hongera sana na ninaunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati yako, imeleta taarifa nzuri sana na tumeipokea na kuikubali, lakini ninashangaa waliotajwa kuhusika na kashfa ya *Richmond*, badala ya kulilaumu Bunge na Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwa kupokea na kuikubali Taarifa hii, wanawalalamikia ninyi! Waache kuwaonea; lawama zao wazielekeze kwenye Bunge lenyewe na Kamati ya Kudumu ya Uwekezaji na Biashara, maana Kamati Teule ikimaliza na kuhitimisha hoja, Kamati hiyo haitakuwepo. Bunge na Kamati ya Kudumu ya Sekta hii itakuwepo na Bunge na Kamati zote, zitaendelea kuwashughulikia mafisadi wote hapa nchini.

**MHE. TEDDY L. KASELLA-BANTU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninapenda kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri, walioteuliwa na Rais, wakiongozwa na Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu. Aidha, ninampongeza Rais na Baraza lake jipya,hongera sana.

Mheshimiwa Spika, sina sababu ya kueleza mengi ambayo Waheshimiwa Wabunge wamesema. Yale yote waliyotueleza yameeleweka, cha msingi, lazima niende moja kwa moja kama ifuatayo: Kuzuia mara moja *TANESCO/*Serikali kuilipa kampuni

hewa ya *Richmond/Dowans.* Hakuna sababu ya kuilipa *Richmond* Sh. 150m kwa siku, kwa kazi hewa na kampuni hewa.

Mheshimiwa Spika, hii haina haja ya kwenda shule, kuwa na digrii ni busara tu; *why paying a company which is not there,* maana ni kitu cha ajabu sana? Ninaamini jambo la kwanza ni kuzuia kulipa hizo pesa ili tusiendelee kupoteza pesa za wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzuia hela hizi kupelekwa kwa kampuni hewa, Serikali isiishie hapo; iwatafute hawa *Richmond/Dowans* ni akina nani. Ninajua Serikali ina macho/masikio na ndio maana inaitwa Serikali; ichukue hatua kwa hawa watu waliokuwa wanalipwa pesa hizi kama kampuni ambayo haipo, lakini kwa kuwa walikuwa wanalipwa hivyo wapo in *brackets.* Hivyo, pendekezo langu ni kwamba, warudishe pesa zetu zote walizochukua, ikiwezekana na *interest* ili zirudi zifanye kazi nyingine.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, umeme vijijini; sisi wa Bukene/Ndala tumeukosa. Ninaomba pesa hizi zirudishwe, maana yangu washitakiwe na pia wafirisiwe tusioneane aibu, tunawatesa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, Waziri Mkuu na Mawaziri husika, wameachia ngazi, lakini pengine kuna Wabunge wafanyabiashara na kadhalika; ninaomba sheria ichukue mkondo wake. Wahusika wote hata kama ni Wabunge, washtakiwe na wafilisiwe, hakuna aliye *above the law*. Serikali isaidie, ifanye mambo mazuri ili pesa hizi zirudi na zifanye kazi ya kutuletea umeme vijijini, kikiwemo Kijiji cha Bukene, ambacho *in fact, budget* ilishapitishwa ikabakia fedha tu. Sasa fedha hizi zipo tupate umeme.

Mheshimiwa Spika, hawa waliotajwa wote na wengine, ninaomba wamwogope Mungu, wajiuzulu wote; Wabunge, *IPTL*, *Richmond/Dowans* na kadhalika na tusiwaonee huruma au aibu. Pesa zetu zirudi kabisa.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaipongeza Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Baada ya kuona matatizo yote yaliyotokea na kwa kutambua mzigo mkubwa wanaobebeshwa *TANESCO*, muhimu sana ninapendekeza Serikali Kuu, ichukue mzigo wa kulipia *capacity charges* zote mfano, *IPTL, SONGAS, AGGREKO, DOWAS/RICHMOND* na nyingine zote ili kuifidia *TANESCO* na gharama halisi tu.

Tuivunje Mikataba yote mibovu, kwani hata Taasisi za Kimataifa, haziungi mkono Mikataba inayonyonya wananchi na nchi yoyote. Vilevile waliohusika wote, washughulikiwe kwa mujibu wa sheria zilizopo. Daima tusiruhusu mikataba mibovu. Mwenyezi Mungu, azidi kutubariki Tanzania.

**MHE. USSI AMME PANDU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue nafasi hii, kuipongeza Kamati Teule ya Bunge, chini ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, kwa kazi nzuri waliyoifanya, kwa niaba ya Bunge hili na kwa niaba ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, ninaungana na Wabunge wenzangu, kuunga mkono hoja hii na kutaka zichukuliwe hatua za kisheria, kwa wale wote ambao wamehusika na wawajibishwe kama alivyowajibishwa Waziri Mkuu, pamoja na Mawaziri wawili.

Mheshimiwa Spika, pamoja na matatizo yote yaliyojitokeza na ukweli kujulikana kwamba, uhalali wa kuwepo na kuendelea kuwepo na Mkataba huo wa udanganyifu:-

1. Je, Serikali baada ya kugunduliwa udanganyifu huo, imeshachukua hatua ya kukatisha Mkataba huo?

2. Kama bado; je, zile shilingi milioni 152 ambazo zinalipwa kila siku zinaachiwa ziendelee?

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu, pamoja na Waziri Mkuu na Mawaziri kujiuzulu, ninaomba Serikali isitishe mara moja kulipa fedha hizo, pamoja na kusitishwa Mkataba huo wa *Richmond.*

Mheshismiwa Spika, ninaunga mkono hoja.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, ninaomba Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKUKURU), isitishwe mara moja. Wananchi hawana imani nayo, hapo hapo wao pia wapo kwenye suala la Mikataba ya Madini; kama waliweza kuongea uongo kuhusu *Richmond*; je, huko kwingine ndio wataongea ukweli?

Ninakubaliana kabisa na mapendekezo ya Kamati; watu wote waliohusika kwa namna moja au nyingine wawajibishwe, sio tu kujiuzulu; lazima washtakiwe wapelekwe Mahakamani na haki itendeke, kama hawana hatia basi ijulikane siyo kulalamika hawakutendewa haki. Hivi hizi fedha za *capacity charge* zilikuwa zinapelekwa wapi? Hizi ni fedha ambazo zingeweza kujenga barabara. Kwa mfano, nimekuwa nikilalamika kuhusu barabara za kuelekea kusini *(Southern Circuit)*, kwa ajili ya kutembelea mbuga za wanyama. Barabara zile ni mbaya sana, zingetengenezwa watalii wangekuwa wengi na hatimaye kuliongezea Taifa mapato.

Mheshimiwa Spika, kujenga darasa moja ni shilingi milioni saba, nyumba ya mwalimu ni shilingi milioni tisa. Swali la kujiuliza; haya mabilioni yanayolipwa kwa Kampuni hewa yangejenga madarasa na nyumba za walimu ngapi kwa kila Kata na bado fedha zingebaki? Inatia uchungu, wahusika wafunguliwe mashtaka wachunguzwe na wafilisiwe.

Mwisho kabisa, ninapenda kwa moyo wa dhati, kuipongeza Kamati Teule, kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa uadilifu na uaminifu mzuri. Ninaomba tuungane sote

kuupiga vita ufisadi na tuikomboe nchi yetu katika ufisadi uliopo katika kona ya Tanzania. Mungu ibariki Tanzania, tuzidi kuishi kwa amani na utulivu.

Mheshimiwa Spika, nininaunga mkono hoja hii.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na Kamati nzima, ambayo imefanya kazi kubwa na hatimaye kutoa taarifa kwenye Bunge lako hili.

Kwanza, ninaunga mkono mapendekezo yote ya Kamati. Pili, inaonekana *Richmond* ni kitu ambacho hakipo kisheria na hata *Bank Account* haina, wakati ilikuwa inalipwa fedha na Serikali! Hivyo basi ni vizuri Serikali ifuatilie na fedha hizo zote zirudishwe Serikalini.

Mwisho, ninaomba Serikali ilete kwenye Bunge, utekelezaji wa Taarifa ya *Richmond* kwa yale yote yaliyopendekezwa.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, tumejifunza kuwa, nafasi ya Waziri Mkuu kama Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, akiondoka Bungeni anakwenda kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wa CCM, kunapelekea nafasi ya Waziri Mkuu na Serikali, kuwabana Wabunge wasiwe na maoni humu. Chama kiliruhusu mjadala huu uwe wazi ili Mbunge achangie maoni yake. Chama kimerudisha heshima kubwa na hususan Wabunge wa CCM, machoni mwa wananchi.

Ninapendekeza Waziri Mkuu. asiwe Mwenyekiti wa Kamati ya Wabunge wa CCM. Aidha, Mwenyekiti achanguliwe miongoni mwa Wabunge au la awe Katibu Mkuu wa CCM na hiyo itahalalisha Ubunge wa Katibu Mkuu wa CCM.

Tumejifunza kuwa, kiapo cha utii kwa Rais unaofanywa na Baraza la Mawaziri hakitoshi. Kwa mfano, “... na kwa vyovyote vile sitatoa siri za Baraza la Mawaziri.”

Tumeona katika *issue* ya *Richmond*, Mawaziri wachache walikiuka maagizo ya Serikali, kwa kufanya mambo yao kinyume cha maagizo ya Baraza la Mawaziri. Hawakutoa siri ila walitumia *advantage* ya siri kufanya kinyume cha maamuzi ya Baraza la Mawaziri. Ninapendekeza kiapo kirekebishwe kwa kusema: “ ... Sitakiuka au kwenda kinyume na maamuzi ya Baraza la Mawaziri…”

Wahusika kwenye kashfa hii ni *Richmond;* ni matajiri sana, hatua zichukuliwe na Serikali kuzirejesha fedha zote walizochota.

Mkataba wa *Richmond* uvunjwe mara moja na ulipaji unaofanywa na *TANESCO* wa Sh.152m kwa siku usimamishwe mara moja, baada ya kudhihirika kwamba, kampuni hii ni ya kitapeli.

Ninaunga mkono taarifa na mapendekezo yote ya Kamati Teule ya Bunge, iliyochunguza ufisadi huu. Hii ni historia ya kipekee. Ninaomba kuwasilisha.

**MHE. ANIA S. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kuchangia kwa maandishi, Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge ya kuchunguza mchakato wa Zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura, kampuni ya *Richmond Development Company LLC* ya *Houston, Texas* - Marekani mwaka 2006.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, ninapenda kuipongeza Kamati kwa kazi kubwa waliyoifanya kufanikisha kwa uchunguzi ambao umeliokoa Taifa kuendendelea kupoteza fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Spika, Taarifa hii imekidhi haja na imekuwa wazi. Kwa maana hiyo, ninapenda kutoa maoni yangu juu ya kampuni ya *Richmond Development Company*.

Mheshimiwa Spika, wale ambao walihusika kwa namna moja katika kuipa ridhaa *Richmond Development Company* ili ikandamize Taifa la Watanzania, wachukuliwe hatua za kisheria na si vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, *Richmond Development Company LLC* na *Dowans Holdings S.A*, isimamishwe mara moja kuendelea na uzalishaji wa umeme. Mikataba yote ya *TANESCO* kati yake na *SONGAS*, *IPTL*, *AGGREKO*, *Richmond Development Company*, ipitiwe upya na iletwe Bungeni. Kama taarifa inavyosema ni kweli kabisa kuwa, utata usiofichika ili kuondoa hofu kubwa waliyopata Wananchi wa Tanzania na kuendelea kubebeshwa mzigo mkubwa wa malipo yasiyo ya lazima, bado umeme haujawafikia wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, uchunguzi wa TAKURU (TAKUKURU hivi sasa) ni aibu kubwa, chombo ambacho kinategemewa na Watanzania kuwaondolea kero ya rushwa; hawa ndio wala rushwa wa dhahiri kutokana na taarifa waliyoitoa. Kamati imeeleza wazi ufisadi uliofanywa na TAKURU (TAKUKURU). Ninapendekeza wale wote wawajibishwe, maana hawawezi tena kazi na majukumu makubwa waliyokabidhiwa, badala yake itakuwa ni kuwaonea sangara wadogo na wakubwa wakiachwa wakiendelea kuliangamiza Taifa. Wala rushwa wakubwa ndio adui wa nchi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba niungane na Kamati Teule, kwa kazi kubwa waliyoifanya na ninaunga mkono hoja.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, ninasikitika sana kwa kukosa nafasi ya kuchangia kwa maeneo (kusema), ndani ya Bunge lako Tukufu. Hata hivyo, nimeona kuna haja walau kuchangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, ni wazi viongozi hawa, wamekiuka taratibu zote za uongozi na uadilifu. Hivyo, ni vyema basi wawajibishwe na sheria ichukue mkondo wake, ikiwa ni pamoja na kufilisiwa. Kujiuzulu ni hatua moja, lakini hii haitoshi, inabidi

wanyang’anywe uanachama wa vyama husika na hivyo kama ni Wabunge, viti vyao vitangazwe viko wazi. Haiwezekani Wabunge wawe mafisadi na majambazi.

Mheshimiwa Spika, jambo hili si bahati mbaya ni makusudi, kwani walishauriwa kama inavyoonyesha katika ripoti na pia kutumia nafasi zao za uongozi na hasa umaskini wa Watanzania wakati tulipokuwa na matatizo ya umeme nchi nzima. Inasikitisha zaidi kuona wakati viongozi hawa wakijineemesha kwa kujipatia shilingi milioni 152 kwa siku, sawa na shilingi 110,960,000,000. Hii ni hatari sana kwani watu hawa si tu wameturudisha nyuma, bali wamewavunja moyo sana wananchi hasa katika suala zima la uchangiaji wa ujenzi wa shule na baadaye zahanati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TAKUKURU ni jambo la kusikitisha sana, kuona taasisi nyeti kama hii inaweza kupotosha umma kwa kiasi hicho kusema kwamba, *tender* ilikuwa shindanishi na upungufu ulikuwa mdogo tu. Hivi walisema hivi kwa manufaa ya nani; ina maana walitishwa na wahusika wa *Richmond?* Ninaomba TAKUKURU waulizwe kwa nini waliupotosha umma?

Mheshimiwa Spika, suala la aliyekuwa Waziri Mkuu, kulalamika kuwa hakutendewa haki *(Natural Justice),* linatia hasira kwa sababu alikuwa anaweza kabisa kwenda kwenye Kamati, hasa ikizingatiwa TAKUKURU ilishatoa ripoti ambayo ilimgusa, lakini mkuki kwa nguruwe, kwa binadamu mchungu. Mheshimiwa Edward N. Lowassa, jengo lile la Temeke, aliamuru yule Mhandisi afukuzwe kazi mara moja; je, yeye alizingatia *natural justice?* Ninakumbuka pia aliwahi kumfukuza kazi Mkurugenzi wa Halmashauri ya Same, kwa kushindwa kutoa taarifa ya hali ya tatizo la chakula; je, *natural justice* ilikuwepo?

Mheshimiwa Spika, lakini pia, nikiangalia ripoti hii inaonyesha wazi jinsi gani *TANESCO* na *PPRA* walifanya kazi nzuri na wanapaswa kupongezwa sana. Kuna taarifa kuwa, *Richmond* imenunua kiwanja Mtaa wa Malik karibu sana na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na wamejenga jengo kubwa sana kwa jina la *Richmond Tower*. Jengo hili lina ghorofa 13 na lina *apartments* sita kila *floor* na kila *apartment* ni *USD 2200* kwa mwezi. UDS 171,600 x 12 months x 1300 sawa sawa na shilingi 2,676,960,000 *per year*. Kama kwa mwaka wanapata bilioni mbili ni wazi wamejineemesha.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa kama taarifa hizi ni kweli au si kweli, Kamati ichunguze na kama ni kweli, jengo hili litaifishwe na liwe mali ya Serikali kwani Serikali haina ofisi. Lakini pia kuna jengo lingine karibu sana na *Richmond Tower,* ambalo litafunguliwa hivi karibuni. Ninaomba Kamati au Polisi wachunguze ukweli wa jambo hili.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia nafasi hii, kwa njia ya maandishi, kuipongeza Kamati Teule, kwa taarifa nzuri iliyotolewa mbele ya Bunge, ambayo inaonyesha wameifanya kazi hii kwa moyo, uaminifu mkubwa, bila woga na kumtegemea Mungu kwa maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, kwani aliimudu nafasi ya kiti na kielelezo kikubwa ni pale alipokuwa anawasilisha Bungeni alionyesha umahiri wa hali ya juu ni wachache wenye ujasiri kama yeye na Kamati yake.

Mheshimiwa Spika, ninampongeza pia Mheshimiwa Edward N. Lowassa, aliyekuwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha na Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, kwa uzalendo na ukomavu wa kisiasa, kwa kuwajibika kwao kwa maslahi ya Serikali ya CCM. Kitendo ambacho kimemrahisishia Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kufanya zoezi la kupanga Baraza la Mawaziri vizuri, sambamba na matashi ya Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Spika, maoni yangu, ninapenda kutoa wito kwa Wabunge wenzangu, wataalam wetu na Watanzania wenzangu, kuiga mfano wa Kamati kufanya kazi yoyote ambayo Serikali inaweza kukutuma kwa uwazi na ukweli ili kumsaidia Mheshimiwa Rais, kujenga nchi yetu na kuinua uchumi. Inadhihirisha wazi, kwenye Kamati hii hapakuwepo na mwanya wowote wa rushwa.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuishauri Serikali kuwa, mabilioni yaliyopotea ni mengi sana ni vizuri kufuatilia kujua yameenda kwa nani au wapi ili yarudishwe. Nina hakika, fedha hizo zikirudishwa, zitaweza kusaidia kuboresha sekta ya elimu kwa kuwalipa walimu madeni yote, kujenga nyumba za walimu, kuajiri walimu wengi, kujenga maabara na maktaba kwenye shule za sekondari hasa za Kata na kero nyingine tulizonazo.

Mheshimiwa Spika, ninawashauri wanasiasa wenzangu, wanapopata dhamana ya Serikali, tusiingilie masuala ya kitaalam wakati wataalam wapo. Kazi yao iwe ni kushauri, sio kulazimisha mfano, kusaini mikataba na kadhalika. Matumaini yangu ni kuwa, tukiheshimu taaluma za watendaji, hatutakuwa tunaifikisha Serikali mahali pabaya kama ilivyotokea.

Mheshimiwa Spika, ninapenda nimpongeze sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi alivyopanga Baraza lake la Mawaziri, hususan kwa kumteua Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda kuwa, Waziri Mkuu, tumefarijika sana. Amewatuliza watanzania wengi, ingawa bado kuna dukuduku kwa baadhi ya Mawaziri walioteuliwa, mimi ninawaomba Watanzania wenzangu, tumvumilie Rais wetu, kwani yeye sio Mungu, ataendelea kurekebisha kila inapobidi, hata Roma haikujengwa kwa siku moja.

Mheshimiwa Spika, ninaishauri sana Serikali juu ya ile Kamati ya TAKUKURU iliyopewa kazi ikaficha ukweli, ipewe karipio kali, kwani haikutumia nafasi yake vizuri na imepotosha ukweli na kuwafanya Watanzania kukosa imani na TAKUKURU. Hii ni dhahiri kuwa ilifanya kazi kwa nidhamu ya woga.

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii ya *Richmond* imeonyesha utapeli wa juu, ninaiomba Serikali isitishe Mkataba huu haraka, tusiendelee kupoteza fedha za walipa kodi kwa kiwango kikubwa kwa kampuni isiyojulikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikataba mingine; Mkataba wa *Richmond*, umetupa somo au darasa, ninaishauri Serikali kuwa, sasa wakati umefika wa kuipitia mikataba yote ili tujiridhishe uhalali wake na maslahi ya kila Mkataba kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wana imani kubwa na Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, hivyo basi, amepata mshauri mahiri sana, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. Tuna imani kubwa kuwa, mambo mengi ambayo yalikuwa ya kuzunguka au kumharibia sasa basi, adui hana nafasi.

Mheshimiwa Spika, ninawaomba Wabunge wenzangu na Watanzania wenzangu, tumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu, Waziri Mkuu na Serikali yote, katika kufichua maovu yanayoendeshwa kwa usiri wa hali ya juu, kwa lengo la kuififiisha nguvu Serikali ya CCM ili yabainike na kukomeshwa. Mungu libariki Bunge, Mungu mbariki Rais wetu na Tanzania. *Amina.*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, ninaunga mkono hoja hii. Pili, ninampongeza mtoa hoja, ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, kwa uwasilishaji mzuri na mahiri wa hoja. Tatu, kwa moyo wa dhati, ninataka niwapongeze Wanakamati wote kwa pamoja, kwa jinsi walivyo waaminifu wa wazalendo kwa nchi yetu, maana walichokipata ndicho walichowasilisha Bungeni bila mabadiliko. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, ninaomba ieleweke kuwa, hoja hii ni ya Bunge hivyo, ni yetu sote. Matokeo yake ni yetu sote. Kazi nzuri ya Kamati, imetufumbua macho na imesaidia kuondoa vichaka vya maovu ambavyo kimsingi haikuwa rahisi sisi kuyajua.

Mheshimiwa Spika, tumeiona hoja ya uwajibikaji kwa viongozi, japokuwa si lazima kila mmoja awe amehusika moja kwa moja. Vilevile tumeona kuwa makini na kila jambo hasa katika utumishi wa Serikali, itajenga nchi kwa staili ya kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. Viongozi na wananchi, wawe majasiri. Linapokuwa suala linalohusika ni la nchi, watu waache tabia ya kulindana.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo yangu ya kuiokoa *TANESCO* ili iishi na ifanye kazi yake ni kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iache kabisa kulazimisha mambo pale pasipowezekana.
(ii) Serikali iache kuingilia na kubadili taratibu zilizowekwa kisheria kinyemela.

(iii) Bunge lisitishe malipo ya *TANESCO* kwa *Richmond*, badala yake Serikali ibebe mzigo huo wa shilingi milioni 152 kila siku hadi mwisho wa mkataba.

(iv) Wawekezaji wengine wanaojulikana na tusiowajua sisi wakiwemo, *Songas, Aggreko, IPTL*- kwenye umeme/ nishati, wote walipwe na Serikali badala ya *TANESCO.*

*(v)* *TANESCO* iheshimiwe inapotoa ushauri kwa Serikali.

(vi) Vyombo vyetu vingine vitoe ushirikiano na viwe *smart* kutoa ushauri kwa wakati unaofaa mfano, TAKUKURU, Usalama wa Taifa na vinginevyo, navyo vidhibitiwe.

Ninarudia kuipongeza Kamati na Bunge letu kwa ujumla na ninalitakia kheri Baraza jipya chini ya Waziri Mkuu Mpya, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda. Ninaomba kuwasilisha.

**MHE. ALOYCE B. KIMARO:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuipongeza Kamati kwa kufanya kazi nzuri na kwa usiri mkubwa. Ninaunga mkono mapendekezo yote na ninaomba Serikali mpya ichukue hatua haraka.

Mheshimiwa Spika, ninaomba mkataba baina ya Serikali na *Richmond Development Company* usitishwe mara moja na wahusika wachukuliwe hatua za kisheria, kwa kuwa walidanganya. Kiingereza unaitwa *fraudulent misrepresentation,* hili ni kosa la jinai. Serikali iliyopita, kwa kupitia Wizara ya Nishati na Madini, ilisema kupata mkataba ni ngumu kwa kuwa gharama yake itakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, hawa wasingeweza kuufuta kwa kuwa dalili zote zinaonyesha ni mkataba uliotengenezwa kwa maslahi yao. Walidanganya ya kuwa wamefanya kazi nyingi Tanzania, kitu ambacho siyo kweli. Waliendelea kudanganya kuwa, wana uhusiano wa karibu na kampuni kubwa ya kimataifa ya *Pratt & Whitney,* kitu ambacho sio kweli. Hivyo, ni dhahiri kampuni inayodanganya haina sifa, kwa hiyo, mkataba usitishwe.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Mwanasheria Mkuu, Mheshimiwa Johnson P. M. Mwanyika, kama yeye, ninaona hana tatizo. Tatizo liko kwa wasaidizi wake aliowakuta na wenye uzoefu wa mikataba michafu na yenye dalili za rushwa. Ninapendekeza wasaidizi hao wafukuzwe wote ili wasiambukize wengine wasafi na vijana wapya.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ninamshauri Balozi Kazaura, Mwenyekiti wa Bodi ya *TANESCO,* ajiuzulu kwa kuifedhehesha Kamati Teule ya Bunge.

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa spika, ninaomba kwa dhati kuipongeza sana Kamati Teule, kwa kazi nzuri waliyoifanya.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kupendekeza yafuatayo:-

(a) Ninaunga mapendekezo yote ya Kamati kama yalivyoainishwa.

(b) Serikali isimamishe haraka (mara moja) mkataba kati ya *Richmond/Dowans* na Serikali, ili kuokoa Serikali kuendelea kulipa shilingi milioni 150 kwa siku.

(c) Serikali iwawajibishe wote waliohusika na ufisadi huu.

(d) Wale wote wanaohusika, mali zao zifilisiwe kulingana na kiwango cha upotevu wa mali ya umma.

(e) TAKUKURU waeleze ni kwa nini walitoa ripoti ambayo sio sahihi na walilazimishwa na nani ili kukiuka maadaili hayo.

(f) Kwa kuwa Mkataba wa *Richmond* na Serikali umeiingiza Serikali katika mzigo mkubwa wa kulipa madeni na hivyo kusababisha bei ya umeme nchini kupanda; ninapendekeza Serikali ione namna ambavyo itauchukua mzigo huu kwa wananchi; igharamie baadhi ya gharama, yaani Serikali itafute fedha kwenye vyanzo vingine ili kuisaidia *TANESCO.* Hii hatua inaweza kuisaidia *TANESCO* kupunguza bei za umeme.

(g) Mwisho, ninaomba kuchukua nafasi kuwapongeza sana viongozi wote waliojiuzulu ili kulinda maslahi ya nchi. Hakika huu ni mfano bora wa kuigwa na viongozi wengine.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

**SPIKA:** Sasa ninamwita mtoa hoja, Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE – MWENYEKITI WA KAMATI TEULE YA *RICHMOND:*** Mheshimiwa Spika, bahati mbaya upepo umepita asubuhi ya leo ninajisikia kukohoa, ningemwomba Mheshimiwa Mchungaji Dr. Getrude Rwakatare na wengine wanaojua kukemea, wakemee ili niweze kuwasilisha bila matatizo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ninaomba kuchukua fursa hii, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati Teule, kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki, kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuteuliwa kuwa Waziri Mkuu na baadaye kuthibitishwa na Bunge hili kwa kishindo. *(Makofi)*

Ninaomba vilevile nichukue fursa hii, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu, kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote, walioteuliwa siku tatu zilizopita na juzi kuapishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ikulu Ndogo ya Chamwino.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nisiishie hapo bila kumpongeza kwa dhati, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mbunge wa Monduli, kwa kuchukua uamuzi mgumu lakini wa kiungwana na wa kidemokrasia wa kujiuzulu wadhifa wa Uwaziri Mkuu katika kutekeleza dhana ya uwajibikaji. Aidha, ninampongeza vilevile Mheshimiwa Dr. Ibrahim Said Msabaha, Mbunge wa Kibaha Vijijini na Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini, kwa kuchukua uamuzi wa kujiuzulu nyadhifa zao za Uwaziri katika kutekeleza dhana hiyo hiyo ya uwajibikaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja iliyoko mbele yetu, imekaribisha jumla ya michango 58; michango 37 ya kusema na 21 ya maandishi. Ninaomba kwa ruhusa yako, niwatambue waliochangia kwa kusema kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Mheshimiwa Anne K. Malecela, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mheshimiwa Anna M. Komu, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa, Mheshimiwa George B. Simbachawene, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, Mheshimiwa Yono S. Kevela, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Mgana I. Msindai, Mheshimiwa Tatu M. Ntimizi, Mheshimiwa Grace S. Kiwelu, Mheshimiwa Charles N. Keenja na Mheshimiwa Ruth B. Msafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wengine ni Mheshimiwa Said J. Nkumba, Mheshimiwa Kabuzi F. Rwilomba, Mheshimiwa Magdalena H. Sakaya, Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mheshimiwa Beatrice M. Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Raphael M. Chegeni, Mheshimiwa Kabwe Z. Zitto, Mheshimiwa Dr. Guido G. Sigonda, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Magalle J. Shibuda, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, Mheshimiwa Said A. Arfi, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi, Mheshimiwa Mohamed Habib Juma Mnyaa, Mheshimiwa Lucas L. Selelii, Mheshimiwa Philip S. Marmo - Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Bunge na Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya. *(Makofi)*

Waliochangia kwa maandishi nao ni wengi na wote ni Waheshimiwa Wabunge, hivyo nitawataja majina: Mheshimiwa Meryce M. Emmanuel, Mheshimiwa Savelina S. Mwijage, Mheshimiwa Castor R. Ligallama, Mheshimiwa Rostam A. Aziz, Mheshimiwa Felix N. Kijiko, Mheshimiwa John P. Lwanji, Mheshimiwa Teddy L. Kasella-Bantu, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Ania S. Chaurembo, Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Ruth B. Msafiri, Mheshimiwa Aloyce B. Kimaro, Mheshimiwa Ussi Ame Pandu, Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mheshimiwa Dr. Binilith S. Mahenge, Mheshimiwa Susan A. J. Lyimo, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Mariam S. Mfaki, Mheshimiwa Khadija Salum Ally Al-Qassmy, Mheshimiwa Diana M. Chilolo na Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kukiri kuwa, michango ya Waheshimiwa Wabunge wote ilikuwa mizito na ya manufaa makubwa kwa mustakabali wa nchi yetu. Michango hiyo, imeichambua hoja kwa kina na kusaidia kuboresha maudhui ya hoja yenyewe hivyo, kutoa mwelekeo bora zaidi katika utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Februari, 2008, Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, aliahidi kuwa, mapendekezo yaliyomo kwenye Taarifa ya Kamati Teule, yatafanyiwa kazi na Serikali. Utayari wa kuyapokea mapendekezo ya Kamati Teule na kuyafanyia kazi, umeonyeshwa wazi vilevile na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kikao chake na Wazee wa Dar es Salaam jana. Kutokana na moyo huo wa viongozi wetu waandamizi wa nchi wa kutambua nafasi ya Bunge Kikatiba katika kuisimamia na kuishauri Serikali, sihitaji kuchukua muda mrefu kulishawishi Bunge lako Tukufu, likubali mapendekezo ya Kamati Teule, kama yalivyorekebishwa, kufuatana na Jedwali la marekebisho ambalo Waheshimiwa Wabunge wote mmekwishalipata.

Mheshimiwa Spika, nitagusia michango michache tu ambayo Kamati Teule inaamini ikiachwa bila kutolewa maelezo ya ziada**,** inaweza kupotosha ukweli wa hatua hii muhimu ya kihistoria katika maendeleo ya demokrasia nchini mwetu. Ninaomba nianze na mchango wa Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Mbunge wa Kibaha Vijijini, ambaye mbali na suala la *Letter of Credit (LC),* ambalo Mheshimiwa Herbert J. Mntangi alilitolea ufafanuzi wa kina sana jana, alilalamikia matumizi ya maneno kiburi na jeuri katika Taarifa ya Kamati, kuelezea tabia ya uongozi wa Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, tunasikitika ikiwa matumizi ya maneno hayo yamemkwaza Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha. Tunajiuliza; tungetumia neno gani ambalo ni zuri zaidi au bora zaidi ya hayo maneno, kuelezea hali ya uongozi wa Wizara kukaidi maelekezo ya Baraza la Mawaziri, kuipuuza Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, kuilazimisha *TANESCO* kusaini mkataba ambao vyombo vyake vya ndani vya maamuzi kisheria havijaupitia wala kuuona na kadhalika? Kwa hali hiyo, hata kama tungetakiwa kuiandika ripoti hiyo upya, tungeshindwa kukwepa kutumia maneno hayo hayo ambayo yanamkwaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha hakupendezwa nalo ni hatua ya Kamati Teule, kumpa pole mwandishi wa habari, Ndugu Said Kubenea na mwenzake Ndugu Ndimara Tegambwage, kutokana na tukio lililowapata la kushambuliwa na kuumizwa vibaya, kwani kwa maoni ya Mheshimiwa Mbunge, kutajwa kwa waandishi wa habari hao, kunaashiria uhusiano fulani kati ya mkasa uliowapata na suala la *Richmond.*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa, hatua tuliyochukua ya kuwapa pole waandishi hao wa habari, ilikuwa ni hatua ya kiuungwana tu na wajibu kwa Kamati, kutokana na ukweli kuwa, mwandishi wa habari, Ndugu Said Kubenea ni mmoja wa Watanzania wanne tu kati ya 75 waliohojiwa na Kamati Teule,

kwa hiari bila kupelekewa *summons.* Sasa wiki mbili baadaye, tulipata taarifa ya kushambuliwa kwake; ulikuwa wajibu wetu kumpa pole mwanahabari huyo na mwenzake wakati wa kuwasilisha taarifa ya Kamati kama tulivyofanya. *(Makofi)*

Kwa kumalizia, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, alijitolea kutusaidia kuiboresha Taarifa ya Kamati Teule. Tunamshukuru sana kwa moyo wake wa ushirikiano, ingawa sisi kama Kamati Teule, kazi yetu imekwisha na kwa uhakika hatukioni cha kurekebisha au kuboresha hapa. Ushauri wetu kwake ni kuisoma Taarifa ya Kamati Teule, kwa umakini zaidi ili kuondoa hisia zinazotokana na usomaji wa juu juu wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Mbunge mwingine ambaye mchango wake unahitaji maelezo ya ziada ni Mheshimiwa Rostam A. Azizi, Mbunge wa Igunga, ambaye amedai katika mchango wake wa maandishi kuwa, hakutendewa haki na Kamati Teule, kwa kumpelekea hati ya kuitwa tarehe 24 Desemba, 2007, kwani kufuatana na maneno yake; mazingira ya tarehe hizo ni magumu kwa barua kuwafikia walengwa kabla ya sikukuu kupita. Amedai vilevile kuwa, Kamati Teule ilikuwa na muda wa kutosha, kwa maneno yake mwenyewe "zaidi ya siku 45" kuweza kumtafuta.

Mheshimiwa Spika, hadidu za rejea ulizotupa, zilitutaka tumalize kazi yetu katika siku 45 na si zaidi ya siku 45 kama Mheshimiwa Mbunge anavyotaka ieleweke na siku 45 hizo zilijumuisha siku za Ijumaa, Jumamosi, Jumapili na siku za sikukuu, ambazo Mheshimiwa Rostam A. Azizi huwa anapumzika. Kwa maneno mengine, Mheshimiwa Spika, hukutenga pembeni siku za kwenda msikitini, kanisani na za kupumzika kwa Wajumbe wa Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, tarehe 24 Desemba, 2007 ilikuwa siku ya kazi, ambayo tuliitumia kusambaza hati za kuitwa za watu wanne akiwemo Mheshimiwa Rostam A. Azizi, kwa lengo la kuhojiwa na Kamati tarehe 27 Desemba, 2007, siku ambayo vilevile haikuwa ya sikukuu. Watu hao ni Ndugu Jamhuri Ngelime wa *TANESCO*, Ndugu Edward Hosea wa TAKUKURU, Mkurugenzi Mwendeshaji wa *Dowans Holdings Ltd.* na Mheshimiwa Rostam A. Azizi. Wote waliopelekewa *summons* walifika mbele ya Kamati tarehe 27 kama walivyotakiwa, kasoro Mheshimiwa Mbunge ambaye alipelekewa hati ya kuitwa nyumbani kwake *Oysterbay* na ndugu yake akaipokea kwa kusaini kwenye *dispatch book* ya Bunge na kumweleza mtumishi wa Bunge aliyepeleka hati hiyo kuwa, Mheshimiwa Mbunge alikuwa safarini nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, pale itakapobidi, tunaweza kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, ushahidi wa *dispatch book* ya Bunge na Hati ya Kiapo ya mtumishi wa Bunge aliyempelekea Mheshimiwa Mbunge *summons* nyumbani kwake, hati ambayo imesainiwa na Hakimu Mkazi wa Dodoma, kuthibitisha niliyoyasema.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rostam A. Azizi, amelalamika kuwa, Kamati Teule imembabikizia yeye umiliki wa Kampuni ya *Dowans* eti kwa sababu tu kampuni hiyo inatumia barua pepe na sanduku la barua la kampuni yake ya Caspian. Amejitetea

kuwa, ninamnukuu: "Pia watumishi wa kampuni yangu, wanaweza kushirikiana na kampuni yoyote ambayo kampuni yetu ina nia ya kufanya nayo biashara."

Mheshimiwa Spika, malalamiko ya Mheshimiwa Rostam A. Azizi, yanadhihirisha wazi kuwa, Mheshimiwa Mbunge hajaisoma Taarifa ya Kamati Teule. Mimi ninaamini anasimuliwa tu na wapambe au wasaidizi wake. Ninamshauri aisome yeye mwenyewe, asiogope unene wa hii taarifa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hakuna ukurasa kati ya kurasa 165 za Taarifa ya Kamati Teule, unaotamka kuwa, Mheshimiwa Rostam A. Azizi ni mmiliki wa *Richmond* au *Dowans.* Uchambuzi wa kina wa umiliki wa Kampuni ya *Richmond,* umefanyika kuanzia ukurasa wa 125 hadi wa 141 wa Taarifa ya Kamati; jina lake halijitokezi kwenye kurasa hizo!

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Kamati Teule, inamtaja Mheshimiwa Rostam A. Azizi katika ukurasa wa tisa, tena si kwa kumtuhumu bali kueleza kuwa, Kamati Teule haikuweza kumhoji kwa maelezo kuwa, alikuwa nje ya nchi. Taarifa inasema, Kamati Teule ilitaka kumhoji ili ajieleze kwa nini barua pepe na anuani ya posta ya kampuni yake ya Caspian, inatumiwa vilevile na *Dowans* na kwa nini baadhi ya wafanyakazi wa kampuni yake wanadaiwa kuifanyia kazi *Dowans?* Kamati Teule ilikuwa na maswali mengi ya kumwuliza zaidi ya hayo, kwa mfano, sababu zipi za msingi zilizomsukuma achukue jukumu la kuitafutia *Richmond,* kampuni ya ushauri ya uandishi wa habari *(G & S Media Consultancy),* ili *Richmond* iandikwe vizuri na vyombo vya habari vya Tanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile ametajwa ukurasa wa 38, kwa kunukuu matamshi nje ya kiapo ya shahidi ambayo Kamati Teule haikuyanzingatia kama ushahidi wa msingi.

Kwa kumalizia, Mheshimiwa Rostam A. Azizi, anadai kuwa ana ushahidi kuwa, Kamati Teule ilikuwa inaendelea kumalizia kazi zake mpaka wiki ya kwanza ya Bunge. Taarifa za uongo za aina hii, ziliwasababishia Wajumbe wa Kamati Teule, usumbufu mkubwa kisaikolojia, mwanzoni mwa Mkutano huu wa Bunge. Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati Teule, ninamtaka Mheshimiwa Rostam A. Azizi, athibitishe kauli yake hiyo ambayo hainidhalilishi mimi na wajumbe wenzangu wa Kamati Teule tu, bali vilevile Bunge lenyewe kwamba, linaendeshwa bila taratibu. Kauli hiyo ya Mheshimiwa Rostam A. Azizi, ambayo tayari imeingia kwenye mchakato wa kuingizwa kwenye *Hansard,* itakuwa na madhara makubwa kwa Bunge, ikiwa haitathibitishwa au kufutwa. Kwa kuwa Mheshimiwa Rostam A. Azizi simwoni Bungeni leo, nitaomba Mwongozo wako Mheshimiwa Spika kuhusu suala hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na taarifa vilevile kuwa, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini, hakupewa nafasi ya kusikilizwa na Kamati Teule. Taarifa hizo si sahihi, kwani taarifa rasmi za majadiliano na Kamati *(Hansard),* ambazo Waheshimiwa Wabunge mnazo, zinathibitisha kuwa, alihojiwa na Kamati Teule.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ambao unahitaji ufafanuzi tena wa kina ni ule uliotolewa na Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mbunge wa Monduli. Mchango wake ulisisitiza masuala makuu manne, ambayo bila kuyatolea ufafanuzi, yanaweza kutibua maana au maudhui ya mchakato wa kidemokrasia, tulioushuhudia katika siku za hivi karibuni hapa Dodoma. Masuala hayo ni kwamba, hakutendewa haki kwa kutopewa fursa ya kusikilizwa; kwamba, ushahidi wake muhimu wa barua aliyoiandika kwa Waziri wa Nishati na Madini, haukuzingatiwa na Kamati Teule; kwamba, shida ya Kamati Teule ilikuwa Uwaziri Mkuu aliokuwa nao; na kwamba, Kamati Teule imesema uongo Bungeni kwa kumsingizia.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nianze na utangulizi mfupi na rahisi; uwajibikaji kwa viongozi waandamizi katika nchi zinazolinda na kuenzi demokrasia kama vile Tanzania, una sura mbili; sura ya kwanza, kiongozi anawajibika kwa makosa yake mwenyewe ya kiutendaji. Kiongozi anafanya maamuzi mabaya, pengine kwa kishawishi cha pesa, maamuzi yake yakaleta hasara au kiongozi ameshindwa kutoa ushauri mzuri kama kiongozi, kwa kukiuka kanuni kukiuka taratibu na kadhalika, matatizo yakatokea anawajibika. Sasa sura hii ya uwajibikaji, inahusisha uvunjwaji wa maadili, kanuni, sheria, miiko ya uongozi na kadhalika. Chini ya uwajibikaji wa aina hii, kiongozi anaweza akashitakiwa, akaadhibiwa mbali na kuachia ngazi. Nitarejea kwenye sura hii hivi punde. Suala la msingi hapa ni kuwa, kuna *element* ya adhabu katika hii sura ya kwanza.

Sura ya pili; kiongozi anawajibika kwa makosa ambayo si yake moja kwa moja ila yaliyofanywa na watendaji chini yake. Kitendo cha kuwajibika kwa aina hii, kunaijengea Serikali au taasisi heshima na imani ya pekee katika jamii, kunatoa picha ya kwamba, uongozi unajali, unalielewa tatizo kwa kubeba lawama wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala hili la *Richmond*, Viongozi wa Wizara ya Nishati na Madini na Waziri Mkuu, walikuwa wanakabiliwa na uwajibikaji wa aina hizo mbili. Kwanza, uwajibikaji unaotokana na makosa ya viongozi wenyewe katika maamuzi yao, maelekezo yao, maagizo yao na kadhalika. Mawaziri wote wawili wa Nishati na Madini; aliyetangulia na aliyefuatia baadaye, Katibu Mkuu na Kamishna wa Nishati, wote tukawaona wana makosa ya moja kwa moja, waliyoyafanya wao kwa njia moja au nyingine. Kwa kuwa uwajibikaji wa aina hii, unatokana na ukiukwaji wa kanuni, taratibu, maadili, sheria na kadhalika, Kamati Teule ikahakikisha inawahoji wote ili kusikia *their side of the story* kabla ya kutoa pendekezo la kuwawajibisha kwa makosa waliyofanya. Ndiyo maana baada ya kuwahoji, tumependekeza hatua za kuchukuliwa dhidi yao.

Hali haikuwa hivyo kwa Waziri Mkuu; Kamati Teule ilikuwa na ushahidi wa mawasiliano ya karibu kati ya Waziri Mkuu na Uongozi wa Wizara. Ushahidi huo haukutosha kwa uwajibikaji wa sura ile ya kwanza wa kiongozi kukutwa na makosa ya moja kwa moja, aliyoyafanya yeye mwenyewe kwa njia moja au nyingine, lakini, ushahidi huo ulitosha kwa uwajibikaji wa sura ya pili, ambao hauhitaji mahojiano, kusikilizwa wala utetezi. Unawajibika kwa makosa ya watendaji walio chini yako. Hiyo ndiyo demokrasia. Wabunge wengi, wametoa mifano mingi hapa, ukiwemo wa Mzee

wetu Ali Hassan Mwinyi, alipokuwa Waziri wa Mambo ya Ndani; aliwajibika kwa makosa ya askari huko Shinyanga wakati yeye alikuwa Dar es Salaam; hatukumsikia akidai apewe nafasi ya kusilikizwa na hata kama angepewa, bado angewajibika yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati Teule, inatamka ukurasa wa 37 wa taarifa yake kuwa, ninanukuu: "Ushiriki huu wa karibu wa Waziri Mkuu katika kila hatua ya zabuni ya umeme wa dharura si lazima uwe ushahidi wa kwamba, kiongozi huyo wa Kitaifa alihusika katika kuibeba Richmond. Unaweza pia ukawa ushahidi wa *style* yake ya kawaida kabisa ya Waziri Mkuu katika kufuatilia masuala yote ya Kitaifa kwa karibu sana, tukizingatia kwamba, nchi wakati huo ilikuwa katika kipindi kigumu sana cha ukosefu wa umeme. Watu pekee waliokuwa wanaujua ukweli wenyewe, ukweli ambao ungeipa Kamati Teule msingi wa kumhoji Waziri Mkuu kwa kiapo."

Mheshimiwa Spika, ninaomba nirudie hapo: "Ukweli ambao ungeipa Kamati Teule msingi wa kumhoji Waziri Mkuu kwa kiapo ili awajibike kwa sura ya uwajibikaji wa kwanza, walikuwa watatu." Tunasema kwenye hiyo taarifa, Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Katibu Mkuu, Ndugu Arthur Mwakapugi na Mwenyekiti wa Bodi, Balozi Kazaura; viongozi hawa watatu kama tunavyosema kwenye taarifa ya Kamati ukurasa wa 37; walitamka chini ya kiapo kwamba, hawakupokea maagizo kutoka kwa Waziri Mkuu ya kuibeba *Richmond,* lakini baada tu ya kiapo; wawili kati yao wakatoa ushahidi wa kumuhusisha Waziri Mkuu. Kwa wale walisoma hii taarifa vizuri, Kamati Teule, haikuukubali ushahidi huo. Ukurasa wa 38 tunasema na ninanukuu: "Tumelazimika kuelezea hata mambo tuliyoelezwa kwa siri, kiungwana, in confidence, kutokana na uzito wa suala lenyewe na dhamana kubwa tuliyopewa na Bunge ya kuelezea kilichotokea kwa uwazi na ukweli. Ushahidi huu wa ziada na nje ya kiapo wa viongozi hawa wawili haukutoa msaada kwa Kamati Teule, kwa kuwa msingi wa maamuzi yote ya Bunge si minong'ono au tetesi, bali taarifa zenye uthibitisho halisi."

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa watatu, wangethibitisha kuwa Waziri Mkuu alikuwa anahusika, tungelimhoji kwa sababu ya kuvunja miiko, maadili na kanuni za sheria ya ununuzi wa umm,a kwa lengo la kupendekeza adhabu kwa Bunge mbali na kuachia ngazi. Hivyo, haki ya kusikilizwa ingelijitokeza hapo, lakini Kamati Teule iliona kuwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu, anawajibika chini ya sura ya pili ya uwajibikaji bila wasiwasi. Uwajibikaji kwa makosa ya walio chini yake, watu ambao wanapuuzia maamuzi ya Baraza la Mawaziri, wanapuuzia vyombo vilivyowekwa kisheria kwa mamlaka ya udhibiti wa ununuzi, wanavinyanyasa vyombo vya maamuzi ndani ya *TANESCO* na kadhalika. Halafu tulikuwa na ushahidi kwamba, wamekuwa na mawasiliano ya karibu na Mheshimiwa Waziri Mkuu, ndio maana Kamati Teule, haikupendekeza kuwa, Waziri Mkuu awajibike au awajibishwe; ilipendekeza katika ukurasa wa 163 kuwa, Waziri Mkuu apime mwenyewe uzito wa matokeo ya uchunguzi wetu na wajibu wake Kikatiba ndani na nje ya Bunge. Mwenzetu akapima akaamua kujiuzulu. *(Makofi)*.

Mheshimiwa Spika, fursa ya kujieleza Mheshimiwa Edwars N. Lowassa mbele ya Bunge hili na sio mbele ya Kamati Teule, tunachanganya hapo, ilikuwepo hakutaka

kuitumia kwa sababu zake mwenyewe, pengine alikuwa hajaisoma taarifa ya Kamati Teule vizuri. Sisi tuliamini alipopewa nafasi ya kwanza kuchangia hapa, angetumia muda huo kujenga hoja mbele ya Bunge kuwa, kaonewa na kushutumiwa visivyo kwa kuwasilisha mbele ya Bunge picha mbadala. Ndio maana alipoanza tu mimi na wenzangu wote tukakaa kunakili anachokisema kwa nguvu. Hakufanya hivyo, badala yeke ikageuka suala zima likawa la Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe na mbwembwe za kusoma taarifa na kushambulia uelewa wangu kuhusu *natural justice.*

Mheshimiwa Spika, sipendi kuingia huko, yamepita. Ninaomba nichukue fursa hii, kusisitiza kuwa, Kamati Teule ya Bunge, kimsingi ni chombo cha uchunguzi na si chombo cha maamuzi. *It is a fact finding organ for the National Assembly,* lakini maamuzi ni ya Bunge. Ndio maana Kamati Teule hupewa muda mfupi kukamilisha kazi zake. Kwa kuwa kazi yake kuu ni kufichua taarifa na takwimu zilizofichika na kulipelekea Bunge kufanya maamuzi, ndio maana Kamati Teule au Kamati ya Bunge, ikipata chochote haiitishi *press conference* na kusema tumeamua hivi ni Bunge lenye maamuzi ya mwisho.

Mheshimiwa Spika, uchukulie picha ya Kamati Teule kama Idara ya Upelelezi wa Polisi; umewahi kusikia mtu akidai hakupewa haki ya kusikilizwa na polisi? Mimi ninadhani hapana, kwa kuwa yote yanayokusanywa na polisi yanakwenda Mahakamani hivyo, unakwenda Mahakamani kudai haki ya kusikilizwa. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ninaomba nitoe angalizo kama Mwanasheria ambaye kwa kweli nimefundisha vijana wengi mno; wengine ni washauri, tena ninafikiri wote ni washauri wa Ofisi ya Waziri Mkuu, *Administrative Law* na *Constitutional Law.* Nitoe angalizo kwamba, pale ambapo Kamati Teule inaamua kufanya zaidi ya kuchunguza na kutoa mapendekezo kuhusu mtu fulani, basi wajibu wa kumhoji mtu huyo unajitokeza katika suala la Waziri Mkuu aliyepita, hatukutoa mapendekezo ya yeye kuwajibika au kuwajibishwa, tulitoa ushauri tu. Ushauri wenyewe ni wa kujipima. Suala la kwamba alikuwa na barua muhimu sana ambayo hatukuitilia maanani, lilijibiwa vizuri sana na Mjumbe wa Kamati Teule, Mheshimiwa Lucas L. Selelii kuwa, barua hiyo iliandikwa miezi kadhaa baada ya mchakato wa kuiteua *Richmond* kukamilika hivyo, isingesaidia kuboresha hali iliyokuwepo.

Mheshimiwa Spika, hoja ya kwamba, shida ya Kamati Teule ilikuwa Uwaziri Mkuu aliokuwa nao, ilitusononesha sana Wajumbe wa Kamati Teule. Hata hivyo, tuliamua kusamehe na kusahau, kwani kilikuwa kipindi kigumu sana kwa mwenzetu; hasira ilitawala busara.

Mheshimiwa Spika, kazi tuliyopewa na Bunge lako Tukufu haikuwa ya kuitafuta nafasi ya Uwaziri Mkuu, bali ukweli kuhusu *Richmond.* Ukweli huo umedhihirika ingawa kwa gharama ya baadhi ya wenzetu kujiuzulu na wengine wanasubiri hatua mbalimbali za uwajibishwaji. Hiyo ndiyo demokrasia na ni *achievement* kubwa kwa nchi yetu. Kauli yake kwamba, Kamati Teule imesema uwongo Bungeni kwa kumsingizia;

tumeamua kuisamehe na kutoifuatilia zaidi ili kuondoa mvutano usio wa lazima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema kuwa, Kamati Teule ilisikika kupitia vyombo vya habari, ikiwaomba Watanzania wote wenye taarifa zozote kuhusu *Richmond* wajitokeze; Kamati Teule ilisikika ikivutana na Viongozi wa Serikali katika kupata nyaraka ilizokuwa inazitaka; Mheshimiwa Edward N. Lowassa wakati huo akiwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Shughuli za Serikali Bungeni, hakushtuka wala kujali kuitikia wito wetu mpaka tunawasilisha Ripoti kwa Mheshimiwa Spika.

Kwa kiongozi ambaye Serikali yake ilikuwa inachunguzwa, ambaye yeye mwenyewe alikuwa magazetini mara kwa mara akishutumiwa kuhusika na uteuzi wa kampuni hiyo, kukaa kimya kusubiri afuatwe au aje aseme hakupewa nafasi ya kusikilizwa na chombo cha uchunguzi ni suala la kushangaza!

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia *rules of natural justice* kwa karibu sana, ambazo zina vipengele viwili wanasheria mnajua hapa; sio tu kusikiliza upande mwingine, lakini vilevile usiwe hakimu katika suala lako. Ndio maana Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya ikabidi ajiuzulu kutoka *TANESCO,* kukwepa kubanwa na *rules of natural justice.* Wengi ninaona wanaongea na vyombo vya habari *out of context,* ninaomba wapate ushauri tuwaelezee *rules of natural justice* ambazo zina sehemu mbili*; audi alteram partem* au *nemo judex in causa sua,* tunasema kilatini zinatumikaje, hata polisi utafute usikilizwe.

Mheshimiwa Spika, kutokana na michango mizuri mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, tulilazimika kufanya marekebisho kadhaa ya mapendekezo yetu na kuongeza mapendekezo mapya saba kama ifuatavyo na ningeomba niwaongoze Waheshimiwa Wabunge kwenye hayo. Pendekezo la kwanza halina mabadiliko; linasema, Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2004, haina nguvu ya kutosha ya kuwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma, kutekeleza majukumu yake ya kuhakikisha kwamba, ununuzi wa umma unaboreshwa kwa kuongeza ushindani wa ukweli na uwazi na hivyo kuipa Serikali thamani halisi ya pesa zake. Kamati Teule inapendekeza kwamba, Sheria hii ipitiwe upya ili kuiboresha kwa kuipa nguvu zaidi, udhibiti na uwezo wa kuchukua hatua pale sheria na kanuni zinapokiukwa, badala ya kutoa ushauri tu kama ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la pili halina mabadiliko. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma isiwajibike. Wizara ya Fedha ambayo nayo ni taasisi ya ununuzi *(Procurement Entity),* badala yake iwe chombo huru kinachowajibika Ofisi ya Rais na taarifa zake kuwasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tatu halina mabadiliko lakini nitasoma tu ule uamuzi badala ya kusoma na *background.* Kamati Teule, inatoa rai kwa Serikali kuwa, mikataba yote hii, ipitiwe upya mapema iwezekanavyo, yaani ya umeme kama ambavyo mikataba ya madini inavyopitiwa upya sasa na Serikali. Bila kufanya hivyo, mzigo mkubwa wa gharama za umeme utawaelemea wananchi na kushindwa kufikia azma ya Serikali ya maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la nne, lina marekebisho kama mnavyoona kwenye *schedule of amendments* na kwa hiyo itasomeka, Mkataba kati ya *TANESCO* na *Richmond Development Company LLC/Dowans Holdings S.A,* ulikuwa wa uzalishaji umeme wa dharura kipindi ambacho nchi ilikuwa katika hali ngumu ya ukame, uliokausha mabwawa yote ya uzalishaji umeme. Kamati Teule, inaitaka Serikali, kutathmini upya uhalali wa kuwepo kwa mkataba huo, kwa lengo la kusitisha malipo kwa *Dowans Holdings S.A,* na kuvunja mkatba huo mapema iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tano, halina marekebisho lakini linasomeka tu sehemu ya mwisho ya pendekezo lenyewe; "Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye katika majadiliano yake na Kamati Teule, alionesha kutokuelewa kabisa kilichokuwa kinatendeka na wasaidizi wake na Mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wakili wa Serikali, Ndugu Leonard Chidowu, ambaye ushiriki wake katika *GNT* haukuwa na tija yoyote, wawajibishwe na mamlaka ya juu ya nchi, kwa kuchangia kuiingiza nchi katika mkataba wa aibu."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la sita, lina marekebisho kama tulivyoonyesha kwenye *schedule of amendments* na itabidi isomeke kuwa: "Katika mikataba yote na makampuni ya nje, Serikali ihakikishe kuwa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA),* inatumika kikamilifu katika kupata taarifa kamili za makampuni hayo kama vile wanahisa, mitaji na anuani. Aidha, ofisi zetu za Ubalozi zilizo sehemu mbalimbali duniani, zihusishwe katika majadiliano na makampuni yanayotoka nje ya nchi, vilevile katika kuyachunguza makampuni hayo kwa lengo la kupata taarifa zao za msingi na kuboresha nguvu ya hoja ya Serikali."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la saba lina marekebisho na litasomeka sehemu ya mapendekezo tu mwishoni kwamba: "Kamati Teule inapendekeza kuwa, Wajumbe wote wa *GNT,* yaani *Government Negotiation Team,* ambao ni Maafisa Waandamizi wa Serikali, wawajibishwe mara moja kwa manufaa ya umma, kwa kulitia hasara Taifa kutokana na kushindwa kutumia elimu na ujuzi wao kulinda maslahi ya Taifa."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la nane halina marekebisho, lisomeke tu ile sehemu ya mwisho kwamba: "Hivyo basi, Kamati Teule inapendekeza kwamba, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Nazir M. Karamagi, aliyeshabikia sana uhalalishaji huo awajibishwe."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la tisa lina marekebisho na litasomeka kama ifuatavyo: "Kamati Teule, inapendekeza hatua zifuatazo zichukuliwe mara moja: Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU awajibishwe kwa manufaa ya umma na Maafisa wa TAKUKURU, walioshiriki katika zoezi hilo la uchunguzi na kuandaa taarifa hiyo, iliyoficha ukweli, nao pia wawajibishwe kwa manufaa ya Umma."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la kumi lina marekebisho, kwa hiyo, baada ya kubadilisha tarakimu ya fedha, litasomeka kwamba: "Gavana wa Benki Kuu, pamoja

Bodi ya Wakurugenzi, wachunguze kwa umakini uhalali wa malipo hayo na kuwachukulia hatua za kinidhamu waliohusika na uzembe huo."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 11 lina marekebisho na ukiingiza marekebisho hayo litasomeka kama ifuatavyo; sehemu ya mwisho: "Kamati Teule, inatoa rai kwa serikali kuanza rasmi, maandalizi ya majadiliano ya kina kuhusu suala hili ndani na nje ya Bunge kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali." Hili ni suala la Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 12, Serikali ijiepushe kadri inavyowezekana, lina marekebisho na lisomeke: "Serikali ijiepushe kadri inavyowezekana na utaratibu wa kutumia mawakala katika ununuzi wa umma na kuhakikisha kuwa, Wizara zina taarifa za bei halisi za mahitaji yao kila wakati ili kujiepusha na mchezo wa kawaida wa mawakala, kupandisha bei mara mbili au zaidi ya bei halisi."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 13, halina marekebisho ila lisomeke tu mwishoni kwamba: "Kamati zote za Bunge zihakikishe kuwa, zinapitia mikataba mikubwa na ya muda mrefu ya kibiashara chini ya sekta zao ili kuliondolea Taifa mizigo isiyo ya lazima. Pale ambapo upatikanaji wa mikataba hiyo unakwamishwa kwa urasimu usio wa lazima, Kamati zitumie utaratibu uliotumiwa na Kamati ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara ya kuunda Kamati Teule yenye ufunguo wa mikataba iliyofichika."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 14 hakuna marekebisho, ila isomeke tu mwishoni kwamba: "Kamati Teule, inapendekeza kwamba, Waziri wa Nishati na Madini wa wakati huo, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha na Katibu Mkuu, Ndugu Arthur Mwakapugi, wachukuliwe hatua kali za kinidhamu, kwa kuliingiza Taifa kwa makusudi kwenye mkataba na kampuni ya mfukoni, ambao umesababisha hasara kubwa kwa nchi. Aidha, Kamishna wa Nishati, Ndugu Bashir Mrindoko, naye achukuliwe hatua za kinidhamu, kwa kushindwa kumshauri Katibu Mkuu mpya wa Wizara, kuhusu udhaifu wa *Richmond* ambao ulijulikana dhahiri na Wizara toka mwaka 2004, kwenye mkataba wa bomba la mafuta."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 15 hakuna marekebisho. Isomeke vilevile kwamba: "Utaratibu wa kuteua Wakurugenzi na Makamishna katika Wizara kuwa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi za Mashirika yaliyo chini ya Wizara, unazua mgongano wa kimaslahi, kudhoofisha usimamizi na uwajibikaji hivyo, Serikali iupige marufuku mara moja. Mfano, Kamishna wa Nishati ni Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya *TANESCO*, ambaye alishiriki kwenye kikao kilichokataa wazabuni wote kuwa hawafai na kuishauri Serikali vilivyo, aliporejea Wizarani alishiriki katika kutengua maamuzi ya Bodi ya *TANESCO*."

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 16, hakuna marekebisho. Pendekezo hili lilimtaka Waziri Mkuu, ajipime; ninafikiri mnalijua?

Mheshimiwa Spika, kuna mapendekezo mapya saba yanaongezeka mlivyoona. La 17 linasema, *Richmond Development Company Tanzania Limited* ni kampuni ambayo

mmoja wa wanahisa wake ni kampuni hewa ya *Richmond Development Company, LLC.* Hivyo, kisheria, imekiuka masharti ya usajili wa makampuni. Kwa mantiki hiyo, Kamati Teule inapendekeza Msajili wa Makampuni, kuifuta kampuni hiyo mara moja kutoka kwenye orodha ya makampuni halali nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 18, kutokana na mfululizo wa vitendo vya udanganyifu kuhusu uwezo wa kifedha, kiufundi na uwezo wake wa katika masuala ya uzalishaji umeme, udanganyifu kuhusu usajili na uwepo wake kisheria kama kampuni halali yenye ukomo wa hisa nchini Marekani na Tanzania; upotoshaji wa makusudi kuhusu uhusiano wake kisheria na kampuni kubwa ya kimataifa ya *Pratt & Whitney* na kadhalika; Kamati Teule inapendekeza kuwa, wamiliki wa *Richmond Development Company, LLC* na *Richmond Development Company Tanzania Limited,* wafunguliwe kesi ya jinai mara moja, kwa udanganyifu na njama za kuiibia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kampuni hii ya *Pratt & Whitney,* imegundua kwamba, jina lake linachafuka na imeendelea kutuletea barua ikikana uhusiano kati yake na hiyo kampuni ya *Richmond.*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 19, Kamati Teule inaishauri Serikali kuviboresha na kuvitumia ipasavyo vitengo vya utabiri wa hali ya hewa na kitengo cha maji *TANESCO* ili kuiepusha nchi na maamuzi ya zimamoto, ambayo uzoefu unaonyesha yanaiingiza nchi kwenye hasara kubwa.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 20, Kamati Teule inaitaka Serikali iendeshe uchunguzi maalum, kubaini kama kweli taarifa rasmi ya *TAKUKURU,* iliyotoa matokeo ya uchunguzi kuhusu mchakato wa zabuni ya *Richmond,* ilikataliwa na kuharibiwa na kutolewa nyingine na kama kweli jalada halisi lililohusu kampuni ya *Richmond Development Company Tanzania Limited,* lililokuwa *BRELA* liliharibiwa na kuwekwa lingine kwa lengo la kuficha ukweli.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 21, Kamati Teule inaitaka Ofisi ya Bunge, ianzishe Maktaba Maalum itakayohusika na utunzaji wa mikataba yote inayoingiwa na Serikali. Kwa kuanzia, Kamati Teule inawasilisha mikataba sita ya umeme ya *IPTL, Songas, Aggreko, ALSTOM Power Rentals, Richmond Company Development Company LLC* na *WATSILA,* ianze kutunzwa katika Maktaba hiyo ili Waheshimiwa Wabunge waweze kufanya rejea kila wanapohitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 22, Kamati Teule inaishauri Serikali kuwa, Miswada yote inayowasilishwa Bungeni hasa ya umeme na mafuta, izingatie changamoto zilizoonekana katika ripoti hii.

Mheshimiwa Spika, pendekezo la 23, Kamati Teule inaitaka Serikali kufanyia kazi mapendekezo ya Kamati Teule na kuliarifu Bunge kuhusu utekelezaji wake ndani ya miezi mitatu toka tarehe ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ninakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge, nina hakika kwa niaba yenu, mtapenda nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati Teule ya Umeme wa dharura ya *Richmond,* kwa ufafanuzi na majumuisho mazuri na pia kuwasilisha mapendekezo. Hoja yake ameitoa na imeungwa mkono, sasa ninaomba muiamue. Nitatoa dakika chache tu, ninadhani mapendekezo yako wazi, kwa hiyo, nitatoa dakika chache kwa wale ambao wanataka kuchangia. *(Makofi)*

Ninaona yote yameungwa mkono. Nilikuwa ninasema hivyo kwa sababu nilipata makaratasi hapa yana mapendekezo, lakini ninaona yamewekwa vizuri ndani ya mapendekezo ya ziada yanajitosheleza. Walinileteа kutaka kurekebisha hapa na pale, ninadhani kwa mapendekezo haya ambayo yamekwisha kamilishwa na yamerekebishwa, tumepata msingi mzuri wa mapendekezo, unaotokana na zoezi hili la Kamati Teule na kazi iliyobaki ni kwa Serikali tu. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa muiamue hoja iliyo mbele yetu.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Mapendekezo ya Kamati Teule ya Bunge*
*yalikubaliwa na Bunge)*

**SPIKA:** Ninafurahi kuliarifu Bunge kwamba, mapendekezo yote ya Tume ya Umeme wa Dharura ya *Richmond*, yamekubaliwa na Wabunge wote ila Waziri mmoja ambaye sitamtaja. Kwa hiyo, mapendekezo haya yamepita. *(Kicheko/Makofi)*

Katibu kwa hatua inayofuata.

**ND. DAMIAN S. L. FOKA - KATIBU WA BUNGE:** Mheshimiwa Spika, ulikuwa umeomba tutengue Kanuni, labda ingefanyika hivyo.

Mheshimiwa Spika, shughuli zilizokuwa zimepangwa kwa ajili ya Mkutano huu wa Kumi zote zimekwishafanyiwa kazi, inayofuata sasa ni hoja ya kuahirisha Bunge.

## KUAHIRISHA BUNGE

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri Mkuu, ili atoe hoja ya kuliahirisha Bunge, ninatumia mamlaka yangu chini ya Kanuni ya 28(2) kwamba, endapo ikitokea kuwa shughuli zinaendelea; mathalani hotuba ikiwa ndefu kupita kipindi cha saa 07.00, inabidi niwahoji ili mkubali Bunge liweze kuendelea kukaa kupita ule muda wa saa 07.00 kwa kipindi kisichozidi dakika 30. Kwa hiyo, sasa ninaomba muiamue hoja ya kutengu kanuni hiyo.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Hoja ya kutengua Kanuni ili kuongeza muda wa Bunge ilipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imekubaliwa, kwa hiyo tutaendelea na shughuli hizi kupita ule muda wa kawaida kwa kipindi kisichozidi dakika 30. Kwa hiyo, kwa heshima kubwa na taadhima, ninaomba sasa kumwita Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu, aweze kutoa hoja ya kuliahirisha Bunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu. *(Kicheko/Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, kwanza, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutuweka salama hadi siku ya leo, tunapohitimisha Mkutano wa Kumi wa Bunge, ulioanza tarehe 29 Januari, 2008.

Pili, ninaomba niungane nanyi, pamoja na Watanzania wote, kutoa pole kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto, Marehemu Benedict Kiroya Losurutia. Aidha, ninampa pole Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, kwa kufiwa mke wake mpendwa na Mheshimiwa Richard S. Nyaulawa, kwa kufiwa mama yake mzazi. Tunaomba Mwenyezi Mungu, aziweke roho za marehemu wote mahali pema peponi, *amina.*

Nitumie nafasi hii, kumpongeza Mheshimiwa Mchungani Dr. Getrude Rwakatare, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Viti Maalum, kupitia Chama cha Mapinduzi. Tunampongeza sana na kumkaribisha hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru tena Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuniteua kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa imani yake kubwa aliyoionesha kwangu. Ninarudia tena kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge, kwa kunithibitisha kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kura nyingi hapa Bungeni. Aidha, ninawashukuru sana wananchi wote kwa moyo wao wa kuniunga mkono na kuwa na imani nami. Shukrani za pekee ni kwa Wananchi wa Mpanda Mashariki, ambao mimi ni mwakilishi wao. Ninataka niwashukuru sana wana-Rukwa wenzangu. Nimepokea pongezi nyingi, ninawashukuru sana. Ninajua kazi iliyo mbele yangu ni nzito na yenye majukumu mazito, lakini kutokana na imani kubwa mliyonionesha, ninaamini nitaweza. Ninachowaomba wote ni ushirikiano wenu, kwani wahenga walisema “umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu na kidole kimoja hakivunji chawa.” Ninarudia kusema, nitajitahidi sana kutowaangusheni na nitatumia uwezo wangu wote, kutimiza yale mnayoyatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nitumie nafasi hii pia kumshukuru kwa moyo wa dhati kabisa, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, Mbunge wa Monduli na Waziri Mkuu Mstaafu, kwa uamuzi wake wa busara wa kuamua kujiuzulu. Haikuwa kazi rahisi, ameonyesha ujasiri na heshima kubwa kwa Taifa letu. Kwa ujasiri mkubwa, alitamka

kujiuzulu kwa moyo safi. Aliyekuwa Waziri Mkuu wa Uingereza kati ya mwaka 1957 na 1963, Bwana Harold McMillan, aliwahi kusema: *"When the curtain falls, the best thing an actor can do is to go away."* Mheshimiwa Edward N. Lowassa, aliamua kujiuzulu kutokana na mapenzi yake kwa nchi yetu. Ninampongeza kwa ujasiri huo na hasa kwa kuonyesha jinsi sisi viongozi wengine, tunavyoweza kukabiliana na misukosuko ya kisiasa. *(Makofi)*

Ninadiriki pia kusema kwamba, Mheshimiwa Edward N. Lowassa, alikuwa ni kiongozi ambaye amejitahidi kuonyesha njia. Mwandishi wa vitabu na mtaalam wa masuala ya uongozi, Bwana John Maxwell, aliwahi huko siku za nyuma kusema: *"A leader is one who knows the way, goes the way and shows the way."* Mheshimiwa huyu aliijua njia, ameipita njia na kwa hiyo ameonyesha mfano na sisi wengine hatuna budi kuiga tunapokabiliwa na matatizo kama hayo. Ninamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri walioteuliwa na kuapishwa kuongoza Wizara mbalimbali. Uteuzi huu ambao umefanywa kwa umakini na Mheshimiwa Rais ni ishara ya kuonyesha matumaini makubwa aliyonayo kwa wale wote walioteuliwa. Wito wangu kwenu, Mawaziri na Naibu Mawaziri mlioteuliwa ni kufanya kazi kwa umakini, bidii, ushirikiano na kuweka mbele maslahi ya Taifa na Watanzania wote kwa ujumla. Changamoto kubwa kwa Mawaziri na Naibu Mawaziri ni kuwajibika zaidi na kuongeza kasi ya utekelezaji wa majukumu yetu. Sote tumesikia maelekezo ya Mheshimiwa Rais, aliyoyatoa kwetu tarehe 13 na 14 Februari, 2008, alipokuwa anawahutubia Wananchi wa Mkoa wa Dodoma na vilevile alipokuwa anazungumza na Wazee wa Dar-es-Salaam. Hatuna mbadala bali ni kuhakikisha utumishi wetu unakidhi matarajio ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninasimama mbele ya Bunge lako Tukufu, baada ya taratibu zote za kuteua Waziri Mkuu, kukamilika. Aidha, ninasimama hapa baada ya Mheshimiwa Rais, kukamilisha kuunda Baraza Jipya la Mawaziri. Sote tunakubaliana kwamba, Mkutano huu wa Kumi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, utabaki kuwa wa kihistoria katika nchi yetu. Matukio katika Mkutano huu, yameitambulisha nchi yetu kama nchi yenye kukomaa kidemokrasia na yenye Utawala Bora. Mkutano huu umeonyesha jinsi nguvu za mihimili mitatu zinavyofanya kazi. Aidha, Mkutano umeonyesha uwajibikaji na upeo mkubwa wa viongozi wetu katika kukubali demokrasia ifanye kazi kwa amani na utulivu. Tumetimiza yote yaliyomo katika Katiba yetu. *(Makofi)*

Huu ndio uthibitisho kwamba, Katiba yetu inaweza kutuongoza kukabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza. Ninapenda kutumia nafasi hii kumpongeza sana, Mheshimiwa Rais, kwa kufanya mabadiliko ya Baraza la Mawaziri kwa busara kubwa. Aidha, ninapenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi kwa ujumla, kwa kuonyesha utulivu mkubwa na upendo kwa nchi yetu na kwa kupokea mabadiliko haya kwa amani. Wito wangu kwa Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote ni kwamba, sasa sote kwa pamoja, tushirikiane na Serikali ili tuweze kuhimiza maendeleo. Masuala ya makundi kati yetu sasa yaishe na tufanye kazi kwa faida ya taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa Kumi, Bunge lako limepitisha Miswada mitatu. Miswada hiyo ni pamoja na Muswada wa kutoa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mfumo wa Mashtaka nchini wa 2007. Sheria hii inaweka utaratibu wa kusimamia na kuendesha mashtaka nchini kwa haki na kufuata misingi ya Utawala Bora. Muswada unaohusu Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Virusi vya UKIMWI nchini wa mwaka 2007. Sera hii imeweka bayana mambo mbalimbali katika kuzuia na kudhibiti maambukizi ya virusi vya UKIMWI nchini. Mwisho ni Muswada unaokusudia Kufuta Sheria ya Hoteli na Mawakala wa Hoteli kwa dhamira ya kuweka utaratibu mzuri katika kukuza biashara, utalii na kuimarisha na kuboresha usimamizi wa shughuli za utalii hapa nchini.

Ninapenda kuwashukuruni sana Waheshimiwa Wabunge, kwa michango yenu mizuri na hatimaye kukubali kupitisha Miswada hiyo. Michango yenu na ushauri wenu mlioutoa, itatumika katika kuboresha shughuli mbalimbali za maendeleo ya ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge pia limepata nafasi ya kuuliza maswali 145 ya msingi na mengi ya nyongeza, ambayo yote yamejibiwa kwa umahiri mkubwa. Vilevile katika Mkutano huu, Bunge lako Tukufu lilipitisha Azimio la Kumpongeza Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti Mpya wa Umoja wa Afrika, kwa kipindi cha mwaka mmoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, kuchaguliwa kwake kunaipatia nchi yetu nafasi kubwa ya kushughulikia matatizo yanayoikabili nchi za Bara letu la Afrika. Aidha, kuchaguliwa kwake, kutaipatia nchi yetu sifa ya kipekee katika kutoa mchango wake wa kuliongoza bara hili. Kazi hii ni ngumu, Watanzania tumuunge mkono na kumpa msaada wote unaohitajika katika kufanikisha majukumu yak. Viongozi na wananchi, sote tumwombe Mwenyezi Mungu, ampe afya njema, nguvu, hekima na busara katika kutatua matatizo mengi yanayoziandama baadhi ya nchi za Afrika na hasa majirani zetu.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu pia lilipata nafasi ya kupokea na kujadili taarifa ya Kamati Teule ya Bunge, iliyochunguza mchakato wa zabuni ya kuzalisha umeme wa dharura, uliyoipa ushindi *Richmond Development Company LLC* ya Houston Texas Marekani mwaka 2006. Ninaomba kuipongeza Kamati hiyo Teule ya Bunge, kwa dhati kabisa, kwa kazi nzuri waliyoifanya. Ninaipongeza kwa taarifa yake ambayo imeipa Serikali changamoto nyingi mbalimbali na sisi kama Serikali tumejifunza mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu wa kuunda Kamati Teule, upo kwa lengo la kuwezesha kuwepo kwa *checks and balances* ndani ya nchi yetu, hasa katika utendaji wa vyombo mbalimbali, lakini ni dhahiri utaratibu huu unapata mwanya wa kutumika inapobainika kuwa sheria, taratibu na kanuni mbalimbali zimepuuzwa na Serikali katika

utendaji wake wa kazi. Kwa hiyo, jibu sahihi kwa Serikali ni kufanya kazi kwa umakini na uadilifu mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninataka nikuahidi mbele ya Bunge lako hili kuwa, nitahakikisha timu hii mpya ya Mawaziri, inatimiza wajibu wake kama inavyotakiwa. *(Makofi)*

Kwa nini Serikali ifikishwe katika hatua ya kuundiwa Kamati Teule, wakati Serikali inao uwezo mkubwa na ina wataalam wa kutosha? Serikali katika hili, ninaamini haikutimiza wajibu wake vizuri. *(Makofi)*

Tarehe 13 Februari, 208, Rais ametuagiza tusiile nchi yetu ama kwa makusudi au kwa uzembe, kwani kwa kufanya hivyo ni kuwasaliti Watanzania. Kwa hiyo, dawa ya kweli kwa Serikali kuepuka kuundiwa Kamati Teule za Bunge ni kufanya kazi kwa uadilifu mkubwa na kutanguliza mbele uzalendo na maslahi ya Taifa letu, vinginevyo, Kamati hizi zitaendelea kuundwa tu. Serikali sasa hatuna budi kujipanga upya kwa maslahi ya wananchi wetu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati Teule ya Bunge, imetoa mapendekezo mbalimbali mazito, yanayotakiwa kufanyiwa kazi na Serikali na kwa kauli ya Mwenyekiti wa Kamati hiyo, wangependa kupata taarifa ya kazi hiyo ndani ya miezi mitatu. Ninataka kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, tutayapa uzito unaostahili mapendekezo hayo, kwa kuzingatia Katiba, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za nchi yetu. Kutokana na uzito wa masuala yenyewe, ambayo yamewasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu, nimelazimika kujiandaa ipasavyo na kwa hiyo, nimeunda timu ndogo ambayo ninataka ipitie kwa umakini na kujaribu kutuwasilishia mapendekezo ya namna ya kutekeleza maelekezo yote yaliyomo ndani ya Tume hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaijua nia njema ya Mwenyekiti wa Kamati yako, kutaka jambo hili liharakishwe na liwasilishwe mbele ya Bunge hili mapema iwezekanavyo, lakini ninaomba na mimi nilitahadharishe Bunge lako Tukufu kwamba, baadhi ya mapendekezo ni mazito na yanahitaji kuyaazimia kwa kina katika mpango wake wa namna ya kuyatekeleza. Yako ambayo tunaweza kuyatekeleza ndani ya kipindi kilichoombwa, lakini nitaomba radhi, kama itaonekana mengi mazito zaidi, itabidi pengine yaende mbele zaidi kidogo lakini yote tutakupa taarifa. *(Makofi)*

Timu hiyo ndogo nimedhamilia itokane na Wajumbe toka Ikulu, ambayo ni Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri; nitakuwa *senior* kutoka ofisini kwangu; ninataka nipate mtu mmoja kutoka Tume ya Mipango; mmoja kutoka Menejimenti ya Utumishi wa Umma; mmoja kutoka Bodi ya Wasajili wa Wakandarasi; mmoja kutoka Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi *PPRA;* mmoja TAMISEMI na mmoja kutoka Tume ya Maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaamini timu hii itafanya kazi kwa uharaka iwezekanavyo ili tuweze kuyachambua yote mliyotuwasilishia kama mapendekezo. Kwa kuzingatia michango yenu ambayo nimeiona, baadhi ni ya kina na tutatumia *Hansard* katika

kujaribu kuboresha uelewa wetu juu ya mapendekezo na hatua zinazostahili kuchukuliwa kwa kila pendekezo. Bunge lako kama nilivyosema, litaarifiwa hatua zote tutakazo kuwa tumezifanya, kadri muda utakavyokuwa unaenda.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa kauli hiyo, ninaomba niseme mambo mengine ya jumla ambayo yako kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka miwili tangu Serikali ya Awamu ya Nne iingie madarakani, tumefanya mambo mengi yenye mafanikio kwa maendeleo ya nchi yetu. Ninaomba hapa niseme machache, nianze na hili la elimu: Katika Ilani ya Uchaguzi, tumeahidi kushirikiana na wadau mbalimbali, kuimarisha elimu katika ngazi zote. Serikali kwa kushirikiana na wananchi, tumeweza kujenga shule nyingi zaidi za sekondari na idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kidato cha kwanza imeongezekana sana. Kwa mwaka 2006/2007, shule mpya 1,090 zilijengwa na kuwezesha wanafunzi 401,011 kuanza masomo ya kidato cha kwanza. Mwaka huu wa 2007/2008, jumla ya wanafunzi 419,136 waliofaulu mtihani wa darasa la saba, wanatarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Mheshimiwa Spika, lakini tumeanza vizuri kwa kutekeleza Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo; tumeongeza ruzuku ya mbolea kutoka shilingi bilioni saba mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 19.5 katika mwaka 2006/2007. Vilevile Mfuko wa Mkopo wa Pembejeo umengezeka kutoka shilingi bilioni 4.4 mwaka 2005/2006 hadi shilingi bilioni 5.6, kwa ajili ya kununulia matrekta mapya, mbegu bora, dawa za mimea na mifugo, pamoja na majembe ya mkono. Tutaendelea kusimamia kwa karibu, utekelezaji wa Programu ya Kilimo, pamoja na kusimamia kwa karibu, matumizi ya rasilimali zilizowekwa ili kuiendeleza Sekta hii ya Kilimo.

Tunayo malengo tuliyojiwekea kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005 katika Sekta ya Barabara. Ilani imetoa ahadi ya kukamilisha ujenzi wa miradi mbalimbali ya barabara inayoendelea, kwa kiwango cha lami na kujenga mpya. Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008, Serikali imeongeza bajeti ya matengenezo kwa takriban mara 2.5, ikilinganishwa na mwaka 2006/2007, ili kuzifanyia matengenezo barabara kuu za wilaya na za vijiji ili zipitike wakati wote. Serikali itaendelea kusimamia ujenzi wa miundombinu ili kuongeza kasi ya maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, bado ninayo imani kwamba, kila mmoja wetu anayo nafasi katika kujenga uchumi wa nchi yetu, kwa kutumia fursa zilizopo kikamilifu. Tumejiwekea majukumu ya kutekeleza kimikoa na kiwilaya, kwa utaratibu eneo moja zao moja *(one district one product).* Kwa maana hiyo, kila wilaya na halmashauri, zitoe kipaumbele katika shughuli inayofaa katika eneo lake. Aidha, nimeelekeza Wakuu wa Wilaya wote, kupeleka mipango yao ya kazi kwa Wakuu wa Mikoa ili kuonyesha majukumu yanayoweza kutekelezwa kwa ajili ya kuleta maendeleo katika maeneo yao. Lengo ni kutumia kikamilifu, fursa za kiuchumi zilizopo. Hakuna jambo gumu na lisilowezekana, kilichopo ni kuthubutu.

Moja ya changamoto zilizopo mbele yetu ni kukabiliana na tatizo kubwa la kushuka kwa ufaulu wa wanafunzi wanaomaliza elimu ya msingi. Takwimu za matokeo ya Darasa la Saba kwa mwaka 2007, zinaonyesha kuwa ni asilimia 54.112 tu ya wanafunzi 419,136 waliofanya mtihani wa kumaliza elimu ya misngi ndio waliofaulu. Kiwango hiki ni kidogo kwa asilimia 16.4, ukilinganisha na asilimia 70.51 ya wanafunzi 41,011 waliofanya mtihani mwaka 2006. Uchambuzi unaonyesha kuwa, mikoa iliyofanya vizuri ni Kagera asilimia 73.1, Dar es Salaam asilimia 71 na Iringa asilimia 69.5. Mikoa iliyofanya vibaya ni Shinyanga asilimia 34, Dodoma asilimia 40.7 na Mtwara asilimia 41.6.

Aidha, Halmashauri zilizofanya vizuri Kitaifa ni Manispaa ya Iringa asilimia 85, Chato asilimia 83 na Biharamulo Asilimia 83. Halmashauri zilizofanya vibaya Kitaifa ni Nanyumbu asilimia 17, Kondoa asilimia 21 na Tunduru asilimia 27. Hivyo, ni vyema kila Halmashauri, hasa zile zilizofanya vibaya, kuangalia sababu za kushuka kwa viwango vya wanafunzi kufaulu na waweke mikakati na kutekeleza mikakati hiyo kwa lengo la kupandisha viwango hivyo.

Mheshimiwa Spika, masomo yaliyochangia katika kushuka kwa ufaulu ni Hisabati ambapo ni asilimia 17.42 tu ya watahiniwa waliofaulu na Kiingereza ambapo ni asilimia 31.31 tu ya wanafunzi walifaulu. Takwimu hizi zinaonyesha kuwa, kuna matatizo katika masomo hayo. Hali hii haiwezi kuachwa iendelee, katika Karne hii ya Sayansi na Teknolojia, bila hesabu hatutafika. Hivyo, ninatoa changamoto kwa Wizara, kuweka mikakati ya kuinua kiwango cha wanafunzi kufaulu masomo hayo.

Nimepewa taarifa kuwa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, tayari imeunda Timu ya Wataalam, kufanya utafiti wa kubaini sababu za kushuka kwa kiwango cha ufaulu wa wanafunzi kwa mwaka 2007. Taarifa ya wataalam, inategemea kukamilika mwishoni mwa mwezi huu. Mategemeo yangu ni kuwa, timu hii itaanisha sababu za kushuka kwa kiwango cha ufaulu na kutoa ushauri makini kwa Serikali na njia ya kuondoka na tatizo hilo kwa baadaye.

Mheshimiwa Spika, wasichana waliofaulu mtihani wa kumaliza elimu ya msingi mwaka 2007 ni 377,110, sawa na asilimia 48.7 ya wanafunzi wote waliofanya mtihani huo, lakini ni wasichana 170,921 sawa na asilimi 40.8 tu kati ya wanafunzi 419,136 waliofaulu. Hali hii inaonyesha kutokuwepo kwa uwiano sawia wa wavulana na wasichana katika ufaulu. Kiwango cha ufaulu kwa wasichana bado ni kidogo sana, tofauti hii inaongezeka kadri wanafunzi hawa wanavyoendelea na masomo ya sekondari na vyuo. Hii ni kinyume na lengo tulilojiwekea kwenye Dira ya Taifa mwaka 2025. Sifa kuu ya kwanza ya maisha bora na mazuri, inaelezwa kuwa ninanukuu: "Ifakapo mwaka 2025 tofauti za rangi na kijinsia zitakuwa zimefutika na hivyo harakati za kiuchumi kutokuendeshwa kwa misingi ya rangi au jinsia. "

Kwa msingi huo, bado tuna changamoto kubwa ya kuongeza kasi ya kupunguza tofauti hiyo ili kuleta uwiano mzuri katika ngazi zote za elimu na makazini. Aidha, ile dhana ya kuwa ukimwelimisha mwanamke umeielimisha familia au jamii yote, tukiendelea hivi itapoteza maana yake au kutoweka kabisa. Hali hii inakinzana na Ilani

ya Chama cha Mapinduzi kuwa, rasilimali watu ndiyo nyenzo kuu ya maendeleo yote ya nchi. Hata mwanaharakati maarufu nchini Marekani, Bwana Martin Luther King, aliwahi kusema na ninatafsiri kwa kiswahili: "Taifa au ustaarabu ambao unaendeleza kuzalisha watu wenye elimu duni, linanunua kifo chake lenyewe kwa utaratibu wa kifo cha taratibu. "

Kupanda bei ya mafuta, zipo changamoto nyingi ambazo Serikali inaendelea kupambana nazo. Miongoni mwa changamoto hizo, moja ni matatizo yanayoukabili uchumi wa dunia hivi sasa, hasa ongezeko kubwa la bei ya mafuta yasiyosafishwa katika Soko la Dunia. Takwimu zinaonyesha kuwa, bei ya mafuta iliongezeka kutoka dola za Kimarekani 62.3 kwa pipa mwezi Desemba, 2006 hadi dola 97.12 kwa pipa mwishoni mwa mwezi Desemba, 2007. Hivyo, ni dhahiri kuwa, kupanda kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia, kumeathiri sana maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika nchi zote duniani; tajiri na maskini, ingawa nchi maskini kama Tanzania, zimeathirika zaidi.

Hali hii ya kupanda kwa bei ya mafuta katika Soko la Dunia, imesababisha gharama za uzalishaji wa bidhaa na utoaji huduma kwa wananchi kupanda sana. Vilevile, gharama za usafirishaji wa bidhaa na hasa vyakula na vifaa vya ujenzi katika mikoa mbalimbali zimeongezeka. Tanzania haizalishi mafuta hivyo, hii ni changamoto kubwa ambayo ipo mbele yetu ili kupunguza uchumi wa taifa letu, awali, Serikali iliondoa kodi ya ongezeko la thamani yaani *VAT,* kwenye mafuta yanayoingizwa nchini. Aidha, katika Mkutano wa Bunge, Serikali ilipitisha Sheria mpya iliyoipa nguvu Mamlaka ya Kudhibiti Nishati na Maji *(EWURA)*, kuweza kudhibiti kupanda kiholela kwa bei za mafuta nchini, baada ya kuwa na Soko Huria. Hivi sasa, *EWURA* imeanzisha mtandao wa kufuatilia bei za mafuta katika Soko la Dunia na kuzingatia katika vyombo vya habari ili kutoa ushauri kwa wanunuzi wa biashara hii na walaji.

Pamoja na hatua hizo, Serikali inaendelea kuhamasisha sekta binafsi, kuzalisha nishati mbadala kutokana na mimea hususan miwa, mawese na mibono-kaburi *(jetropha).* Vilevile Serikali inaendelea na jitihada za utafutaji mafuta na gesi asilia hapa nchini. Serikali ina matumaini kuwa, jitihada hizi zitawezesha kupunguza kwa kiasi fulani makali na athari za ongezeko la bei ya mafuta duniani. Hivyo, ni muhimu tuendelee kuwa waangalifu katika matumizi ya mafuta nchini na tuepuke matumizi yasiyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, hali ya chakula nchini hadi mwishoni mwa Desemba, 2007 ilikuwa ya kuridhisha kutokana na upatikanaji wa kuridhisha wa mazao hasa yasiyo ya nafaka, katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, kumekuwepo na upungufu wa vyakula vya aina ya nafaka hususan mahindi. Sababu za upungufu huu ni mwelekeo wa bei za vyakula hasa mahindi kuendelea kupanda na uingizaji mdogo wa nafaka hiyo katika masoko hasa maeneo ya mji.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanyika Desemba, 2007, ilionyesha kwamba, chakula kilichokuwepo kutokana na uzalishaji wa msimu wa 2006/2007, kilikuwa jumla ya tani milioni 10.66. Aidha, takwimu hizo zilionyesha kwamba, uzalishaji wa mazao ya chakula ungefikia tani milioni 11.02 mwaka 2007/2008, wakati mahitaji ya chakula kwa

mwaka 2007/2008 ni tani milioni 10.09 na hivyo kuwezesha taifa kujitosheleza kwa chakula katika mwaka 2007/2008 kwa asilimia 106.

Mheshimiwa Spika, kulingana na tathmini hiyo, uzalishaji wa mazao ya nafaka ulifikia tani 5,422,208, wakati mahitaji ya nafaka ni tani 6,251,117 na hivyo kujitokeza kwa pengo la takriban tani 828,909. Hata hivyo, uzalishaji wa mazao yasiyo nafaka, uliofikia tani 5,238,093 wakati mahitaji ni tani 3,782,357, umesababisha kuwa na ziada ya tani 1455,726 za mazao yasiyo nafaka, hali ambayo inaondoa pengo la uhaba wa nafaka na kuwa na ziada ya tani 626,817 za chakula nchini.

Mheshimiwa Spika, kupungua kwa nafaka hususan katika maeneo yanayozalisha mahindi kwa wingi, kumesababisha kupanda kwa bei ya mahindi nchini. Aidha, kupanda kwa bei ya nafaka kwa kasi, kumesababishwa na kuongezeka kwa matumizi ya nafaka duniani katika uzalishaji wa nishati. Hali hii inasababisha uhaba wa mahindi yanayoweza kuagizwa kutoka nje ya nchi. Kutokana na hali hii, haitegemewi kwamba, bei za nafaka katika Soko la Dunia zitashuka katika muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hali ya upungufu wa nafaka uliojitokeza, Serikali imechukua hatua zifuatazo:-

Moja, kusimamisha kwa muda uuzaji wa mazao ya nafaka hususan mahindi na mchele kwenda nchi za nje hadi Mei, 2008. Hatua hii itasaidia chakula kilichopo nchini, kuendelea kupatikana na pia kupunguza kasi ya kupanda kwa bei.

Pili, kuondoa ushuru kwa waagizaji wa zao la mahindi kutoka nje ya nchi. Lengo ni kupunguza uhaba wa nafaka kwa kipindi hiki hadi Mei, 2008 ambapo mazao mapya yataanza kuingia sokoni. Aidha, tani 300,000 za mahindi, zimeruhusiwa kuingizwa nchini bila kodi kati ya kipindi cha Januari hadi Mei, 2008.

Mheshimiwa Spika, tarehe 16 Novemba, 2007, Serikali iliieleza Bunge lako Tukufu juu ya changamoto zinazolikabili Taifa letu. Moja ya changamoto hizo ni uimarishaji wa masoko ya mazao ya wakulima, hususan kupitia Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Utaratibu huu umelenga kuwasaidia wakulima, kuondoa walanguzi wa kati katika soko. Aidha, kwa kutumia mfumo huu, wakulima wamewezeshwa kutumia mazao yao kama dhamana ya kupata mikopo kutoka Benki wakati wanasubiri bei za mazao yao ziwe nzuri. Ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, mafanikio ya mfumo huu yameanza kuonekana na ninaomba nitoe mifano: Katika Mkoa wa Mtwara; hali ya ununuzi, usafirishaji, mapokezi na mauzo ya zao la korosho katika maghala makuu zimeboreka sana. Taarifa za maendeleo ya ununuzi wa zao hilo hadi tarehe 2 Februari, 2008, zinaonyesha kuwa kiasi cha tani 59,210 kimenunuliwa kutoka katika maghala makuu. *(Makofi)*

Mheshimwa Spika, malipo kwa wakulima kwa awamu yalifanyika kama ifuatavyo: Kiasi kilichonunuliwa na vyama ni tani 59,852 kwa bei ya shilingi 610 kwa kilo; Malipo ya awamu ya kwanza yalikuwa asilimia 60 ya mauzo ambayo kila mkulima alipata kwa bei ya awali ya shilingi 366 kwa kilo. Jumla ya shilingi bilioni 21.9

zilitolewa; Jumla ya malipo awamu ya pili ya asilimia 40 ya bei ya mauzo na ambayo yanaendelea kulipwa kwa bei ya shilingi 244 kwa kilo ni shilingi bilioni 14.6; na malipo yaliyolipwa hadi sasa ni shilingi bilioni 2.4, sawa na asilimia 16.3 ya malipo ya awamu ya pili.

Mheshimiwa Spika, katika kulipa malipo ya awamu ya pili, Wilaya ya Mtwara imelipwa asilimia 72.9, Nanyumbu asilimia 51.6, Masasi asilimia 29.0, Tandahimba na Newala bado hawajaanza kulipwa. Kuchelewa kupata malipo ya awamu ya pili kwa Wilaya hizo, kunatokana na jinsi Wilaya zilivyopokea kwa haraka utaratibu wa kutumia mfumo huu wa stakabadhi ya mazao. Wilaya zilizowahi kuukubali utaratibu huu, ndizo zilizoanza mchakato na hivyo kuanza kulipwa mapema.

Mheshimiwa Spika, malipo ya awamu ya pili, yanaendelea kulipwa na vyama vya msingi. Aidha, baadhi ya wanunuzi wanaendelea kukamilisha malipo ya fedha benki na benki kuendelea kuziingiza fedha hizo kwenye hesabu za vyama husika, ndipo vyama viweze kuchukua na kufanya malipo. Kwa maana hiyo, Wilaya zote zitapata malipo ya awamu ya pili kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mafanikio hayo, baada ya malipo ya awamu ya pili kukamilika, kikosi kazi *(Task Force)*, kitakaa na kuangalia mwenendo wa soko na kuainisha jinsi gharama za zao hili zilivyokuwa. Matarajio ni kwamba, baada ya kuainisha gharama hizo, mapendekezo ya kulipa kwa kila malipo ya awamu ya tatu yatatolewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kusisitiza kuwa, utaratibu wa stakabadhi wa mazao ghalani, unawezekana ni wa uhakika na ni mzuri. Tunajua wapo waliokuwa na mashaka kwamba, mfumo huu usingefanikiwa, lakini takwimu zinaonyesha mafanikio makubwa ya mfumo huu. Tumejaribu kwa zao la korosho na tumeona mafanikio. Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, mara zote alisisitiza kwamba, inawezekana kabisa kutimiza wajibu wako. Tumejaribu mfumo huu na tumeona kuwa unawezekana kutumika. *(Makofi)*

Nitumie nafasi hii, kumshukuru Mheshimiwa Rais, aliyetembelea Mikoa ya Kusini na kuagiza kuwa, mfumo wa ununuzi wa korosho ubadilishwe ili kutumia vyama vya ushirika, badala ya wanunuzi binafsi ambao walikuwa wanawadhulumu wakulima. Jukumu sasa ni la wakuu wa Mikoa na Watendaji katika maeneo yenye mazao yanayofaa kwa mfumo huu, kusimamia kikamilifu utekelezaji wa zoezi hili. Tusirudi nyuma, tuwasaidie wakulima, tuwaelimishe waelewe ili wafaidike na mfumo huu tuliouanzisha, ambao unaongeza kipato ili nguvu zao zisipotee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda nigusie kidogo hali ya ushirikiano katika Jumuiya ya Afrika Mashariki, hususan baada ya kutangazwa matokeo ya uchaguzi nchini Kenya. Nchi yetu ni mdau mkubwa katika Jumuiya hiyo. Tumekuwa na mipango mingi ya pamoja, ambayo imekuwa ikiendelea kwa ajili ya kuiimarisha Jumuiya hii kwa maendeleo ya nchi zote zinazohusika. Hali ya amani na utulivu nchini Kenya, baada ya matokeo ya uchaguzi mkuu hususan ya Rais ni muhimu katika kuimarisha Jumuiya hii.

Ninapenda kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, Jumuiya hii ni ya wananchi. Shughuli za jumuiya zinaendelea na mikutano muhimu kwa ngazi ya wataalam inaendelea kufanyika kule Arusha. Aidha, pamoja na hali tete iliyoko nchini Kenya, ukanda wa usafiri kwa njia ya barabara kutoka Nairobi hadi Arusha na Mombasa kuingia Tanga, uko shwari na salama. Wafanyabiashara wanaendelea na shughuli zao kama kawaida. Tunawaombea wenzetu wa Kenya, waunge mkono juhudi za kutafuta muafaka ili kurejesha amani na utulivu katika nchi yao. Kurejeshwa kwa amani katika nchi hii, kutazisaidia nchi wanachama wa Afrika Mashariki, kama ndugu, kurejea katika hali ya kawaida ya kujiletea maendeleo katika nchi zao.

Mheshimiwa Spika, iko hadithi ya bwana mmoja, aliyepewa kazi ya kukata mbuyu na tajiri wake. Bwana huyu akaanza kuukata mbuyu ule asubuhi na mapema kwa kutumia shoka butu. Hata hivyo, baada ya kutumia saa kadhaa kukata mbuyu ule na kwa kutumia nguvu nyingi sana hadi mchana, hakuweza kuuangusha. Basi mpita njia mmoja, ambaye pia ni rafiki yake, kwa kuona vile akamwambia bwana yule, rafiki yangu unatumia nguvu nyingi hivyo; kwa nini usilinoe shoka lako? Bwana yule akajibu sina muda hata wa kunoa shoka hili ni lazima nikate na kuangusha mbuyu huu ifikapo kesho asubuhi!"

Nasi kama taifa, muda hautungoji; tuna matatizo na changamoto nyingi; maendeleo hayana subira; hivyo, tunao wajibu basi wa kutumia muda mdogo uliopo kwa umakini, ufanisi na kwa tija kubwa. Kila linalowezekana leo lisingoje kesho. Tukifanya hivyo, tutaweza kuokoa muda wetu kwa kutumia saa chache zilizopo kwa mfanikio makubwa katika maendeleo ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema kwamba, mkutano huu ulikuwa wa kihistoria; utawekwa kwenye kumbukumbu za Bunge lako Tukufu, ambazo zitahitajika kwa vizazi vijavyo. Yote tuliyopata nafasi ya kushiriki kuyajadili tumejadili na yale yenye kuhitaji maamuzi tumefanya.

Vile vile, yale yenye matokeo tumeyaona. Mwanazuoni mmoja, Bwana Ralph Bunche aliandika: "*To make our way, we must have firm resolution, persistence and tenacity. We must gear ourselves to work hard all the way. We can never let up!*

Sote tunakumbuka mazingira yaliyojitokeza, yaliyoleta mtikisiko wa aina yake katika nchi yetu. Ninarudia kuwaombeni kwa dhati kabisa, sasa sote tuondoke hapa Bungeni na dhamira moja kuwa, yaliyopita si ndwele, tugange yajayo. Twendeni sasa tukashirikiane na wananchi kufanya kazi, turejeshe ushirikiano na mshikamano. Tuwasaidie na kuwaongoza wananchi kutatua matatizo yao. Tusibaki tunapoteza muda kwa kutafuta wachawi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuwashukuru wote waliotuwezesha kukamilisha shughuli zilizopangwa kwenye Mkutano huu wa Kumi, kwa ufanisi mkubwa. Ninakushukuru wewe Mheshimiwa Spika, kwa kuongoza kwa umahiri mkubwa, hasa mjadala uliokuwa mbele yetu. Ninawashukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu, kwa kutuongoza na kusimamia vizuri shughuli zote zilizopangwa katika mkutano huu. Ninarejea kuwashukuru Mawaziri na Naibu Mawaziri

waliotutangulia, kwa mchango wao. Ninawashukuru watumishi wa Serikali, ambao tumekuwa nao hapa Dodoma, kwa kazi nzuri. Ninawashukuru pia waandishi wa habari, kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuwafikishia wananchi yale yote yaliyojitokeza hapa Bungeni. *(Makofi)*

Kama nilivyokwisha kuwaahidi kwamba, nitatoa ushirikiano wa karibu kabisa kwa vyombo vyote vya habari, hasa katika kutoa habari ambazo zinaashiria ujenzi na usimamizi mzuri wa utendaji ndani ya Serikali, ni dhahiri tumeweka historia ya pekee kwa jinsi mambo yote yalivyoshughulikiwa kwa amani na utulivu.

Hii ndiyo demokrasia ya kweli na huu ndio Utawala Bora. Ninaamini kabisa huu utakuwa mfano wa kuigwa na nchi nyingine duniani na hasa Afrika katika kushughulikia matatizo ya ndani ya nchi zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, shukrani za pekee ni kwa Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yenu mbalimbali, ambayo imeisaidia Serikali katika kutekeleza majukumu yake. Mwisho, ninamshukuru Katibu wa Bunge na Wasaidizi wake. kwa huduma mbalimbali zilizofanikisha Mkutano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninarudia kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, ofisi yangu itasimamia kikamilifu, hatua zote stahiki katika kuhakikisha kwamba, mapendekezo yaliyopitishwa na Bunge lako Tukufu, kufuatia taarifa ya Kamati yako Teule yanazingatiwa na kutekelezwa na hatimaye kuwasilisha taarifa ndani ya Bunge lako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, basi niwatakie safari njema na ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa hadi Siku ya Jumanne, tarehe 8 Aprili, 2008, saa tatu asubuhi litakapokutana tena hapa Mjini Dodoma.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwa hotuba nzuri sana ya kuahirisha Bunge, imejaa matumaini, imeweka mwelekeo wa ushirikiano mzuri na Waheshimiwa Wabunge na tunakutakia afya njema. Ninadhani kwa *style* hiyo, nchi yetu inaweza kupata maendeleo ya haraka zaidi.

Waheshimiwa Wabunge, hoja hiyo imetolewa na imeungwa mkono, lakini kabla ya kuwahoji, nina maneno machache ya kusema. Niliombwa Mwongozo wa Spika na Mwenyekiti wa Kamati ya *Richmond*, kuhusu matamshi ya Mheshimiwa Rostam A. Aziz; kwa kuwa hayupo, haitakuwa haki, basi nitatoa nafasi hiyo kwenye Mkutano ujao wa Kumi na Moja ili aweze kutoa ufafanuzi. *(Makofi)*

La pili, kuhusu mikataba; uamuzi wa Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyestaafu, tulikwishakubaliana tutakuwa na nafasi maalum ndani ya Jengo la Utawala, ambapo

mikataba yote ambayo tunaihitaji, itawekwa kwa ajili ya rejea ya Waheshimiwa Wabunge.

Ninapenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, ndani ya Maktaba ghorofa ya pili, tunatenga sasa chumba maalum, ambapo kuanzia hii mikataba ambayo Mwenyekiti wa Kamati Teule ametupatia, itawekwa mle na kuanzia hapo utaratibu utakuwa kwamba, Katibu wa Bunge kwa niaba ya Mbunge yeyote ambaye anahitaji mkataba, msiwaandikie Mawaziri moja kwa moja, haiwezekani.

Hivyo, Mbunge yeyote ambaye ana shida na Mkataba wowote wa Serikali, basi afikishe ombi hilo kwa Katibu wa Bunge, Katibu ataomba kwa niaba ya Bunge na Mkataba huo katika siku si nyingi sana utafikishwa pale katika Mikataba Maalum, ataarifiwa na Wabunge wote wataarifiwa kwamba mkataba huo upo ili waweze kufanya rejea na kuuangalia.

Huo ndiyo utaratibu, tunaomba ushirikiano upande wa Serikali kwa sababu amekwishasema Waziri Mkuu, sasa kama itakuwa tena kuzungushana, itabidi twende kwenye Kamati ya Maadili, yeyote anayehusika ndiyo utaratibu. Waziri au Katibu Mkuu chini ya Sheria ya *Powers and Privileges*, sasa tutampeleka kwenye Kamati ya Maadili ili aweze kushughulikiwa. *(Makofi)*

Ninawashukuru sana kwa kikao kizuri, niwakumbushe tu kwamba, kwa mujibu wa Kanuni ya 29(3), mara baada ya hoja hii kukubaliwa, tutabaki tumesimama ili tuweze kuimba Wimbo wa Taifa. Kwa hiyo, sasa nitawahoji, muiamue hoja ya kuahirisha Bunge.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, ninaliahirisha Bunge hadi Siku ya Jumanne tarehe 8 Aprili, saa tatu asubuhi, hapa Dodoma.

**WIMBO WA TAIFA**

*(Hapa Wabunge Waliimba Wimbo wa Taifa)*

*(Saa 07.10 mchana Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 8 Aprili, 2008, Saa Tatu Asubuhi)*